# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS

## MWATATE CONSTITUENCY, HELD AT

## MWAKINYUNGU ACK CHURCH

## ON

**THURSDAY, 2nd MAY 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MWATATE CONSTITUENCY HELD AT ACK MWAKINYUNGU CHURCH**
**ON THURSDAY, 2nd MAY 2002**

**Present**

Com. Abubakar Zein Abubakar
Com. Prof. Wanjiku Kabira
Com. Keriako Tobiko

**Secretariat In attendance**

Fatuma Jama - Program officer
Onesmus Kipchumba - Assistant program officer
Alice Thuo - Verbatim recorder
Nancy Odipo - Sign language interpreter

**The meeting was called to order at 9.30 a.m.**

**Com. Zein:** Habari ya asubuhi. Kwa niaba ya Tume ya kurekebisha Katiba ya Kenya, ningependa kukitambua kikao hiki kama kikao rasmi cha kukusanya maoni ya Wakenya, ili kurekebisha Katiba yetu. On behalf of the Constitution of Kenya Review Commission, I would like to declare this as an official formal gathering of the people of Kenya for the purpose of reviewing our Constitution. Kabla sijaenda mbele kwa kawaida ya ada yetu, huwa tunaanza na maombi lakini kwanza ningetaka kumuomba mwenyekiti wa 3 C's, ile kamati ya sehemu ya uakilishaji bungeni inayohusika na mambo ya Katiba, aje kutuanzia mkutano wetu huu rasmi. Bwana mwenyekiti. Yeye ni mwenyekiti wa kamati hiyo. Na kama mnavyojua pia yeye ni mwenyekiti wa baraza. Karibu mwenyekiti.

**Chairman CCC's:** Asante sana Bwana Commissioner na Commissioners wale wengine. Nafikiri kabla hatujaenda mbele sana, kama kawaida yetu sisi ni watu wa Mungu, ningemuomba madam Ngati atufungulie kwa maombi mafupi. Karibu.

**Madam Ngati:** Asante Bwana chairman, chairman wa baraza la county council, na pia chairman wa kamati ya 3 C's. Asante sana kwa kunipatia fursa hii ya kufungulia watu kwa maombi, natuweze kuanza mambo yenye yametuleta hapa. Tuinamishe vichwa na tuombe.

(**Prayer in Kitaita**) kwa vizazi vyetu vinavyokuja na vizazi vilivyoko saa hii. Baba tunaomba hasa tunapoendelea kurekebisha

Katiba hii yetu, iwe ni ya kutufaa sisi vizazi vya saa hii na vizazi vinavyokuja Baba. Naomba hayo kwa jina la Yesu Kristu Bwana wetu. Amina.

**Chairman CCC:** Asante sana. Ndugu Ma-Commissioners na wale wote ambao mumeandamana nao kutoka Nairobi, nataka kuchukua fursa hii kusema karibuni sana. Eneo hili ni Mwakinyungu ACK, iko ndani ya tarafa ama eneo la ubunge la Mwatate. Mbunge wetu ni Mheshimiwa Marsden Madoka ambaye ni waziri wa uhusiano wa nchi za kigeni. Tungekuwa naye hapa lakini kwa shughuli nyingi basi ndiyo hatunaye. Lakini pia ana uhuru wa kuja wakati wowote.

Niko na members wa committee na ningeomba members wa committee hii ya Mwatate 3 C's wasimame, nikianzia na Tom, secretary wetu. Labda kwa kukomboa wakati, nitataja tu pahali walipo. Tuko na Secretary Tom Mwachumbi, yeye ndiye mwandishi wa Mwatate 3 C's, na yuko pale mlangoni. Yeye ndiye anafanya ile general registration. Niko pia na Loise Mwambela. Niko pia na Stephen Maganga kutoka Ronye juu na tumemkuta hapa. Niko pia na huyu Madam Ngati ambaye alikuwa anatuombea sisi hapa. Tuko pamoja na Councillor Clara Saru Juma, hawa ni baadhi ya akina mama ambao wanatakikana kisheria wawe waakilishaji katika hii committee.

Kamati yetu Commissioners ni kwamba tumefuata muongozo ule ambao unatakikana. Kwamba local authority iwakilishwe, walemavu waakilishwe, vijana waakilishwe, na akina wamama watatu waakilishwe. Halafu pia na Bunge na co-ordinator. Madam co-ordinator Frida Mwadime, hayuko nasi hapa leo. Ameenda Taveta kwa shughuli kama hii. Kwa hivyo ndugu Commissioner Zein kwa hayo mafupi ningerudisha usukani kwako uendelee na mkutano. Thank you.

**Com. Zein:** Asante sana mshitahiki mwenyekiti wa kamati ya kubadirisha Katiba. Kwa heshima kubwa tumekuja mbele yenu ili kufanya kazi hii muhimu kwa taifa letu. Na ningependa kuanza kwa kuwatambulisha wenzangu ambao tumekuja nao, ma-Commissioners kutoka Tume ya kurekebisha Katiba. Nitaanza na bibi aliyekaa mkono wangu wa kushoto halafu niende kwa yule mwenzangu aliyekaa mkono wa kushoto mwisho pale.

**Com. Kabira:** Hamjamboni. Mimi naitwa Wanjiku Kabira, na mimi ni Commissioner.

**Com. Keriako Tobiko:** Hamjambo ndugu. Kwa jina naitwa Keriako Tobiko, na mimi ni Commissioner.

**Com. Zein:** Na mimi naitwa Abubakar Zein, na mimi pia ni Commissioner. Utaona tumekuja na wenzetu pia, ambao ni wafanyi kazi wa Tume. Wako hapa rasmi kufanya kazi hii ya leo. Na nitawaelezea kidogo kuhusu baadhi ya watu wanaofanya kazi hizo. Huyu binti aliyoko hapa, huyu hapa, aliyekaa hapa. Yeye ni mtafsiri wa ishara. She is a sign language interpreter. Ikiwa kuna mwenzetu ambaye ni mlemavu, hasikii, basi yeye itakuwa kazi yake kumtafsiria yale maneno tunayozungumza hapa ili aweze kufuatilizia mkutano huu. Kama unaweza kujitambulisha, unaweza kutumia microphone hii.

**Nancy Odipo:** Kwa majina naitwa Nancy Odipo.

**Com. Zein:** Yule binti aliyekaa pale, kazi yake yeye ni ku-record maneno haya tunayoyazungumza hapa katika tape recorder. Sisi tutakuwa tunaandika maneno haya, lakini kwa vile hatutaki kupoteza hata neno moja mtakalosema nyinyi wananchi watukufu, kazi yake yeye itakuwa ni ku-record mazungumzo haya kwa tape recorder. Halafu tukienda Nairobi, tutayaandika chini katika mswada.

**Alice Thuo:** Kwa majina naitwa Alice Thuo.

**Com. Zein:** Huyu kijana mvulana amekaa hapa, yeye kazi yake ni kuandika kwa mkono mrefu si kwa ku-record mambo yanayoendelea hapa. Yaani ni rapporteur. Karani wa mkutano. Kama unaweza kujitambulisha.

**Onesmus Kipchumba:** Kwa majina naitwa Onesmus Kipchumba. Asanteni.

**Com. Zein:** Huyu binti anayefuata. Yeye ndiye kiongozi wa hawa wafanya kazi wa Tume waliokuja hapa. Na yeye atajitambulisha kwenu.

**Fatuma Jama:** Mimi naitwa Fatuma Jama.

**Com. Zein:** Fatuma Jama asante sana. Yeye ni Program Officer katika Tume ya kurekebisha Katiba. Sasa baada ya kujitambulisha kwenu, ningependa kupitia haraka haraka utaratibu tutaka- ufuata leo ili tuanze kutoa maoni yetu kwa kutumia utaratibu huo. Kwanza kabisa kama ulipokuja uliona kuna watu pale, wamekaa kwenye meza pale nje, kazi yao ni kuandika register. Na register hiyo tumepata majina ambayo tumepata hapa. Utaratibu wetu kama Tume ya kurekebisha Katiba kama tulivyowaalifu mapema, ni kwamba tutatumia haya majina. Aliyeandikisha jina lake kwanza ndiye atakayeitwa na kupewa fursa ya kuanza kuzungumza. Kwa hivyo tutafuata utaratibu huu.

Ukisha pewa fursa ya kuzungumza, utakuja hapa mbele ya microphone hii, ndio uitumie ili tu-record. Utaje jina lako. Useme mimi ni fulani fulani, ndio jina lako liwe recorded, halafu uendelee na kazi yako. Kuna njia tofauti za kutoa maoni. Ikiwa umeandika mswada wako, una haki ya kuleta mswada na kuutoa bila kuzungumza ikiwa unataka hivyo. Ikiwa umeandika mswada wako na unataka kuzungumza, tutakupa dakika tano na tungeomba sana dakika tano hizo usizitumie kusoma mswada. Dakika tano hizo usitumie kuchambua au kutaja mambo muhimu katika mswada wako.

Njia nyingine ya kutoa maoni ni kwamba, ukiwa wewe hukuandika mswada, unataka kutoa maneno yako kwa kauli yako. Kwa mazungumzo peke yake. Tutakupa dakika kumi. Una haki ya kutumia lugha gani? Una haki ya kutumia Kiswahili, Kiingereza na una haki ya kutumia lugha yoyote ingine ya Kenya. Ikiwa unataka kuzungumza Kidawida, una haki hiyo. Na

ukianza kuzungumza hapa, tuta-record mambo hayo na pia tutamwomba mtu atafsiri ndio kila mtu aweze kufuatilizia maoni unayo yatoa.

Halafu pia kuna uwezekano ikiwa mmoja wetu kati yetu hakufahamu vizuri au anataka kufafanuliwa jambo, anaweza kukuuliza swali ili ufafanue katika mambo hayo unayozungumza. Na juu ya hayo, ikiwa kuna mmoja wetu hapa amekereka sana na jambo, anataka kuuliza swali, na jambo hili nitalizungumza tulitie akilini vizuri. Sio kwamba ikiwa kuna mtua amezungumza jambo hulifurahii, utakuwa na haki ya kusimama kwanza kubishana naye. La, hatusemi hivi. Tunasema, ikiwa mtu amesimama hapa, kasema jambo, unataka kufafanuliwa, una haki ya kututumia kikaratasi na swali lako na sisi tunaweza kumuuliza.

Lakini ikiwa haukubaliani na jambo analosema, au pengine unakubaliana naye na unataka kulititilia mkazo au kulichangia zaidi, ngojea upate fursa yako, utakuja utasema, "mimi naunga mkono jambo lile lilosemwa mwanzo au wakati fulani au napinga jambo hili na rai yangu mimi au maoni yangu ni haya". Sijui kama tunakubaliana hivyo? Kila mtu awe na maoni yake.

Baada ya kusema hivyo nitawaomba sana kwa vile sisi sio tu tuko mahali pa ibada, lakini kwa vile sisi ni Wakenya tunaheshimiana tutatumia lugha murua. Sisi kule Mombasa tunasema lugha murua. Siyo? Lugha ambayo mzee akiisikia hatakasirika, mama akiisikia hatakasirika, mtoto akiisikia pia ataona kwamba ni lugha inayotumika, inafaa na ina heshima. Hiyo sio kusema kwamba huna hati ya kusema mambo yanayokusumbua moyoni. Sijui kwamba tunakubaliana hivyo.

Halafu ningewaomba pia ya kwamba, ukishamaliza kufanya hivyo, utahitajika uje hapa. Na sijui nafikiria itakuwa rahisi zaidi, ..Fatuma mkibadirishana kiti au mtu atakuwa akizunguka sana. Ndio akija mtu hapa unakuja ukimaliza kuzungumza, kuna register, lazima ui-sign kwamba umetoa maoni yako. Ukisha sign register hiyo, una haki kusikiliza wenzako au kama una shughuli zingine za kujenga taifa tunajua mambo mengi tunaendelea nayo katika nchi yetu, una haki pia ya kwenda kuendelea na kazi hiyo.

Lingine la muhimu ambalo unafaa kujua na kukumbuka ni kwamba sisi tutakaa hapa kwanzia sasa mpaka saa kumi na mbili jioni. Ikifika saa kumi na mbili jioni na kuwe na Wakenya ambao hawajafikiwa na wana maoni ya kutoa, tutabadirishana rai tuendelee mpaka tutakapomaliza. Au si sawa hiyo?

La mwisho kabisa ambalo ningependa kuwajulisha kabla hatujaanza kazi hii rasmi, ni kwamba tungewaomba kubadirisha utaratibu huu nilioutaja wa kuanza na mtu aliyekuja mbele halafu twende kwa hivo kufuata hivyo, ikiwa kuna sababu la kutosha kufanya hivi. Tunajua sisi Wakenya tuna hali mbalimbali. Kukija mwanamke au bibi ambaye ni mjamzito na hataweza kuvumilia kusubiri kwa muda mrefu, tungewaomba ruhusa tumpe yeye fursa ya mbele. Sijui kwamba munakubali hiyo?

**Audience:** Tunakubali.

**Com. Zein:** Akija mtu mzee sana na yeye pia hawezi kuhimili kukaa kwa muda mrefu, pia tungeomba ruhusa hiyo ya kumpa mzee kama huyo haki ya kumtambua umri wake na mchango anaotoa kuupa fursa ya mbele. Sijui kama mnakubali hayo?

**Audience:** Sawa.

**Com. Zein:** Sawa. Na juzi tulikuwa Tausa. Ilipofika jioni, watu waliokuwa wanakwenda katika location, ndovu wamekuwa wakisumbua watu na kuwatendea watu unyama, wakatuomba wakasema; " Jamani mtupe fursa ya mbele kwa sababu ndovu wanatusumbua sana huku. Tukichelewa hatutafika nyumbani tutalala njiani". Wao pia tukawaruhusu. Lakini yakitokea hayo tutawaomba nyinyi mtupe ruhusa. Sasa sijui kama kuna mtu yeyote ana swali ambaye hakuelewa mambo haya ninayoyaeleza. Nadhani hakuna mtu. Ndiyo mzee wangu.

**Speaker:** Swali langu ni. Je kwa hiyo muda wa dakika tano ukiisha unagonga au nitajua aje muda wangu umekwisha?

**Com. Zein:** Katika sisi watatu tuliokaa hapa, mmoja wetu ataanza tu, kuwa mwenyekiti wa kikao. Na kwa leo tutamwomba Professor. Saa ile alipokuwa akijitambulisha kwenu amesema mimi naitwa fulani wa fulani lakini mimi nitampa hadhi yake, Professor Wanjiku Kabira aanze kuwa mwenyekiti wa kikao hiki baada ya mimi kuzungumza haya. Ikisha kwisha dakika tano zile atakuambia, 'tunaomba ufupishe au please summarize.' Sijui kama tuko pamoja? Sio kwamba tutakwambia eeh, imeisha kaa chini. Tutakuomba u-summarize. Lakini ukishaombwa ufupishe, na wewe pia utuheshimu na uheshimu wengine ufupishe. Sijui kama nimejibu swali lako?

**Speaker:** Sawa.

**Com. Zein:** Sawa. Sasa ningewaomba tuanze rasmi na kumwomba Bi Professor Wanjiku Kabira aanze mkutano wetu kwa kuita mtu wa kwanza katika orodha yetu. Asanteni sana.

**Com. Kabira:** Okey asante sana Zein. Lakini Zein alisahau, kuna mtu mwingine tulikuja naye na hakumtaja. Mnaona mwanamke mwingine ako huko nyuma, bibi mwingine? Huyu ni bibi wa Zein. Mmemuona? Nimefurahi kumuona kwa sababu aliolewa wiki moja tu iliyopita. Today is the first week. So it shows how committed Zein and the wife is to the Constitutional Review. Kwa hivyo tumpigie makofi ameingiaa…..asante sana. Thank you very much. Tutaanza na kama Zein alivyosema tutaenda tu na majina yale tumepatiwa leo. Kwa hivyo tutaanza na Jacob Nyange.

**Jacob Nyange:** Bwana chairman Commissioner wa Tume ya kurekebisha Katiba, Ma-Commissioners na maofisa wote mliokuja nao na viongozi wote wako hapa, kwa majina mimi naitwa Jacob Nyange. Mimi ni mwenyeji wa Rong'e location, Msau sub-location. Basi kwa niaba ya sub-location ya Msau Rahai in Taita district na wale wote wapendao amani na maisha bora, ninafurahi kwa nafasi hii nikabili mbele yenu maoni na mapendekezo yao vile walivyopitisha. Tukishawishiwa na hali

ngumu sana ya maisha hapa Kenya na tukielewa kwamba mdudu mubaya anayesababisha dhiki na maisha magumu ni Katiba mbaya. Tumetaja kwa ufupi tu mambo yafuatayo. Memorandum yetu ina mambo kama haya:

Tunapendekeza Serikali ya Kenya iwe ya *majimbo*. Kwa sababu katika *majimbo* ndipo kutakuwa na maendeleo kamili na rasilimali za nchi hiyo zitatumika sawasawa. Jimbo hilo tunapendekeza liongozwe na governor atakayetoka mahali hapo hapo kwenye jimbo hilo. Na district tunapendekeza zipewe majina tofauti na lijimbo. Na ziwe na autonomy. Kwa mfano inaweza kuitwa "County ya Taita". Na ipewe daraja fulani ya kuendesha mambo yake ya ndani. Mambo ya ndani kama yafuatayo: Revenue, ukulima, maji, madini, ardhi, wanyama pori, samaki na mengineo. County iwe na mamlaka juu ya ardhi yake na matumizi ya ardhi hiyo.

Tunapendekeza kuwa, taratibu za kuhamia kwingine kutoka kwa jimbo lingine ziwe za kistaarabu. Kuwe na taratibu kamili ili kwamba, mtu anapohamia kutoka mahali pengine na kuingia kwingine, isiwe kiholela. Iwe ni kwa sababu amekubaliana na wale wanaoishi pale. Kwa mfano sisi Wataita, kufinywa kwa mipaka yetu kutoka Taru mpaka Nyaseni. Na kutoka Mtito-andei mpaka mto wa Tsavo. Hilo tunaliona kama bomu ambalo siku moja litalipuka. Na tunapendekeza Katiba irekebishe mipaka hiyo iwe kama ilivyokuwa kabla ya uhuru.

La pili, Serikali kuu jimbo la Nairobi. Kuwe na mkuu wa Serikali kando na mkuu wa taifa. Mkuu wa Serikali awe anaitwa Prime Minister na mkuu wa taifa awe anaitwa Rais. Hawa wote wawili pasiwe na mmoja aliye na uwezo zaidi wa kupindukia wala kupita uwezo wa Bunge. Mtanisamehe nifanye kwa ufupi. Wote wawili wachaguliwe kwenye uchaguzi mkuu. Na iwe mwiko kwa viongozi hao wote wawili kuwa wa umri wa chini ya miaka hamsini au kuzidi miaka sabini na tano. Elimu ya chini kabisa iwe ni school certificate O'level. Na wakae ofisini kwa mihula miwili pekee.

Katiba ya Kenya iweke vikwazo kabisa. Serikali ya Kenya isiwezekane kabisa kutawaliwa na jeshi wala polisi. Serikali ya Kenya twapendekeza iwe ya ki-democracia ya kweli kabisa. Ambapo sauti ya mwananchi wa kawaida na haki zake zinasikizwa na kushughulikiwa. Wakuu wa Serikali wakitajwa katika kashfa, wajiuzuru mara moja. Katiba izuie mkuu wa Serikali kuzuia na kunyanyasa wananchi hasa polisi. Wakati wananchi wanaposherehekea vinywaji kama pombe za kienyenji za kiasili zao. Na iwapo basi watapiga marufuku *muratina, mnazi* na *busaa*, basi hata hizo pombe za kizungu nazo pia zipigwe marufuku. Maana mwacha asili ni mtumwa.

Mahakama: Mahakama ziwe huru na za kutekeleza wajibu wao bila uoga na wakuu wa Serikali wasiingilie kazi zao. Bunge. Bunge iwe na uwezo wa kutunga sheria pasipo na kushawishiwa na Serikali, wakuu wa Serikali au matajiri. Kuwe na kamati ya bunge ya kuamua ni lini Bunge litafungwa wala isiwe ni kiholela kama ilivyo sasa. Tume maalum. Kuwe na tume maalum ya kushughulikia masilahi ya wabunge na wakuu wa Serikali hata Prime Minister na Rais na Mkuu wa Sheria. Tume hii ipewe uwezo wa kuwataja. Kuahirisha, kufungua au kuvunja Bunge wanapohitajika kufanya hivyo. Kusimamisha, kukosoa, kuonya au kushitaki Prime Minister au Rais inapositahili.

Mikataba ya kikoloni: Mapatano yote yaliyopitishwa wakati wa kikoloni yavunjiliwe mbali na yafanywe upya, wakishirikisha wenyeji. Hii itawapa nafasi wananchi kuamua iwapo wana ardhi ya kutosha ya kutumia wenyewe na kutenga kwa maendeleo. Katiba ya Kenya itilie mkazo kilimo cha kisasa ambapo wanyama na mimea vitenganishwe.

Viwanda: Ili kuwe na usawa wa kimaendeleo na kupunguza umaskini, Katiba ihimize uzambazaji wa viwanda vijijini. Na wale wazingatie tu kujenga viwanda mijini na vitongoji vyao. Maana hali ilivyo sasa ni ya kubagua vijana wa mashambani maana hawana uwezo wa kukaribia viwanda vya mijini na kutafuta kazi. Vijana wa mashambani wamekwisha kata tamaa na kazi, na hivyo kugeukia uhalifu na kutojali hata kujiendeleza kimaendeleo na kielimu. Hawaoni maana tena ya elimu. Nafasi za kazi ndogo ndogo zinufaishe vijana wa district hiyo badala ya kuleta wageni kutoka nje ya district.

Ufisadi: Bunge iteue Tume maalum ya kupambana na ufisadi ambapo haina mipaka kati ya wakuu na wandogo. Yeyote atakayepatikana akipora uchumi wa Kenya, ajiuzuru mara moja na hapo kuchukuliwa hatua za kisheria bila kujali nafasi yake katika jamii. Watu wote walioibia Kenya mamilioni ya pesa au mali nyingine walazimishwe kuzirudisha ili zisaidie kufufua uchumi wa Kenya.

Elimu: Kuzorota kwa elimu ya Kenya kumesababishwa na mfumo wa 8-4-4 ambao ulioanzishwa bila watu kujitayarisha. Na hivyo sasa kuachia mzazi mzigo mkubwa sana ambao hawezi kubeba wa vitabu na mambo mengine. Elimu iliyoko sasa imekumbwa na ubaguzi mkali ambapo kwa wengine elimu imerundikiwa mambo yote mazuri kutoka nursery hadi University. Ili hali kwa wengine hata ingawaje wangepewa msaada kujengewa training center ya walimu, Serikali inashindwa kumaliza hiyo na basi kuachwa kama white elephant kwa vizingizio ati itamalizwa pesa zikipatikana. Tunapendekeza Katiba ya Kenya, ishurutishe Serikali kumaliza kufungua miradi ambayo itapendekezwa na wananchi na kuianzisha.

Usalama na haki ya mwananchi: Katiba iwe na vipengele zinazotilia mkazo mambo yafuatayo: Usalama kwa watu wote wasio na hatia. Uhuru wa kuabudu kwa kipimo fulani . Uhuru wa watu kukutana au kutokutana. Uhuru wa kujiendeleza - *expression*. Ulinzi wa watu na mali zao kutokana na uhalifu na wanyama pori na askari katili. Uhuru wa media. Haki ya Mkenya kuwa na *passport* bila pingamizi. Na kusafiri nje atakapo. Uhuru wa kuishi kokote nchini Kenya kwa kutimiza masharti ya wenyeji wa mahali hapo. Na kuendesha biashara zake zinazonufaisha wenyeji wa hapo na yeye mwenyewe. Fidia ya mwanadamu anayeumizwa au kuuawa na mnyama pori au polisi katili, isiwe chini ya shilingi milioni moja. Iwapo imedhibitishwa ameuawa kikatili.

Administration: Ili kuwe na adminstration yenye sura ya kupendeka, tunapendekeza mabadiliko ya majina ya kikoloni. Ambayo yamekuwa na sifa mbaya ya unyanyasaji na ukatili. Majina yaliyopendekezwa ni kama haya:

Afisi ya Rais iwe inaitwa ofisi ya Prime Minister. Iliyoko sasa ni ya Provincial Commissioner, aitwe Governor. District

Commissioner aitwe District Administration Officer. District Officer ofisi yake iko relevant yaani haina maana. Chief aitwe Location Administration Officer. Assistant chief aitwe Sub-administration Officer. Headman aitwe Village Overseer.

Watu hao wote wawe ni wa kutoka sehemu hizo hizo wanazoziwakilisha. Headman apandishwe cheo na kuitwa overseer na kulipwa mshahara au marupurupu. Huyu ni vema achaguliwe na wanavijiji na awe wa umri usiopungua miaka hamsini. District Administration Officer akiwa mwakilishi wa Prime Minister ndiye co-ordinator wa district na Serikali kuu kuhusu vile county council inavyoendesha mambo yake na pia hali ya usalama kwa jumla. Hana mamlaka juu ya ardhi bali ni mshauri wa Serikali kuu.

Police force: Katiba izuie polisi kuadhibu au kutesa washukiwa kabla ya kuwa na uhakika wa mashtaka. Mshukiwa akiumizwa na polisi na kutibiwa hospitali, alipwe fidhia kulingana na maumivu. Visa vya polisi kujishughulisha kuchukulia sheria mikononi mwao, zina maana kuwa thamani ya maisha ya Mkenya ni duni sana kuwa Katiba nayo haimlindi kwa vyovyote. Vikosi kama GSU, special branch, administrative polisi viondolewe mbali maana zina tabia ya kudhulumu na ya ukatili isio ya kibinadamu.

Jela: Mateso kwa wafungwa yasipite mipaka ya haki ya binadamu. Yafaa kuwe na kamati fulani ya kuangalia masilahi ya wafungwa. Wakuu wa jela wanaodhulumu wafungwa wao, wakionekana na makosa, washitakiwe na wafungwe jela hiyo hiyo waliotesa wafungwa hao.

Afisi ya county council district autonomy: Mkuu wa afisi ya county council awe wa elimu isio chini ya University na mjuzi wa geographia na historia ya district yake. Umri wake uwe kati ya miaka sitini na sabini na tano. Achaguliwe na wenyeji wa district hiyo moja kwa moja katika uchaguzi mkuu. Yeye atakuwa executive chairman of the county council. Maswala yote ya district; yaani ardhi, mashamba, maji, misitu, wanyama pori, madini, starehe, land business, title deeds, mipaka, elimu ya msingi, ukulima na uzalishaji mali, maendeleo yote katika district yatakuwa jukumu la afisi yake. County council na madiwani wake watakaochaguliwa na wananchi walizao watakuwa na jukumu kamili ya kuongoza county councils zao wakishirikiana na watu wenye profession mbali mbali.

Postscription: Katiba ikaze mkazo yafuatayo: Haya yalikuwa yamesahaulika. Kwanza mfungwa akitoka jela na record nzuri, asifungiwe nafasi zake za kazi bali achukuliwe kama raia wengine wema. Machifu wawe wakipewa uhamisho ndani ya district zao ili kupunguza uwezekano wa mapendeleo na ufisadi. Signed. Jacob Nyange. Mwandishi.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Jacob. Thank you very much. Asante sana kwa hayo maoni yako. Bwana Edward Mwaliko. Okey. Asante. Unakuja? Okey ni sawa tu ataendelea kuandika jina lake. Asante Bwana Mwaliko.

**Edward Mwaliko:** Asante sana mwenyekiti wa Tume ya kurekebisha Katiba pamoja na huyu mwenyekiti wa CCC's. Sasa mimi jina langu ni Edward Mwaliko na nimetoka sehemu hizi hizi za Msau. Maneno ninayoyasoma ni ya watu wa Msau. Yaani

wananchi wa Mwakinyungu. Maneno ninayoyasoma ni mkazo kutokana na yale ambayo yamesomwa juu ya Katiba ya Kenya. Na haya ninayoyasoma nayasoma kwa Kiswahili. Watu wanasema hivi. Wametoa maoni yao namna hii.

Ya kwanza, walisema uwezo mkubwa kupita kiasi ulioekewa Rais uondolewe na Rais anapaswa kuwa na kazi ya kuendesha sherehe, yaani celebrations. Uwezo wote wa kutunga sheria za nchi na uteuzi wa wasimamishi wakuu wa kusimamia idara ya Serikali na mahakama uwekwe kwa Bunge. Uwezo wa kuendesha kazi za nchi, *(executive powers)* kulingana na sheria upewe waziri mkuu anayechaguliwa na wapiga kura wote.

Mahakama and law courts: Mahakimu wawe huru kuendesha kazi zao bila kuingiliwa na Rais au waziri mkuu. Rais asiwe na uwezo wote juu ya mahakama au mahakimu. Wakuu wa mahakama na Attorney General au Solicitor General wachaguliwe na Bunge na waendeshe kazi zao bila uoga. Rais wa Kenya asiwe na mamlaka ya kuwa juu ya sheria na asiweze kutumia wanajeshi au polisi vile atakavyo. Wanajeshi watumike nchini chini ya uongozi wa Waziri Mkuu akishirikiana na bunge. Kugeuza Katiba ya nchi kuwe ni kazi ya watu au tume iliyochaguliwa na watu wote kwa kura ya referendum. Speaker wa Bunge achaguliwe na wabunge.

Nominated members wabunge, waondolewe kabisa kwa kuwa wananyonya mali ya nchi bila kuwa na lolote la faida. Rais asiwe na uwezo wa kuahirisha Bunge, kuvunja Bunge wala uwezo wa kutaja tarehe ya uchaguzi wa Bunge. Hizi ziwe zimepangwa katika Katiba. Isiwe ni lazima Rais au waziri mkuu kuwa Chancellor wa vyuo vyote vikuu nchini. Kwani Chancellor wa University anaweza kuwa mtu yeyote mwenye uwezo na sifa zinazohitajika. Sheria za kikoloni ambazo kwa kweli zimepitwa na wakati ambazo zapaswa kutengenezwa au kuondelewa katika nchi huru ziangaliwe. Ili watu wasiendelee kunyanyaswa na watu wachache. Sheria kama land lease ya miaka tisaini na tisa au miaka mia tisa tisaini na tisa, ziondolewe kabisa na ardhi kama hiyo irudishiwe wenyeji. Kenya iwe nchi ya ki-democracia. Yenye vyama zaidi ya kimoja.

Kenya iwe na Serikali ya *majimbo* ambapo ardhi ni mali ya kabila au imilikiwe na wenyeji wa kabila hilo. Mtu yeyote wa kutoka nje ya eneo hilo, asiingie na kumiliki sehemu yeyote bila ruhusa ya wenyeji. Bila kibali ama mapatano ya wenyeji na Serikali Kuu isiingilie jambo lolote kuihusu ardhi. Kila jimbo liwe na haki ya kukataa amri zozote za Serikali Kuu ikiwa amri hizo hazifai kwa jimbo hilo. Kenya isifanye mkataba na nchi yeyote ambako Kenya inaweza kutishwa na nchi hiyo au agizo kwa kuwekewa vikwazo au kushambuliwa wakati inapokataa kutimiza masharti ya mikataba hiyo.

Mambo ya Wilaya na Serikali ya hapo hapo, yaani Local Government, yaendeshwe na watu waliochaguliwa wa mahali hapo. Na yasitawaliwe na Serikali kuu. Serikali hiyo ya watu wa hapo hapo iwe na uwezo wote kuhusu ardhi na mambo yote kama mali, ya ardhi, madini, maji, misitu na wanyama pori. Mambo yawe ni *majimbo*. Matumizi ya ardhi yatawaliwe na makubaliano ya wenyeji, kwa mfano ardhi kama trust land zitawaliwe na kufaidisha wenyeji wa county councils hizo hizo. State land, national parks na game reserves zitawaliwe na county councils lakini theluthi moja ya pesa zinazopatikana hapo, ipewe Serikali Kuu.

Shirika la Kenya Wildlife Services (KWS) liondolewe kabisa pamoja na sheria zake. Mambo yote kuhusu elimu ya msingi na upili afya, ukulima, maji, towns, barabara, na kesi za mashamba iwe ni kazi ya local Government katika *majimbo*. Elimu ya vyuo vikuu na njia za reli, viwanja za ndege na bandari ziwe kazi ya Serikali Kuu. Lugha ya kutumiwa katika Bunge iwe ni lugha rasmi ya Kiswahili inayoelewa na Afrika yote. Hotuba zote za Rais hasa katika radio na television zitolewe kwa Kiswahili. Bunge lifanye kazi kwa muda wa miaka minne. Halafu livunjwe na uchaguzi mpya ufanywe

Uhuru wa kusema, uhuru wa kutoa maoni ya kibinafsi. Uhuru wa kuzungumza katika baraza, na uhuru wa kuwa mjumbe wa kikundi chochote mtu apendacho udumishwe kwa heshima. Chiefs Act iondolewe kabisa. Uhuru wa kutembea kokote nchini na pia uhuru wa kutembelea nchi yeyote mtu atakayo uwepo bila kukataza kisheria. Haki za kila mwananchi na kila mtoto awe na haki ya kupata elimu ya bure mpaka kiwango atakachoweza kulingana na akili zake. Mishahara ya watumishi wa Serikali hata walimu wa shule na University, polisi na wauguzi wa hospitali iwe ni kazi ya baraza maalum kuamua. Baraza hilo liteuliwe na Bunge. Mishahara na marupurupu ya wabunge iamuriwe na baraza maalum. Na wala si Bunge. Baraza hilo liteuliwe na wananchi kwa kura ya referendum. Polisi wasipewe uwezo au haki ya kupiga washukiwa ili kuwalazimisha kukubali kuwa na hatia.

Uraia wa Kenya uthibitishwe kwa kuzaliwa hapa hapa Kenya na wazazi wote wakiwa Wakenya au babu akiwa Mkenya, au baba akiwa Mkenya kwa kuapa kisheria kuwa Wakenya kwa naturalization. Sheria za kimila na kikabila kuhusu urithi na kulipa fidia kwa kutia msichana mimba zifuatwe. Kwa mfano, kwa Wataita, mtu akimtia msichana mimba na akubali kumuoa atatoa mali kulingana na mali za wenyeji wa huyu msichana.

Mtu huyo akikataa kumuoa huyo msichana atalipa fidia. Kwa Wataita ni ng'ombe jike moja na fahali mmoja na kondoo jike moja. Mtoto atakayezaliwa atachukuliwa na babu mzazi wa mama yake. Mtu akimnajisi msichana au mwanamke kwa kutumia nguvu, afungwe jela kwa miaka isiopungua saba. Na ikiwa amemnajisi mtoto wa umri wa chini ya mwaka mmoja, ahukumiwe kunyongwa.

Haki za watu: Haki ya mtu kukataa kuingiliwa nyumbani ama shambani ili kufanyiwa ukaguzi bila hati maalum ya kisheria iwepo kamili. Yaani hiyo haki iwekwe. Haki ya mtu kukataa kunyang'anywa ardhi yake bila malipo maalum, hata kama ardhi yatakikana kwa matumizi ya raia wote iwekwe na kutimizwa.

Pensions zirekebishwe na kila wakati zilingane na grades na scaling ya mishahara inavyoendelea kuongezeka. Kwa sababu mambo inazidi kupanda. Kazi zilizofanywa na wale watu wa hapo awali, zilikuwa za maana sana. Mtu anayeishi kwa pension akifariki, mjane wake aendelee kupata pesa za bwana huyo mpaka mwisho wa maisha yake. Na ikiwa mtu huyo alimuacha mtoto wake ama mjukuu wake yatima aliyekuwa akimulea, basi mtoto huyo ama watoto hao walipwe pesa hizo za baba au babu yao mpaka atimize umri wa miaka ishirini na miwili.

Wananchi waamue mipaka yao ya location, division na ward zao badala ya Serikali. Kuwe na usawa na haki kisheria kuhusu umilikaji wa ardhi ili kulinda kunyakuliwa kwa ardhi.

**Com. Kabira:** Uko karibu kumaliza?

**Edward Mwaliko:** Imebakia kidogo.

**Com. Kabira:** Okey. Asante.

**Edward Mwaliko:** Presidential clemency. The right of the President to show clemency kwa person condemned to death like courts of law, Rais awe na haki ya kusamehea na kubadirisha adhabu ya hukumu ya kifo na kuigeuza kuwa kifungo cha maisha baada na Rais kushauriwa na makundi ya dini. Neno mtukufu ni la sifa kwa Mungu, basi neno hilo litumike vizuri. Jukumu la kutuma majeshi kuhudumu katika nchi za nje katika shughuli za kivita ziwe ni wajibu wa Bunge. Wawakilishi na wananchi bungeni na katika baraza za miji wawe wenye elimu ya juu kama University. Kazi ya polisi ni kazi muhimu kwa hivyo polisi wote nchini wawe watu wenye elimu isiopungua kidato cha sita.

Kila mtu anayeajiriwa katika utumishi wa umma hadi awe na ujuzi na sifa zinazolingana na masharti na uwezo wa kuendesha kazi hiyo. Vyeo na majina kama district commissioner, chief na kadhalika yabadirishwe. Yaani yasiwe ya kikoloni. Mali au utajiri wa nchi usambazwe kwa usawa kote nchini ili kuondoa umaskini na ujinga. Na kila mtu atendewe haki. Mali zilizoko ndani ya ardhi kama vile madini katika maeneo ambako wenyeji hawana ujuzi au vifaa vya kuzitoa, viachwe hapo hapo mpaka wenyeji watakapopata ujuzi wa kuzichimbua.

Members wa Tume ya Uchaguzi wawajibike kwa umma na sio kwa Rais kama ilivyo sasa. Ingawa utalii ni sekta yenye kutupatia pesa nyingi, usiruhusiwe kutufanya watumwa hata tukasahau mila zetu, kupotewa na lugha zetu na hata kuharibu familia zetu. Kesi nyingi za mashamba, haziendeshwi kwa haki na huenda zikaleta matatizo hapo baadaye. Tusiige mtindo wa maisha ya kigeni kama huko Uingereza na India. Tusikubali mtindo wa vilasi.

Wafalme, balozi, matajiri na watu wa kawaida au hata ule wa caste system wa India. Sheria zilizotungwa na mtu mmoja hata kama ni Rais ziondolewe. Kwa mfano sheria ya kukataza pombe za kienyeji ati kuwa zinaharibu watu haikuwekwa na Bunge, kwa hivyo itupiliwe mbali. La sivyo ikiwa tunalenga kuondoa ulevi kabisa, basi sheria hiyo ipanuliwe ili ikataze pombe zote hata za kigeni kama beer brand whisky na vodka.

Wananchi wapewe uwezo na Katiba wa kumpokonya mamlaka diwani, mbunge na hata Rais endapo atakuwa hahudumii watu kulingana na matarajio yao. Hiyo sio ya mwisho. Ya mwisho ni kuhusu magari ya Serikali inayotumiwa na maofisa. Yatumiwe kwa uangalifu ili pesa ya wananchi iwafae watu. Ikiwa ofisa fulani anatumia vibaya, basi afanywe kugharamia gari hilo.

**Com. Kabira:** Asante sana Mzee Edward. Thank you very much. Na nitakuuliza swali moja Mzee Edward. Niko na swali kwako. Ninauliza ulisema yule mtu akishika mtoto wa chini ya mwaka mmoja, huyo anyongwe. Lakini mtoto akiwa wa mwaka mmoja au miaka miwili au miaka mitatu. What is the difference?

**Edward Mwaliko:** Ahukumiwe pia kunyongwa.

**Com. Kabira:** Hata mtoto akiwa ni wa mwaka mmoja au miaka miwili?

**Edward Mwaliko:** Hapo watu walipendekeza hivyo ili yeyote atakaye mguza mtoto wa chini ya mwaka mmoja tumeelekeza korti imhukumu kunyongwa. Lakini sasa hapo yale mengine yatategemea vile sheria inavyofanywa.

**Com. Kabira:** Nimeliona ni lizuri. Asante. Na swali lingine tena. Serikali ya *majimbo*, umesema tuwe na Governor. Kuna Parliament au Serikali, hiyo itakuwa wapi?

**Edward Mwaliko:** Wajua haya mambo tuliyoongeza hapa yanatilia mkazo yale mengine ambayo yamesomwa hapo mbele.

**Com. Kabira:** Okey. Asante sana.

**Edward Mwaliko:** Haya niliyoongeza ni yale ambayo inagusa wenyeji kamili, yamewagusa hasa.

**Com. Kabira:** Okey na swali lingine pia. Unasema mtu akichukua msichana, awe na mimba na asimuoe, tutukmie ile mila ya Kitaita. Si ndiyo?  Analipa ng'ombe moja.

**Edward Mwaliko:** Hiyo tulitoa mfano wa vile kwa Wataita ilivyo. Sisi tangu hapo zamani, ukimtia msichana mimba, utafanya mapatano na wazazi wa huyu msichana. Sasa ukisema huyu msichana nitamuoa basi hapo utapata laini ile ya kawaida. Yaani utalipa halafu mutafanya mapatano na umchukue. Ukisema huyu msichana si muoi, kwa Wataita utatoa ng'ombe jike moja, dume moja na kondoo jike moja. Lakini mtoto hutamchukua. Mtoto atakuwa ni u mji ule ule.

**Com. Kabira:** Na akiwa na miaka kumi na miwili?

**Edward Mwaliko:** Huyo mtoto?

**Com. Kabira:** Yes.

**Edward Mwaliko:** Hapo itakuwa ni mapatano mengine.

**Com. Kabira:** Okey. Asante sana bwana Edward. Florence Mbalu.

**Florence Mbalu:** Nashukuru kwa fursa hii kwa kuwa mbele yenu, Bi mwenyekiti na Tume yako kutoka Nairobi. Bwana mwenyekiti wa kamati andalizi ya Mwatate, macouncillors, wananchi watukufu, mabibi na mabwana, niliye mbele yenu ni Bi Florence Mbalu kutoka kata ya Kishaba, sub-location ya Mengo. Nikiwakilisha yafuatayo:

Ripoti kuhusu marekebisho ya Katiba tarehe ishirini na mbili mwezi wa nne mwaka wa elfu mbili na mbili. Maelezo ya kwa wahusika. Bwana Kilimo alieleza kuhusu maana ya Katiba. Alitoa mfano wa Katiba ya Wataita vile ilivyokuwa hadi zamani. Alisema kuwa Katiba imerekebishwa mara thelathini na nane. Alishukuru sana kuona kwamba leo hii sisi tumepatiwa nafasi ili tuweze kuchangia katika marekebisho ya Katiba. Bwana L. Mwambela Mwawasi, aliwaeleza waliohudhuria vile tunavyoweza kuchangia kikamilifu. Ingawaje, tuna muda mfupi sana. Alituhimiza kwamba…

**Com. Zein:** Bi Florence. Hiyo ni ripoti mliokuwa nayo. Unaweza kutupa tukaipokea. Lakini maoni yako kuhusu kubadirisha ni nini?

**Florence Mbalu:** Ni yale ambayo yanatuathiri leo.

**Com. Zein:** Sawa. Kwa hivyo utatoa hiyo ripoti baadaye lakini hayo yanayokuadhili ndio muhimu tunataka kusikia.

**Com. Wanjiku Kabira:** Asante sana Bi. Florence, peana hiyo karatasi halafu utwambie maoni yako. Okey lakini tafadhali tumia microphone. Uje karibu na microphone.

**Florence Mbalu:** Katika kitabu cha marekebisho ukurasa wa kumi na nane 'haki ya ardhi na mali'. Anayepaswa kuwa na umiliki wa mwisho wa ardhi ni jamii ya mahali pale. Ndio, Serikali iwe na uwezo, lakini kuwe na makubaliano fulani baina ya Serikali na mwenye ardhi. Kusiwe na lazima. Serikali ya mitaa iwe na uwezo wa kuthibiti wamilikaji na wakaazi wanavyo tumia ardhi.

Jamii ishughulikie mambo ya ugawaji wa mashamba. Mtoto akifika umri wa miaka kumi na nane, apatiwe shamba lake na wazee ili aweze kujiendeleza kimaisha. Ndio kuwe na kiwango cha juu cha ukulima wa ardhi inayoweza kumilikiwa na mtu binafsi. Umilikaji wa ardhi urahisishwe. Kusiwe na malipo mengi katika kukubaliana title deeds kutoka kwa mzee hadi mtoto. Maafikiano na mapatano yaliyokuwepo kabla ya uhuru miongoni mwa wanajamii yasiwepo sasa. Kwa sababu kuna ongezeko la watu.

Wanawake wawe na uwezo wa kumiliki ardhi sawa na wanaume. Lakini kuwe na utaratibu na makubaliano baina ya jamii. Katika ukurasa wa kumi na sita 'haki za kimsingi'. Masharti ya Kikatiba haki za msingi hayatoshi. Serikali iweze kuwasomesha watoto kwanzia shule ya vidudu yaani nursery school mpaka kidato cha nne bila malipo. Hukumu ya kifo iondolewe na badala yake ikuwe ni kifungo cha maisha. Mwananchi afundishwe na apewe uwezo wa kutumia rasilimali yake. Apatiwe vifaa vinavyomwezesha kutumia kwa shughuli hizi. Katiba ilinde usalama, huduma ya afya, maji, elimu, maakazi, chakula na ajira. Usalama upewe muda zaidi chuoni ili wanaohusika wapate elimu zaidi ya kujua sheria.

Huduma ya afya iwe ya bure kwa sababu wale ambao hawana uwezo wa kifedha wanapata shida sana. Katika ukurasa wa kumi na saba 'haki ya makundi yanayoweza kuadhiriwa'. Masilahi ya wanawake hayajahakikishwa kikamilifu na Katiba. Iwapo msichana amepata mimba, hatua za kisheria zichukuliwe. Pia msichana akinyanyaswa kimapenzi mhusika achukuliwe hatua za kisheria. Walemavu wapewe elimu ya bure kwanzia shule ya vidudu hadi chuo kikuu.

Wapewe vifaa vya kutumia ili kuweza kukabiliana na hali yao. Wapewe mikopo ya kuwawezesha kujiendeleza baada ya kumaliza masomo. Wapewe vifaa maalum. Vifaa vya kuwawezesha kuwasiliana. Wapewe nafasi nzuri za kazi kulingana na ujuzi wa elimu yao. Katiba inaweza kulinda haki za watoto kwa kuwapatia yafuatayo: Elimu ya bure, ofisi za kuwashughulikia watoto ziletwe katika kiwango cha kata. Shule za watoto walemavu ziletwe katika kiwango cha kata.

Makundi mengine ambayo hayashughulikiwi na Katiba ni wazee, wajane, maskini na mayatima. Katiba itoe masharti kwa vitendo visawazishi kwa manufaa ya wanawake na makundi mengine. Kuwe na masharti kwa vitendo. Kuwe na kamati tekelezi katika viwango vya vijiji. Katika ukurasa wa kumi na tisa 'haki za wanajamii'na tofauti za kitamaduni kukabiliana na kialeo. Katiba itambue na iendeleze lugha za kienyeji.

Tuwe na lugha moja ya kitaifa yaani Kiswahili ili kuhakikisha umoja na usalama wa mtu binafsi na mali. Ni lazima mtu aheshimu mila na tamaduni za wale wanaoishi pale yaani wenyeji. Mila na desturi lazima zihifadhiwe lakini kwa uangalifu. Katika ukurasa wa ishirini ' uongozi na matumizi ya mali asili'. Mamlaka ya nchi yaziendelee kudhibiti uwezo huu. Mamlaka yadhibitiwe na Serikali za mitaa, yaani local authority. Bunge isiwe na uwezo wa mamlaka wa kuamurisha ukuzaji na matumizi ya fedha za umma. Serikali zipewe uwezo huo.

Msimamizi na mkaguzi wa fedha za umma yafaa apewe ulinzi zaidi. Pia awe akichaguliwa katika bunge. Mkaguzi mkuu ateuliwe na bunge. Tunaweza kuwavutia Wakenya walio talaamika ili waweze kufanya kazi katika mashirika ya umma kwa kuwapatia mishahara mizuri. Anayepaswa kuteua tume ya huduma za umma ni Bunge. Inatupasa kuwa na kanuni za maadili ya maafisa wote wanaohudumia umma. Maafisa wa umma walazimishwe kutangaza mali yao. Katika ukurasa wa ishirini na moja 'mazingira ya mali ya asili'. Masawa ya uhifadhi wa mazingara yanayopaswa kuingizwa kwenye Katiba ni: Viazo vya maji (*water catchment*) misitu ichungwe Kikatiba. Kamati ziundwe za kuhusika na mazingira.

Matumizi ya rasilimali zipitie katika Serikali ya mitaa. Mali zote zinapaswa kulindwa na Katiba. Mwenye jukumu la kulinda na kusimamia mali ya asili ni mwenyenchi kupitia kwa Serikali za mitaa. Mali ya asili izimamiwe na kamati ndogo ndogo kutoka mashinani. Ukurasa wa kumi na tatu,'Serikali za mitaa'. Mayor na wenye viti wa mabaraza wachaguliwe moja kwa moja na wananchi. Mayor na wenye viti wawe na vipindi vya miaka mitano. Mabaraza yasiendelee kufanya kazi chini ya Serikali Kuu. Kiwango cha elimu cha chini cha madiwani kiwe kidato cha nne.Mitihani inayofanywa kwa lugha haitoshi. Kuwe na masharti ya kimaadili na kitabia kwa wagombea viti vya udiwani.

Wananchi wawe na haki ya kumrejesha diwani nyumbani kwa kura ya kukosa imani. Atakaye kata kauli kuhusu mishahara na marupurupu ni Tume ambayo itachaguliwa na wananchi. Ndio tuwe na madiwani walioteuliwa lakini kuwe na njia maalum ya kuwateua. Madiwani waongezwe na masharti yafuatao katika mfumo wenye vyama vingi. Uazi, uajilikaji na uaminifu. Rais na waziri wa Serikali za mitaa asiwe na uwezo wa kuvunja mabaraza. Katika ukurasa wa kumi na nne, 'muundo wa utaratibu wa uchaguzi'. Tufuate mfumo wa kura za siri. Tuendelee kufuata mfumo ambao mwenye kura nyingi ndiye mshindi.

Wanawake watengewe viti maalum hadi kiwango cha wilaya. Kuwe na idadi ya chini ya asilimia hamsini kwa mia. Ikiwa mgombea kiti hajatosheleza kiwango hiki katika duru ya pili asitangazwe kuwa mshindi. Wagombea viti wanaokosa kuteuliwa na chama kimoja wako huru kuomba uteuzi kutoka vyama vingine.

Kuwe na uhuru wa kuhama toka chama kingine hadi kingine. Tuendelee kuwa na kanuni ya asilimia ishirini na tano kwa mia ya uakilishi katika angaa mikoa mitano katika uchaguzi wa Urais. Tuwe na viti maalum vilivyotengwa kwa makundi ya akina mama, walemavu na vijana. Vyuo tuwe na maeneo ya kigeographia katika uakilishi. Hatutosheki na ugawaji wa maeneo ya uakilishi wa Bunge na mabaraza.

**Com. Kabira:** Mama Florence, utajaribu kumaliza. Uko karibu?

**Florence Mbalu:** Ndio niko karibu sasa.

**Com. Kabira:** Okey.

**Florence Mbalu:** Hatutosheki na ugawaji wa maeneo ya uakilishi wa Bunge na mabaraza. Tuendelee kufanya uchaguzi wa Bunge na mabaraza wakati mmoja. Utaratibu wa uchaguzi urahisishwe kwa kuhesabu kura hapo hapo baada ya kumaliza kupiga kura. Tarehe ya uchaguzi itajwe kwenye Katiba.

Uchaguzi wa Urais uwe na kura ya maoni. Pia ufanywe moja kwa moja. Ma-Commissioners wawe na sifa nzuri. Uajibikaji na uwazi. Commissioners wateuliwe na Bunge.

**Com. Kabira:** Bi Florence, so you can give us the highlights. Utatupatia highlights kwa sababu saa imekwisha sana.

**Florence Mbalu:** Sasa nitafika ukurasa wa saba halafu nimalize.

**Com. Kabira:** Asante.

**Florence Mbalu:** Ukurasa wa saba 'vyama za kisiasa'. Vyama vya kisiasa vizitekeleze majukumu mengine. Katiba itekeleze uundaji, uongozi na tabia ya vyama vya kisiasa. Kuwe na idadi maalum ya vyama vitakavyosajiliwa. Tuwe na jumla ya vyama vitatu. Kila chama kiweze kujigharamia chenyewe. Shughuli za vyama vya kisiasa zigharamiwe na fedha za umma. Kuwe na uhusiano mzuri baina ya dollar na vyama vya kisiasa.

Ukurasa wa nane, 'muundo wa aina ya Serikali'. Tusiendelee kuwa na miundo ya Serikali wa Urais. Tufuate muundo wa Serikali ya ubunge ambapo tuna Waziri Mkuu na chama chenye uwezo zaidi bungeni. Waziri Mkuu ndiye atakaye unda Serikali. Rais awe na uwezo wa kuweka sahihi mijadala itakayoitishwa au kuidhinishwa bungeni. Tusifuate muundo wa useto ambao mamlaka ya nchi yamegawanywa baina ya Rais na Waziri Mkuu. Tuendelee kufuata muundo wa Serikali moja kwa ajili ya usawa katika ugawaji wa rasilimali za wenyeji. Njia ambazo zinaweza kufuatwa ili uwezo ufikie viwango vya chini vya Serikali ni kutumia Serikali za mitaa. Maoni zaidi kutoka kwa watu mbali. Malipo ya wastaafu yafanyiwe katika tarafa. Kiti cha Urais kiwe na vipindi viwili vya miaka mitano peke yake.

Mbuga za kuhifadhi wanyama zirudishwe Serikali za mitaa. Pia jina 'national park' liondolewe. Kubuniwe Tume ya kujadili mishahara ya Bunge. Ikiwa mtu aliyestaafu amefariki, yafaa mipango ifanywe ili mjane apatiwe malipo hayo bila kuchelewa. Maafisa wa utawala wawe wakichaguliwa na wananchi. Masanduku ya kupigia kura yafaa yawe na uwazi yaani (*transparent ballot boxes)* ili kuwezesha kuona vile idadi ya kura inaongezeka.

Waganga wa kienyeji waruhusiwe kufanya utafiti katika madawa. Mbunge akichaguliwa kwenda Bunge, abaki vile vile kama mbunge asiteuliwa kuwa waziri kwa sababu hatawatetea waliompigia kura bali atakuwa upande wa Serikali.

**Com. Kabira:** Bi Florence, unajua kwa sababu utatupatia memorandum, taja tu kwa ufupi ile imebaki. Umemaliza?

**Florence Mbalu:** Ninamaliza, imebaki laini tatu. Kuwe na uhuru wa kuabudu lakini uwe na mipaka. Kuwe na klabu cha pombe ya minazi. Wanaogombania viti vya udiwani au ubunge lazima wawe wazalendo wa eneo hilo. Wasiwe watu wa kutoka nje. Hiyo ndio maoni yangu.

**Com. Kabira:** Asante sana Bi. Florence. Thank you very much. Natutamuuliza Peter Mndeke. Yuko. Asante Peter.

**Peter Mndeke:** Commissioners wetu na wazee ambao wako hapa, mabibi na mabwana, kwa majina mimi naitwa Peter Mndeke. Ijapokuwa memorandum yangu ni fupi kidogo kwa sababu mwenzangu Bi. Mbalu amekwisha wakilisha. Zangu tu ni tatu peke yake. Na mtaniwia radhi nitasema kwa Kizungu.

The first memorandum is; the Controller and Auditor General should be given powers to prosecute corrupt public servants and those who are found guilty should not be allowed to hold any public office. The second memorandum is: the Members of Parliament and any other appointed Commissioners' salaries should be vested on a National Salary Commission. A body that will look on their remuneration package to ensure that the taxpayers money is spent wisely. Thus, neither the MP's nor the Commissioners will be overpaid or underpaid.

Third, the President should not have powers to nominate chairmen of parastatal organizations or permanent secretaries but these positions should be advertised in the press. Thank you ladies and gentlemen.

**Com. Kabira:** Thank you very much Peter Mndeke. Peter Mwakodi.

**Peter Mwakodi:** Mimi kwa majina naitwa Peter Mwakodi. Mwenyekiti wa Katiba ya marekebisho na officers wengine, yangu ni mapendekezo machache tu ambayo ninayo. Napendekeza kuwe hivi: Elimu ya msingi iwe ya bure mpaka kidato cha nane. Wazee ambao hawajiwezi nao waangaliwe na Serikali kwa maisha yao ambayo imebakia. Kama hivi sasa hapa Taita district, mbuga za wanyama ndizo kubwa kuliko mahali watu wanapoishi. Ningalitaka iwe ndani ya Katiba kwamba sehemu kubwa ya pesa ambazo zinatoka huko zibaki kwa district. Yangu ni hayo. Asanteni.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Peter. Peter kuna swali Commissioner anataka kuuliza.

**Com. Zein:** Umesema Serikali iwaangalie wazee,

**Peter Mwakodi:** Naam.

**Com. Zein:** Kwanzia umri gani?

**Peter Mwakodi:** Kwanzia umri wa miaka sabini.

**Com. Kabira:** Asante. Now, tutamwita Nelson Heri. Asante.

**Nelson Heri:** Mwenyekiti wa kurekebisha Katiba na Ma-Commissioners, mimi yangu yalitangulizwa na msemaji number one. Mimi jina langu ni Nelson Heri Shikwapo. Kwa hivyo yule alisoma number one na number two tulikuwa pamoja. Isipokuwa

kuna kitu ambacho tulikuwa tumesahau kidogo ambacho mimi nitasema. Ni kuhusu wabunge na madiwani. Mbunge yeyote au diwani yeyote akiwa amepatikana na uhalifu wa aina yeyote ile, iwe ni mwisho wake wa kugombea kiti cha ubunge au cha udiwani hata kama ana qualifications za masomo ya aina gani. Hiyo ndiyo tulikuwa tumesahau. Otherwise, that is all.

**Com. Kabira:** Okey. Thank you very much Bwana Nelson. Now tutamuuliza Jonas M. Chola.

**Jonas Mwachola:** Mwenyekiti wa kurekebisha Katiba na Ma-Commissioners na maofisa walioko, na wananchi kwa jumla, nashukuru kwa nafasi hii. Mimi jina langu naitwa Jonas Chavia Chola na niwakilisha viongozi fulani katika sehemu yetu ya Rong' e juu location, taarafa ya Mwambiro hapa katika district hii ya Taita Taveta.

Maoni yao juu ya marekebisho ya Katiba ni kama yafuatayo: Kuhusu ardhi, wanasema wananchi wa Taita Taveta, waongezewe asilimia kumi ya ardhi kutoka kwa mbuga za wanyama porini kwa matumizi yao. Pili, jina la *national park* ligeuzwe liwe *game reserve*.

Tatu, asilimia hamsini ya mapato ya mbuga za wanyama ilipwe baraza la wilaya ya Taita Taveta. Watu wasiruhusiwe kumiliki ardhi zaidi ya acre hamsini katika area zile ambazo unatoka. Mahali kuna maji ya kutosha yatumiwe kunyunyizia mashamba. Mashamba yalazwe mara moja na watu wapewe hati za kumiliki mashamba. Mashamba makubwa yanayomilikiwa na wageni yarudishwe kwa wananchi.

Rasilimali. Hiyo ni topic ya pili. Misitu iwe inafaidi wananchi wa eneo hilo moja kwa moja. Asilimia hamsini ya mapato ya maji ya *Mzima Spring* yalipwe baraza la wilaya ya Taita Taveta. Asilimia hamsini ya mapato ya bandari ya Mombasa yatumiwe kwa maendeleo ya Mkoa wa Pwani. Madini ya wilaya ya Taita Taveta yasichimbwe na watu kutoka nje ya wilaya hii. Umeme usambazwe kote nchini. Uakilishi. Idadi ya wanawake bungeni na mabaraza za wilaya iongezwe. Katiba imalize kabla ya uchaguzi ujao.

Serikali ijayo iwe ya *majimbo*. Sheria iliyoko kwa sasa inayomruhusu mwananchi kuishi popote pale ifanyiwe marekebisho iwe mtu kutoka nje hawezi kugombea viti vya uongozi kama ubunge au udiwani.

Utawala: Mwenyekiti wa baraza la wilaya achaguliwe na wananchi. Katiba ijayo DC asiruhusiwe kuwa mwenyekiti wa kamati ya maendeleo ya wilaya. Bali awe mtu kutoka wilaya hiyo. Chifu na manaibu wake wachaguliwe na wananchi moja kwa moja. Ofisi ya Mkuu wa Sheria na Mahakama ziwe na uwezo wa kujisimamia zenyewe. Rais ajaye awe chini ya sheria na tena asiwe mbunge. Cheo cha Waziri Mkuu kibuniwe.

Masilahi ya watu: NSSF ibadirishwe kuwa kama shares kutoka ilipoanzishwa ili ifaidi wanachama wake. Katiba ijayo iangalie wazee wote wenye umri wa miaka sitini na tano na kuendelea kwa njia ya kifedha. Kukiwa na nyongeza ya mishahara, wazee

waliostaafu na wao wafikiriwe. Masilahi ya watu: Wajane walipwe malipo ya uzeeni ya mabwana au bibi zao mpaka kifo. Hapo ni kwamba wakifariki, bwana akifariki au kama ni bibi alikuwa akipata pension akifariki basi yule aliyebaki aendelee kupewa mpaka akufe.

Vijana wasio na kazi walipwe ujira fulani kutoka kwa Serikali kuu ili kujimudu kimaisha. Elimu: Katiba ijayo ifanye elimu iwe ya bure kutoka ya msingi hata ya sekondari. Kila mkoa uwe na chuo kikuu. Afya: Katiba ijayo ifanye matibabu yawe ya bure. Uraia. Mwanamke akiolewa kutoka nchi nyingine apewe uraia mara moja.

Mawasiliano: Tuwe na usawa wa barabara kote nchini. Utamaduni: Utamaduni wa Wataita uhifadhiwe na kuheshimiwa. Dini. Dini zichunguzwe na zile potovu zipigwe marufuku. Na list ya walioandika iko hapa. Nitakoma hapo.

**Com.Prof.Wanjiku Kabira:** Asante Bwana Chola. Nikuulize swali tafadhali. Ulisema mwanamke akiolewa, bwana yake awe Mkenya apatiwe uraia?

**Jonas Chola:** Yaani kama mwanamke ameolewa na si raia wa Kenya basi apatiwe uraia mara moja. Asije akabaguliwa kwamba pengine kama ni Mzungu, aonekane kama yeye ni Mkenya maana ameolewa na Mkenya.

**Com.Prof.Wanjiku Kabira:** Lakini mwanamke yule anayeolewa na mwanamume akiwa ni Mzungu au ni Mganda au ni kabila lingine. Huyo mwanaume awe mraia?

**Jonas Chola:** Mwanamume apewe uraia kama ameleta mwanamume.
**Com. Kabira:** Kama mimi nikiolewa na Mzungu nimlete apatiwe uraia?

**Jonas Chola:** Kama mnaishi hapa yaani kama amekata shauri kuishi hapa, apewe uraia pia maana ni mwananchi wa huku.

**Com. Kabira:** Okey. Asante sana Bwana Chola. Julius Katambo.

**Julius Katambo:** Commissioners mimi niko na huyu ndugu Jonas Chavia na tulikuwa tunawakilisha hiyo kata ya Rong'e juu, tarafa ya Mwambiro division. Sasa niko na vipengele viwili nitaongezea hapo. Jina langu ni Julius Katambo. Kuna kipengele kingine ambacho nitaongezea katika ile ambayo imesomwa. Mali ya nchi itumike kwa watu wote sio ipelekwe mahali Rais anatoka peke yake.

Kipengele cha pili, wafanyi kazi wa Serikali au wa kampuni, wachukuliwe kutoka kila pembe ya Kenya. Ni hayo.

**Com. Kabira:** Okey asante sana. Utaandika jina lako. Richard Mwangeka. Mr. Mwangeka kwa sababu ulizungumza Tausa,

si utatumia dakika kidogo? Okey. Asante.

**Richard Mwangeka:** Asante sana Commissioners, wazee wa hapa, mabibi na mabwana hamjambo. Basi kwa niaba ya *Shirikisho Party of Kenya* mimi nilikuja hapa kwanza kusema kwamba Katiba yetu hii mpya ambayo tunaandika, iwe ya *majimbo*. Na *majimbo* haya yawe vipi? Kufuatana na kitabu cha Mwenyezi Mungu kwa sababu Kumbukumbu la Torati mlango wa thelathini na mbili, kifungu cha saba hadi cha tisa kinasema hivi: '*Mungu aliumba ulimwengu na akaapa kila taifa na nchi yao wawe na mahala pao.'* Taita Taveta kuwe ni Wataita. Kwale kuwe na watu wa Kwale. Kilifi, Kisumu, Nyeri namna hiyo.

Katiba hii ambayo tunataka kuandika mpya, sisi tumesema kwamba utawala wa mikoa uondoke. Umetunyanyasa mno. Kupitia kwa Ma-DC mumeona vile mashamba yameenda na plots zimeenda. Kwa hivyo *if we want to heal this country* tuponyeshe dunia hii na kuwaondoa hao mabwana.

Jambo lingine. Kipengele kingine kiandikwe kwamba mwananchi yeyote wa Kenya asitoe pesa nje ya nchi hii. Mumeona vile umaskini umezidi. Pesa ziko kule ng'ambo lakini twataka IMF na World Bank watusaidie. Na pesa ziko nje. Ndugu zangu si makosa haya? Hayo ni makosa.

Jambo lingine wazee ambao wamefikisha umri wa miaka sitini na tano hadi sabini, waendelee kuangaliwa na Serikali kwa kupewa pesa za kuweza kujimudu maisha yao. (kitaita). Jambo lingine Commissioners, Katiba ambayo tunaandika iseme kwamba kila mkoa uwe na universities angalao tatu. Kila mkoa. Unaona sisi hatuna University. Vyuo vya walimu viwe angalao vitano kila mkoa. Sisi hatuna. Tuna moja tu ya Chanzu. Hii yetu imekufa ya Marimbei na hakuna anayefuatilizia. Vile vile kila mkoa ama district iangaliwe na industries kwa sababu tuna vitu vingine perishable ambazo vingetengezwa katika hali ya ki-district katika zile industries ambazo tutakuwa nazo.

Uchaguzi wa mwenyekiti na Mayors uwe direct, wananchi wapige kura wenyewe wachague watu hao. Sio ma-councillors pale ndani. Ndugu zangu, Katiba ya zamani iliyokuwako ilikuwa na Vagrants Act. Sisi siku hizi tunaishi na watu wa kila aina. Humjui ametoka wapi? Alifanya makosa gani? Wapi? Lakini tuko na wao. Tungependa hii Vagrants Act iwekwe ili mtu akifungwa apewe nafasi aende nyumbani aripoti huko. Ilikuwa hivo zamani.

Ndugu zangu tuna tashwishi. Ndugu zetu Commissioners wameomba muda wapewe miezi kumi na nane. Watumie 0.5 billion. Ningeomba kwa sababu hawa ni watu waliosoma, Prof. Ghai, Prof. Wanjiku, Ma-lawyers, Dr. Ombaka na ma-historians wako hapa. Kweli hawajui historia ya Kenya? We simply adapt Majimboism Constitution maanake ilikuwako. Ilikuwako kabisa. Lakini werevu wakaifungua ili wafanyeje? Wapate nafasi kunyakua vitu vingine. Kwa hivyo ningeomba hiyo 0.5 billion zilipwe walimu ambao wanalia kwa mishahara enzi hii yao ya pili ambayo wanapata shida. Ningeomba hivyo, iandikwe kwa sababu ninaomba.

Katiba mpya hii tunayoitengeneza kuwe na kipengele kinasema lazima wananchi walime. Lazima wananchi walime. Vile Kabarage Nyerere alivyosema, tuwe na kilimo cha kufa na kupona. Kuwe na kipengele hicho. Maanake kitakuwa ni sheria utaulizwa '*mbona hujalima'* ? Lakini sasa tunangoja mpaka mahindi ya msaada na mashamba yote yamekuwa manyasi. Kwa sababu tunajua kuna nini? Mahindi ya msaada. Hii ifutiliwe mbali.

Katiba hii tunayoiandika iangalie mambo ya walemavu, wajane na vile vile wasiojiweza kifedha. Katiba hii tunayoandika mpya tuone kwamba katika Kenya kusiwe na wizara moja, mawaziri wawili. Hiyo ni makosa. Wizara moja mawaziri wawili. Hiyo ni sawasawa kweli? Iwe wizara moja, waziri mmoja.

Na vile vile kuwe na kazi ya mtu mmoja, sio kazi mbili awe na moja. Kuna watu wamesoma sana lakini hawana kazi. Kazi moja mtu mmoja. Unakuta mtu ni Commissioner, tena ni director tena sijui ni chairman, sijui ni executive nani. Viti vyote vimemzingira katika hema hiyo. Jambo la kushangaza tunasema tunataka tunataka……hii mbuga za wanyama ningependelea kwamba tuombe kilomita kumi mraba ndani ili tuwe na sisi na Game Reserve. Wawe na National Park yao lakini tuwe na Game Reserve. Kama vile Masai mara wao wanapata pesa councils zako very rich.

Lingine ambalo linaumiza roho sana ni Mines Act. Mines Act. Sheria ya mining. Katiba hii tunaandika igeuzwe kwamba wananchi wamiliki migodi yao wenyewe. Kwa mfano wengi wao ni maskini wa mwisho. Wachache ndio matajiri. Na si wa pale pale.

Mikapa irudishwe vile ilivyokuwa. Commissioners hivi ninavyosema pale tulipokuwa Tausa juzi unakuta kwamba ndio kama headquarter ya watu wa Msau hapa. Watoke hapa waende kuchukua vitambulisho pale. Hiyo si mzuri. Mipaka ilivyokuwa mbeleni ibadirishwe na wananchi wenyewe waseme wanataka wawe wapi. Mbeleni walikuwa Wundanyi Division, sasa wako Mwatate division na sasa wako Tausa division. Tungeomba hiyo ibadirishwe itawasaidia sana kwa sababu they are being punished na resources zao zinaumizwa sana.

Last but not least ni kwamba ningeomba uhakikisho. Kwa sababu Tume hii pengine hata kazungumza mtu, tuliona Yash Pal Ghai na nyinyi mlikuwa na groups hivi. Pengine mtuhakikishie kwamba maneno tunayoandika hapa yasiende ikagawanywe yafike vizuri ili tuweze kuwa na uhakika wa mambo haya. Kwa hivyo sina mengi ndugu zangu Katiba ni ya *majimbo*. Asanteni sana.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Mwangeka. Na maoni yenu itafika vizuri, hatuwezi kuwagawanya. Na Mwangeka tukimaliza kuandika ripoti tutairudisha na mtaangalia muone kama vile tumeandika ni vile mlisema. Asanteni. Bwana Wilson Nyambu Chola.

**Wilson Nyambu Chola:** Niko na memorandum.

**Com. Kabira:** Okey. Kwa hivyo utapeleka na uta-sign. Asante sana. Na mwingine Bwana Javis Muchila.

**Javis Muchila:** Basi mwenyekiti wetu wa Katiba na wananchi watukufu wenzangu nawasalimia nyote, hamjambo. Basi mimi sina maneno mengi bali nataka kusema ya kwamba mazungumzo yaliozungumzwa na msemaji wa kwanza na wa pili ni kama yale ambayo tunarudia kwa sababu hii area moja. Lakini nina machache pengine ningetoa; yaani ni na maneno machache ya kuzungumza hapa. Kwanza nataka kusema ya kwamba Serikali yetu tukufu kulingana na Katiba haikuwa sawa kwa sababu tumeona ya kwamba mtu mmoja ambaye ni Rais yuko juu zaidi. Na mara nyingi tunasema juu, juu, juu zaidi. Nasema ya kwamba Katiba hii iwe na kipengele cha kusema kwamba kila mtu wa aina yeyote katika Kenya hii awe chini ya sheria. Ni mkuu wa upande fulani lakini awe chini ya sheria.

Na kitu ya pili, Serikali yetu iwe ya majimbo. Twataka *majimbo* maana mara nyingi sisi hasa watu wa Pwani, tuna rasilimali zetu nyingi ambazo zinakwenda hivi hivi hatujui zinatumika vipi. Hakuna misaada yeyote. Nikitaja katika wilaya hii ya Taita Taveta ningetaka kusema ya kwamba tuna rasilimali nyingi sana lakini ma-development ya wilaya hii hakuna, hayaonekani kabisa. Sijui gao hilo huwa linagawanywa namna gani.

Tunaona karibu kila kitu hakionekani sawasawa. Watu wa pwani tunaambiwa kwamba tumelalia masikio. Tunaambiwa hatuna mawazo. Tunaambiwa hatuna chochote cha kutufanya kwamba tunaweza kuomba kila kitu ili tupate. Kwa nini tuombe na hali mali nyingi inatoka pwani hii halafu inakwenda kutumiwa katika Central Government na inagawanywa kwa sehemu zingine. Kwa hivyo tunataka majimbo yawe mojawapo katika Katiba hii.

Kitu ya pili ni hii utawala. Nimejaribu kugusia madogo madogo hivi. Utawala wetu naona uko mzito zaidi kwa sababu ni utawala wa kiamri. Nataka kusema ya kwamba kuanzia hawa tunawaita akina *mwalugongo* watu wetu wadogo wawe wanachaguliwa na watu. Lakini mahali pengine wananyakuliwa. Assistant chief na chief wanakuwa ni kama wako mbali na sisi. Sasa zile kazi haziendi sawasawa. Amri mpaka apewe ya kufanya kitu fulani ndipo kazi ifanyike. Tunaomba wachaguliwe na mwananchi. *Mwalugongo* wetu, yaani wale village elders, wachaguliwe na mwananchi. Assistant chief achaguliwe na mwananchi kwa secret balloting. Chief achaguliwe na mwananchi kwa secret balloting. Mambo ya kusema kwamba anapeleka application halafu anaandikiwa huko, sisi tukiwa hapa nyumbani ni kama paka na panya, mambo hayo naona hayafai.

Nikiingia katika utawala, nikija ofisi ya Bwana DO nasema iondolewe. Hiyo ofisi nimeona tu ni ngazi ambayo haisaidii chochote. Haibebi chochote. Kila kitu kinatoka katika ma-location lakini ikifika hapo kinakwama. Hakiendi mbele. Unakuja kushitukiwa kwamba pengine 'Ooh nilipeleka maneno lakini hayakufika.' Wengine wanaohusika hapo katika mikutano mikubwa ya district ama ya wilaya hawa-fit kutuwakilisha sisi wananchi. Kwa hivyo mimi naomba katika Katiba yetu hii inayofanywa ofisi ya DO sioni maana yake.

Ofisi ya bwana DO 1 naiona iwe hapo. Kwa sababu kutoka ma-location hiyo ndiyo ya kupokea mambo yote ya wilaya katika zile locations za wilaya hiyo. Halafu aketi na Bwana DC aliyeko hapo wazungumze jinsi ya kutekeleza sheria za nchi. Kutekeleza kuangalia ma-civil servants na vile vile mwananchi kulindwa kwa ulinzi wao. Mambo hayo yakiwa namna hiyo yatakuwa mazuri. Bwana DC asiwe mwenyekiti wa chochote. Yeye ni mfanyi kazi wa Serikali (civil servant) lakini mwenyekiti wa ulaya awe ni mtu aliyechaguliwa na wananchi wenyewe au pengine chairman wa county council. Asimamie mambo yote ya wilaya katika Kenya hii. Lakini asiwe Bwana DC. DC nikutekeleza tu kile ambacho kinatakikana.

Kitu kingine nasema kwamba katika utawala, kuna mambo mengi ambayo haifikii wananchi. Elimu inaweza kutolewa lakini unakuta huko nje inakuwa ni mambo ya kusumbuana sumbuana hasa tukiingia katika hii mambo ya pombe. Utakuta mwananchi anaweza kukataa hataki pombe lakini sehemu zingine utakuta kwamba mwenye kutengeneza pombe na mwenye kutawala wameshikana, ni ndugu. Sasa mambo yote yaharibika hapo. Hata kama una ubaya wowote unaotendeka karibu na hiyo pombe hapo, ingawaje wananchi wengine wanapenda pombe kuoja kidogo kidogo, si makosa. Lakini utakuta kwamba jinsi inavyotawaliwa ile pombe hairidhishi mwananchi.

Kitu kingine ambacho nataka kuongeza ni kwamba katika Kenya yetu hii, rasilimali zote ziko mahali pamoja, na mwananchi yeyote ana haki ya kutumia. Lakini utakuta hakuna kipengele kinachosimamia malipo ya mbunge na malipo ya diwani. Mimi ni mmoja nikiwa diwani. Ingawa sijasema jina langu mimi ni Diwani Javis Muchila. Tunaona ya kwamba hatuelewi kwa nini kuna mabadiliko kama hayo ama mapendekezo kama hayo. Utakuta mbunge analipwa salary na Consolidated funds. Utakuta kuwa diwani, haya maokoto ya kutoka soko kidogo kidogo, viwanja vidogo vidogo hivi ndio inakusanywa na ndio unasikia napewa allowance.

Na mara nyingi mnasikia madiwani katika Kenya hii, wengine wamebaki na arrears. Sasa imekuwa ni fujo na ile fujo inaleta hii mambo ya kuchukua viwanja kwa nguvu. Mambo mengi yanaharibiwa kusudi kwa sababu wanaona kwamba hawako katika hali ya Kenya ya kusimamiwa vizuri. Naomba madiwani wote Kenya hii walipwe salaries kutoka kwa Consolidated funds.

Kitu kingine kinachofuata hapa ni mambo hasa katika Pwani hii tuna madini. Nataka hicho kifungo kiondolewe kabisa. Hicho kifungo kiondolewe kabisa na Katiba iwe kwamba madini yote katika wilaya, katika Kenya yote sio Taita Taveta zihudumiwe na Local Government. Isimamiwe na Local Government. Maana bado tunaona kwamba mali inakwenda nje, inakwenda inalipwa mahali pengine lakini utakuta katika county council hawapati chochote kinachohusu umilikaji wa mali kama hiyo. Kwa hivyo tunaomba Katiba kama hiyo iwe kama hivo.

Nakuja katika National Park. Wanaita ‘Royal’ sijui nini huko. Imepewa majina makubwamakubwa ili mwananchi ashtuke ama aogope. Kwa kawaida ni jambo la kufaidika. Mwenzangu alisema hapa, Mungu aliumba hata ametoa vifungu viwili katika biblia. Mungu aliumba kitu na kwao.Ni kweli tunajua sisi tumepewa wanyama watu wa Pwani.

Tumepewa madini. Tumepewa misitu kubwa kubwa yenye mali. Lakini utakuta ile mali inatoka hapo haisaidii mwananchi kabisa. Hata ni aibu kabisa kusikia kwamba Bunge sijui ilipitisha wakati gani ati mwananchi akiuawa na mnyama, analipwa elfu thelathini. Kama ambaye anakwenda kununua ng'ombe ya maziwa. Pesa kidogo sana. Napendekeza hapa kwamba mwananchi akiuawa na mnyama, alipwe milioni moja na kuendelea juu.

Ng'ombe ya mwananchi ikiuawa na mnyama wa porini, maana imekuja kumchokoza nyumbani kwake, alipwe elfu thelathini. Na National Parks kutoka leo tukiwa tuko hapa kutengeneza Katiba iwe totally under Game Reserve. Hakuna mambo ya kusema ati tunaomba. Hakuna mambo ya kusema ati tunakwenda ku-beg kwa nani. Sisi tuko hapa Pwani, tuko Taita, tunataka mali hii iwe rasilimali ya Mtaita ili pesa zipatikane. Shule zetu zimekufa nyingi. Watoto wetu wanapita kwenda universities lakini county councils haina pesa. Pesa zinakwenda zinakuwa cycled sijui pande gani, hatuwezi kujua. Tunataka hiyo mambo iwe hapa.

Na kitu kingine nasema ikiwa pengine haitakuwa Game Reserve kama hiyo point A. Point B tuna hii Tsavo West katika National Park iwe Game Reserve ipatiwe nguvu. Part 3, ikiwa wamekataa kabisa katakata, 50% ya rasilimali kutoka katika National Park, iingie Taita, isaidie Wataita. Lakini kitu tunataka zaidi ni yote iwe Game Reserve.

Na lingine ni mipaka yetu. Hii mipaka yetu ilikuja kufurugwa tu na wakoloni. Wale ambao walikuwa ma DC katika wilaya hii. Ndio wametuharibia kabisa. Kuna wakati hii Centre ilikuwa ina-work lakini wakatuharibia huko sehemu ya Taru huko chini ndio kuna shrine, holy places za Wataita wako hapo. Hata tukitoa wengine hapa wanaweza kukwambia hapo ukichimba hapo utakuta kitu fulani hapo. Utakuta nyunge fulani iko hapo ndani ambayo alikuwa anajua kwamba hapa ndio mpaka wangu kutoka huko Taru mpaka Mtito andei. Lakini wakoloni wameturukia na tumekosana na hiyo. County councils ilitoa kamati yake ikazunguka ikizungumza na wananchi, ikiwaambia ukweli ukweli na ikatoa ripoti ikaenda Parliament lakini hakuna chochote kilifanyika. Kwa hivyo tunaomba kuwe na kifungu ile Act ya kusema kila wilaya katika Kenya iwe na haki zake sawa sawa kama ilivyokuwapo hapo zamani. Sio wakati wa sasa.

La mwisho nasema kwamba kuwe na control ya rates. Maana nimefikiria kwa mbali nikaona ya kwamba hii mambo ya kuwa soko huru kumeleta shida. Mwananchi wa kawaida anashindwa hata kufikia ile bei ambayo inauziwa mtu sawasawa ambaye yuko juu, pengine ana hela za kutosha. Na yule ambaye ni wa chini unaona kwamba wananunua kitu sawa.

Pili, biashara nyingi unazikuta zimenyakuliwa na watu wengine. Wananchi wa hapa hakuna. Hata hali hiyo imeendelea mpaka tukawa na *manamba* katika nchi hii ya Kenya. Sijui *manamba* walitoka fulani. Sijui kuna Act fulani katika Parliament. Kama kuna Act katika Parliament iondolewe. Utakuta hata ukienda Taveta, utakuta mwananchi wa kawaida amekwenda kununua vitu vyaake Taveta kuja kufanya biashara zake ndogo ndogo hapo. Baada ya kununua vitu na kuviweka hapo, anaambiwa na manamba, 'weka chini kila kitu' zinahesabiwa halafu unaambiwa utanipa shilingi mia moja ishirini, ama mia mbili au mia moja.

Ndipo yeye mwenyewe tena apate. Wewe mwenye vitu vyako unajua una ruhusa kabisa. Sijui sielewi kwamba Katiba yetu inasimama wapi. Inalinda mwananchi namna gani. Ingawa tunasema kwamba Katiba inalinda mwananchi, mwananchi wapi, ama kivipi? Kwa hivyo mambo hii ya *manamba* tungesema katika Parliament katika Bunge, katika Katiba iondolewe. Haistahili chochote. Mtu ananunua gari anaandika driver, msimamishi wa gari ile ingine, conductor wake afanye kazi. Lakini utakuta hali ya kusumbua sumbuana imekuwa na shida. Kwa vile mengi yako hapo, kwa haya machache nashukuru.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Javis Muchila na sasa tutamuuliza Bwana Nathaniel Kiungu. Nathaniel Kiungu ako? Okey.

**Nathaniel Kiungu:** Mimi kwa majina naitwa Nathaniel Kiungu. Na zaidi hasa mimi nachukua yule msemaji wa kwanza na wa pili. Hayo yote ambayo yamesemwa hapo ndiyo ambayo nayaunga mkono kikamilifu. Na vile vile,ningetaka kuongeza jambo fulani hapo. Kuhusu hasa mambo ya elimu - elimu hii ya kutoka madarasa ya chini yaani elimu ya msingi. Ningeomba kwamba iwezekane iwe ya bure. Hasa kutoka nursery hadi hata ikiwezekana mpaka form four. Kwa sababu watoto wengi wamekuwa hawakuendelea kielimu kwa sababu ya pesa. Wazazi hawawezi kujihudumu kupata pesa. Kwa hivyo ningeomba tu ikiwezekana iwe hivyo. Hilo ndilo ambalo nilikuwa nataka kuongeza.

**Com. Kabira:** Asante sana. Si utaandika jina? Okey. Thank you very much Bwana Nathaniel na tutamuuliza Stephen Mganga.

**Stephen Maganga:** Ndugu Commissioners nawananchi ambao mko hapa, kwa majina naitwa Stephen Maganga. Niko na written memorandum ambayo pengine nilikuwa tu nizungumzie machache habari ya hiyo mambo nimeandika kwa sababu ya muda. Kitu ambacho nilikuwa nataka nizungumzie ni kuhusu hii elimu (education), ni kwamba elimu, kuwe na elimu ya bure kwanzia shule ya msingi hadi chuo kikuu. Kitu kingine ambao ningeongea habari ya elimu ni kwamba mvumo wa 8-4-4 uondolewe na badala yake kuwe na mfumo wa7-4-3-2 kama vile ilivyokuwa zamani. Kwamba walemavu pia (hao disabled) wapewe nafasi ya elimu bure kwanzia kiwango cha chini hadi hata kupitia chuo kikuu.

Kuhusu mambo ya afya ningependa kuzungumza ya kwamba matibabu ama madawa yawe bure katika hospitali zote za KiSerikali. Pia kitu kingine ambacho pengine ningelizungumzia juu yake ni habari ya afya,  kwamba madaktari wa hospitali za Serikali, wasiruhusiwe kuwa na mahospitali ya kibinafsi (private clinics). Badala yake wawe na mishahara ya kufaa ili hali bora ya kiafya iwe ikidumishwa.

Nilikuwa pia nizungumze habari ya rasilimali za watu wa Pwani. Watu wa Pwani wana bahati kwamba wametunikiwa kuwa na nafasi nyingi ya rasilimali tofauti tofauti kama mambo ya utamaduni, ardhi, madini, mbuga za wanyama, msitu na kadhalika. Rasilimali ambazo ziko hapa Pwani ningependekeza kwamba iwe watu wa Pwani wapewe first priority wawe wakisimamia hizi shughuli zote kama za madini, mbuga za wanyama, mambo ya bandari na kadhalika.

Kitu kingine ambacho ningezungumza ni upande wa mawasiliano. Kuna matatizo katika hali ya mawasiliano katika sehemu hii ya

Pwani. Utakuta kwamba sehemu zingine zimesahaulika kabisa hali ya kibarabara na hao pia ni watu ambao wanatoa kodi ama wanalipa ushuru katika Serikali katika kodi. Ningependekeza kwamba hali za barabara ziwe zote zinaangaliwa sawasawa vile ambavyo pande zingine zote zinavyoangaliwa.

Kwa mfano, nitawapatia mfano mmoja, barabara kama hii ya kutoka hapa kwenda Rong'e juu ni barabara ambayo imesahaulika kabisa. Ni watu ambao ni wananchi wa Kenya lakini wana bahati baya kwamba miaka yote wana matatizo ya barabara. Hayo nilikuwa nataka nizungumze ni machache, mengi yameandikwa katika hii memorandum. Asanteni sana.

**Com.Prof.Wanjiku Kabira:** Asante sana Bwana Nathaniel. Natutasikiliza Bwana Norman Mwairuva.

**Norman Mwairuva:** Bwana mwenyekiti, Commissioners na maofisa wote. Yale ambayo nilikuwa nataka kuzungumza.

**Com. Kabira:** Taja jina kwa sababu tuna-record.

**Norman Mwairuva:** Mimi naitwa Norman Mwairuva. Yale yote nilikuwa nataka kuzungumza yamezungumzwa na mtu wa kwanza na wa pili. Kwa hivyo kwa hivi sasa sina lingine lolote la kuzungumza. Isipokuwa tu naweza kutaja kama mambo ya elimu iwe ya bure kutoka msingi mpaka kidato cha nne. Halafu na walemavu wafundishwe bure pia na wasibaguliwe kabisa. Hayo nafikiri yanatosha.

**Com.Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana Bwana Mwairuva. Halafu tutamuuliza Bwana Kenneth Mwarema.

**Kenneth Mwarema:** Asante sana yale yote nafikiri yamezungumzwa. Kwa jina naitwa Kenneth Mwarema kutoka hapa Msau. Sanasana nilikuwa nataka kugusia ingawaje yote yamesemwa, National Park. Tunaona National Park tunadhulumiwa especially hapo Taita Taveta. Barabara zetu pia tunaona ushuru unatolewa lakini hakuna manufaa kwa upande wetu. Barabara zetu mbovu. Hayo ndiyo ninayo kwa leo. Asanteni.

**Com. Kabira:** Okey. Asante sana Bwana Mwarema. Vincent Babu. Bwana Babu.

**Vincent Babu:** Professor na Ma-Commissioners wote, akina baba na akina mama, kwa majina naitwa Vincent Babu. Mambo mengi yameshaongewa lakini naweza kuchangia maneno mawili matatu. Jambo la kwanza ningeweza kusema ni kuhusu kulikuwako na sheria ambayo ingemwezesha mwananchi aliyemchagua mbunge, yaani mbunge wako uliyemchagua, tuwe na uwezo ikiwa hawezi kunisaidia kuwepo na uwezo wa kuweza pia kusimamisha kazi. Isikuwe mpaka tungoje baada ya miaka mitano anakudhulumu halafu tunasema mpaka tungoje miaka mitano. Huo muda ni mrefu sana.

Jambo la pili ni jambo moja lilozungumziwa, watu wamezungumzia mambo mengi juu ya walemavu. Kitu moja ningetaka

kuchangia ni kuhusu sisi vijana hasa wa miaka kumi na nane hadi miaka thelathini. Ningeomba sana kama Serikali ingekuwa ina njia ya kuweza kutusaidia. Ijapo kazi hakuna lakini ningependekeza kupata hata kama ni fidia ndogo ya kuweza kutusaidia kimaisha. Kwa sababu wakati mwingi tunaambiwa tungojee DO. Lakini hata wewe nyumbani ikiwa utamfuata baba yako umwambie shati imeisha, akikwaambia mfuate mjombako utashindwa kwa ni yeye alinizaa kwa nini. Kwa hivyo yangu ni hayo machache.

**Com. Kabira:** Asante sana. Thank you very much Vincent. Jacob Kisombe.

**Jacob Kisombe:** Kwa majina naitwa Jacob Kisombe(Makarios). Mimi natoka sehemu ya Rong'e juu. Karatasi zetu zimeletwa hapa lakini nimeona mengine yamesahauliwa. Na mimi kama Kisombe nataka nipate nafasi hii ya kujaza hayo yaliyosahauliwa. Jambo la kwanza, sijui huko nyuma yangu, sijasikia mtu yeyote amezungumza juu ya umaskini. Yaani specifically umaskini. Ma-Commissioners na nyinyi nyote mnajua umaskini umeingia nchini Kenya sana sana. Hata umezua mambo mengine ambayo hakika hatungeyategemea kuyapata, kwa shauri ya umaskini. Sasa huu mpango uliowekwa na Serikali wa kupunguza umaskini ni wa uwongo. Ni njia tu za kumangamanga mangamanga kuhanyahanya kuhanyahanya. Turidhike ati umaskini washughulikiwa. Njia zenyewe hata ukielezwa huwezi kuzielewa. Pesa zimepurwa kwa kiasi ambacho hatuwezi kueleza. Na wale watu bado wanatembea na milioni moja mfukoni katika briefcase, wanatembea mji mkubwa. Wanakwenda London, Japan, wanarudi. Hawajafikishwa kortini bado. Wale ndio waliopura pesa ambazo tunazitumia sisi tulio maskini. Leo zinatumiwa na watu wachache.

Kwa hivyo basi maoni yangu, naomba nyinyi wasikizaji nyote ambao ni maskini kama mimi muyaunge mkono kwa dhati kwamba, Serikali yetu impatie kila mwananchi aliye na kitambulisho ambaye amefika umri wa miaka thelathini apewe milioni mbili. Msishangae! Najua mtasema Serikali haina pesa, haina nini. Wewe ni nani unasema Serikali haina pesa. Serikali itazumbua pesa maanake tumeingiwa na umaskini na ufukara juu yake. Mnajua maana ya ufukara? Tofauti ya umaskini na ufukara?

Ufukara ni kitu kibaya sana sana. Hadi unashindwa kama Mungu yuko. Unashindwa kujua kama mimi natawala kwetu. Kwa hivyo kila mwananchi mwenye kitambulisho na mwenye umri wa miaka thelathini na kuendelea juu apewe milioni mbili. Fanyeni hesabu na komputa, mfanye na nini iwe hivyo.

Najua italeta maswali mengi. Inflation, vipande vitakuwa nyingi ambazo hazina kazi na nini na nini. Inflation gani? Inflation ililetwa na Serikali yenyewe.

Wakatengeza pesa Kasarani, zikafurika mitaani kila pahali, inflation phew. Kumbe inaleta nini? Umaskini. Ukienda benki utakuta Central Bank iko ripoti imetolewa. Pesa za Kasarani zimejaa tele mpaka leo hazijalipwa. Lakini kwa sababu President ana ile sheria yake sijui yaitwaje. Aliambia Central Bank ikubali hizo pesa halafu tutafikiria habari yake. Mpaka leo hiyo habari

haijafikiriwa. Hiyo ripoti tutaijua! Nani ameleta ufisadi? Aliyekuletea umaskini ni nani? Ufukara ni nani? Ni hiyo hiyo Serikali ambayo tunaitaka sasa ampe mwananchi yule ambaye hajaridhika, ambaye ana taabu shilingi milioni mbili. Asilete sababu nyingine nyingine zozote. Mwasema je hapo wananchi?

**Audience:** Ndiyo.

**Jacob Kisombe:** Hakika. Now, najua itakuwa sherehe moja ya ajabu sana. Huyo mwananchi na hizo pesa, atoe maumivu yote alikuwa akiyasikia akiwa bado fukara. Anywe pombe, aoe wanawake saba, afanye nini, aseme Alhamdulillahi Mungu kweli uko. Umetuletea centi ingawa na sisi tufanane na wengine. Mnipate sawasawa. Milioni mbili kwa kila mtu ni peanuts kwa uchumi wa Kenya. Hizo si pesa za kutajwa. Kuna watu wanatembea kwa kila briefcase iko milioni moja taslimu kila siku. Kwa nini yeye. Mungu alimbariki ki vipi? Hapo najua mumeniunga mkono. Asante sana.

Lingine ni hili. Katiba nataka ikiwezekana na nafikiri yawezekana. Ianze kusomesha watoto kutoka nursery. Ajue anaishi nchi ipi, namna gani, nchi yake iko je, ana uhuru gani. Haki zake aanze kuzijua akiwa nursery. Afundishwe mpaka afike vyuo vile vyote vya mwisho. Hilo ndilo swala langu lingine. Nazungumza habari ya utungaji mimba. Imekuwa ni mchezo watu wakizalishwa tu ovyo ovyo hata afadhali paka yeye ajichunga na watoto wake na anaketi na wao mpaka wakawa wakubwa. Watoto wanazaliwa kiholela. Uhuru umekuwa mwingi wa watu kuchezea mili ya watoto wengine hata wadogo na kadhalika. Zamani ilikuwa sheria ilikuwa inaitwa ‘Affiliation Law’. Mwaikumbuka?

**Audience:** Ndiyo.

**Jacob Kisombe:** Imekwenda wapi siku hizi mbona haifanyi kazi! Kwa nini haifanyi kazi? Nitawaambia kwa nini haifanyi kazi. Kwa sababu wale wale wabunge, wale wenye pesa, wale wenye vyuo vikuu na nafasi zao ndio wanaharibu hao watoto. Wameanza kuwafundisha pesa. Pesa kubwa kubwa. Mtoto hajaona shilingi mia moja naye ni mdogo asha pewa tayari, na hajajua shilingi mia moja ni kusema je. Sasa ile Affiliation Law iliyokuwako wakati wa mkoloni irudi upya na iongezewe kachumbari juu yake. Izidi kuwa kali. Watoto wanafurika mitaani wamezaliwa kiholela ovyo ovyo. Machokora wameletwa na mambo hayo. Tutafanyaje? Ile sheria ukitia mtoto wa watu mimba, utasomesha yule mtoto mpaka afike pahali anapotaka. Hapo je? Sawa.

Jambo lingine nitaongezea kwa wenzangu walivyosema; wanyama, mbuga zetu, mali zetu na mimea yetu, bado hatuitumii kikamilifu. Kuna mimea mingine imetiliwa sheria ambayo huwezi kutumia tunda hili, tumia tunda lile. Na huu ni mnazi. Ule mti unaoitwa mnazi. Hakuna hata theluthi moja ya ule mti unatupwa. Nyinyi mnaojua maana ya mnazi. Hakuna kitu hata kimoja unaweza kusema hiyo ni *rubbish* katika ule mti. Na huo mti ulikuja kihivyo hivyo na wakoloni wakaunga mkono lakini sisi Wafrika sijui tukoje, tukaanza kuudharau. Ati mtu asinywe pombe ya mnazi. Yaani waniambia nisinywe maziwa ya ng’ombe wangu. Mwasikia hapo jamani.

Ule mti, ule mnazi ni kiburudisho changu. Lakini naambiwa kunywa *Tusker*, sikizeni mambo yalivyo ya ajabu hayo. Wafrika sisi sijui tumefika wapi, namna gani. Ati unywe *Tusker, Guinness,* C*astle, Whisky* na nini. Kwa nini? Na hatujasikia madhara yoyote yametokana na pombe ya mnazi. Kila nchi na kila kabila ina tembo yake ya kujiburudisha. Na tumeekewa vipingamizi vingi vingi. Imekuwa hata watu wanatengeza vitu vinavyofanana na C*hang'aa.*

Mtu wa Nyanza tembo yake maarufu ni *Busaa* na C*hang'aa* na walikuwa hawafi. Mimi nimefanya hizo kazi miezi minne na sijasikia mtu ameuawa na C*hang'aa.* Lakini leo imekuja tembo Nairobi sijui yaitwa *Kumi Kumi*, unakunywa mchana hivi saa ile wataka kwenda nyumbani unamwaambia yule bwana 'hebu tafadhali nipatie tochi nifungue ule mlango maanake nataka kwenda zangu. Kumbe amekufa macho. Anaomba tochi, na jua lawaka. Ni kwa sababu ana haja ya kunywa tembo ya kustarehesha kulingana na pesa zake lakini analazimishwa kwenda kununua G*uinness,Godown, Whisky, John walker* na kadhalika. Kweli tunaishi kwetu? Tu Wafrika tunashindwa kutengeza pombe yetu. Vilabu vilivyokuwa vikiendelea na revenue ilikuea inaingia ya kutosha.

Hata walikuwa wanatoa maziwa ya bure kwa nursery. Zile pombe tunazokunywa zetu, ndio nyumba zile za pombe zikaitwa vilabu. Hazikuitwa bar. Wajua kuna tofauti ya bara na club. Klabu ni pahali ambapo wale wananchi walio pale karibu karibu, wakutane jioni jioni, wauziane mashamba, waozane, wanunue ng'ombe, wacheke, waimbe nyimbo zao, wafurahi na kujuana hicho ndio klabu. Leo ule uhuru wa kuketi tule vitu vyetu tunazotengeza sisi wenyewe, haupo. Mnipate hapo sawasawa.
Kwa hivyo vilabu virudi fresh. Na uchumi utabadilika. Sisi tembo yetu ni ya miwa na *muratina*. Mito yote ni miwa mitupu. Inafanya kazi gani? Ni kutafunwa tu, kutafunwa tu. Lakini zamani watu walikuwa wanaandikwa kazi, anapata pesa yule mwenye klabu. Anasaidia maskini wenzake wale jirani. Shangazi zake na wajomba zake na wajukuu wengine ambao wamezaliwa hivi hivi. Vile vilabu virudi. Na hivi vilabu vilifungwa na President, na hiyo ndio sheria tumekataa hapa. President asiwe above the law. Si tumeshasema hapa. Iwe hivyo hivyo. Vilabu virudi haraka sana.

Narudia tena. Ile milioni mbili bado naikumbuka na ninasema tafadhali isipingwe na mtu yeyote. Kama wanajua kukopa pesa huko IMF, Central Bank wazipure. Mwasikia? Si pesa zatengezwa Kasarani, leo watengeze zingine na sisi tupate. Maana zilienda kwa siasa, na sisi tutengezwe zingine nasi tupate. Kwa hayo machache, shukrani. Asante sana kwa kunisikiza nyinyi nyote.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Makarios. Utajiandikisha. Bwana Philip Kisaka. Hayuko? Ako.

**Philip Kisaka:** Ma-Commissioners, waheshimiwa wote, mabibi na mabwana. Nafikiri mengi yamezungumzwa. Kwa majina ni Philip Kisaka. Mengi yamezungumzwa na wenzangu. Kwa hivyo singekuwa na la kuongezea. Bali yote nayaunga mkono.

**Com. Zein:** Ni muhimu ukisema mengi yametajwa na naunga mkono, hayajulikani ni mengi yapi. Taja yale unaunga mkono sio

lazima uyafafanue. Lakini taja kama kwa mfano; mzee alikuja hapa akasema mvulana akimtia mimba msichana lazima amlipe ridhaa na amsomeshe yule mtoto. Kama unaunga hilo mkono sema naunga hilo. Si lazima ufafanue. Lakini ukisema mengi yametajwa, yapi?

**Philip Kisaka:** Shukrani. La muhimu ambalo mimi nitalikazia mkazo ni mbuga ya wanyama. Mimi ningeonelea kwamba hii mbuga ya wanyama imekuwa kubwa kushinda wananchi pahali wanapoishi. Kwa hivyo hii sehemu ingine hapa kubwa irudishiwe wananchi na ndogo iwe ya wanyama. Lingine ningeongezea ni juu ya madini. Madini yahusishwe wananchi wa Taita. Na wale ambao si wageni wa kutoka nje ya wilaya ya Taita. Yangu ni hayo.

**Com. Kabira:** Okey. Asante sana Bwana Kisaka. Na sasa tutamuuliza Bi. Margaret Mwaluala. Margaret ako?

**Margaret Mwaluala:** Kwa wakuu wote na wananchi nawasalimu. Kwa majina naitwa Margaret Mwaluala. Uchungu mkubwa nilio nao moyoni ni kwa ajili ya masomo. Kwa kweli kabisa tumekuwa wanyonge kama hapa Taita. Mtoto anapopita kama nyumba yao haina uwezo, mtoto hawezi kuendelea mbele. Tumeona watoto wengi kweli wamekosa elimu. Mtoto ijapokuwa anataka kusoma, lakini hawezi kuendelea mbele. Hapo mimi naona uchungu sana. Na tunasikia kuna msaada unatolewa, pesa za maskini. Lakini hizo pesa hazitufikii. Unapoenda kuuliza hivi kuna pesa ambazo zinatolewa za bursary. Hizo pesa hatuzioni. Kweli huo ni unyonge mkubwa na mimi naona ni uchungu sana.

Tena natilia mkazo kwa ajili ya vijana. Kenya yetu tunaona vijana wengi wameharibika, wengi wanakunywa madawa ya kulevya, hata hizi bangi zimeharibu watoto sana. Na mimi nasikia uchungu kwa ajili ya vijana. Unaona mtoto amesoma sana, ameendelea kimasomo lakini amekosa hata matumizi ya kufaa katika nchi yao. Yaani bangi ndio zimeharibu watoto na madawa haya ya kulevya. Watoto hawana kazi, vijana wanazurura ovyo ovyo. Kwa hivyo hapo tunataka mtilie mkazo ili vijana hao waendelee kupata kazi kama watapata msaada zaidi ili wapate kufaidika na maisha yao ya baadaye.

Na tena lingine ni kwa ajili ya akina mama. Tunaona sasa kama ni biashara zile ndogo ndogo, wamama hawana uhuru wa kufanya biashara. Utaona mama amefanya kabiashara kadogo lakini utaona msasi amekuja anavuruga mama. Hataki mama afanye biashara kidogo kidogo ya kusaidia watoto nyumbani. Na tena unaona hakuna kazi. Waume hawana kazi. Tena ndio unaona watu wanasumbuliwa sumbuliwa. Kwa hivyo hapo mimi ninasikia uchungu. Sijui hapo namna gani. Kwa hayo najua ni hapo tu. Kwa majina naitwa Margaret Mwaluala.

**Com. Kabira:** Asante sana Bi. Margaret. Andika jina tafadhali. Tutamuuliza Bwana Robert M. Mugendi.

**Robert M. Mugendi:** Ma-Commissioners na maofisa wote ambao wamekuja hapa wanahusika na kazi hii. Wazee na akina mama nawasalimuni. Kwa majina vile mmesikia ni Robert M. Mugendi, ni mkaaji wa hapa hapa Mwakinyungu yaani Msau, Mwatate constituency. Kama vile mlivyosikia, watu waliotangulia wamesema mengi lakini kuna mengine hapa ambayo

ningependa hapa niyakazie mkazo.

Pendekezo langu la kwanza ni kwamba Katiba hii inayokuja iruhusu utawala wa *majimbo*. Sababu ni kwamba Serikali ya majimbo yatoa mamlaka kwa wazalendo wa pale pale kulingana na sheria na kwamba wanaweza kusimamia mambo yao wenyewe. Kila jimbo lipange miradi yake ya kimaendeleo kulingana na matakwa yao. Kutoa priorities katika mambo haya yote ambayo yanataka kuanza hivi mpaka mwisho.

Pendekezo la pili ni kwamba ningependa mambo ya kesi za mashamba, zishughulikiwe kisawasawa katika Katiba hii mpya. Sababu imenifanya niseme hivi ni kwamba, kuna kesi za mashamba ambazo zimeachiwa wazee, na hawa wazee hawana wajualo kisheria. Mahali pengine sisemi ni mbaya saa ingine. Wengine ni wazee ambao wanakata vizuri halafu tena wazee wengine, wazee wa pale pale, wanaweza kukata shamba wapatie mwenyewe kisawasawa. Halafu waletwe wengine, yule amefanya mambo ingine pale, alete mwingine kutoka pale ili asili. Wanakuja watu ambao si wa pale. Hawajui mahali pale na waje wamnyang'anye yule mwenye shamba kwa sheria zao zingine.

Mimi ningependekeza hivi: Ikiwa kesi hizo zinachiwa wazee kama hawa, kuwe na mtu ambaye anaelewa sheria. Kuwe pengine na mwanasheria fulani hapo kufuatana na wazee hao. Ili wazee wanapokata kesi zao yule ajue kama kweli imekatwa kisawasawa. Na kama anaona kuna kitu fulani kombokombo pale, basi ashauri Serikali vile wazee wanakata mambo yao. Huyo mwanasheria awe kama ofisa hapo kwa wakati. Lakini anapo ona mambo hayaendi mzuri, a-report mbele na mambo yarudishwe yafanywe sawasawa. Tumeona kesi nyingi na watu wengi wamenyang'anywa mashamba. Tumeona kwamba tumesema kesi sawasawa kabisa na unaona ushahidi umetolewa sawasawa na mtu anakuja anasema hii ni ya kweli na ni ya hawa. Lakini mwisho uamuzi unapotolewa unaona kesi hiyo imekwenda kwa mtu mwingine. Au shamba hilo limekwenda kwa mtu mwingine.

Tena ningependekeza pendekezo la tatu kwamba mamlaka ya mikono mitatu ya Serikali yawe sawa. Yaani, three arms of the Government. Parliament, Cabinet na Judiciary yawe na mamlaka sawa. Tusiwe na mkono mwingine unanyanyasa mwenzake. Rasilimali za nchi zigawanywe sawasawa. Ya tano, viwanda hasa zile ambazo zinachangiwa na Serikali yenyewe, zizambazwe kila mahali kulingana na rasilimali za mahali hapo. Kwa mfano kama hapa kuna mawe ya madini. Kuwe na kiwanda hapa cha kushughulikia haya mambo ya madini. Na wakati wa kuandika watu basi 75% watakaoandikwa katika kiwanda hicho, watoke pale pale mahali. Ili kwamba kama kuna ujuzi zaidi ambao wale watu wa pale hawana, basi hiyo 25% ilete wale watu wa sehemu zingine waweze kujaza mahali hapo.

Jambo lingine ningependa kusema ni kwamba wakati tunasema *majimbo*, kwa hivyo *majimbo* yanashughulikia mambo yao kama ni barabara. Kwa mfano sasa mabarabara yetu kama vile yalivyo mabaya, tunapoambiwa pesa zimetolewa kwa wahandisi kutengeneza barabara. Wanapotengeneza barabara hiyo, ningependa kuwe na mtu wa hapo hapo mahali asimamie na atoe report ahakikishe kwamba hii barabara imetengenezwa ipasavyo. Maanake mara kwa mara pesa zinatolewa, kwa

mfano tulikuwa na mfano mmoja hapa karibu. Mawe inataandikwa katika korongo yanafutiwa futiwa tu. Mnaambiwa barabara inatengenezwa, maji yakija yanazua kila kitu. Kwa hivyo hakuna ufundi wowote uliotumiwa. Lakini kama tungekuwa na mtu wa hapa hapa angeweza kusimamia hapo na akasema 'hii tunajua maji yanayoteremka hapa yana nguvu sana, vile mmefanya haifai' na ingeweza kurekebishwa. Kwa hivyo naomba hayo muweze kuyatilia maanani hii mambo fulani…tuone katika Katiba ijayo kwamba inaendesha mambo tupendavyo. Asante.

**Com. Kabira:** Na Mzee Mwaliko ulisema umesahau mawili? Okey. Ulisema umesahau mambo mawili ulikuwa ukitaka kutaja.

**Edward Mwaliko:** Asante sana officer wa mambo ya Katiba leo. Hapa tulikuwa na mambo fulani ambayo yalikuwa lazima yaungane na yale ambayo tumetoa. Lakini wakati ule hii haikuwa imenifikia. Kwa hivyo imenifikia na kitu kidogo hapa ambacho kina tofauti kidogo ni kwamba haya mambo yanahusu utawala wa kutoka chini mizizini kwenda juu. Kutoka kule chini mizizini na kwenda juu. Sasa mmoja wa hawa ambao ……

**Com. Kabira:** Mzee waweza kutaja jina. Taja jina kwa sababu tuna-record.

**Edward Mwaliko:** Okey. Edward Mwaliko.Nilikuwa number two wakati wa kusema hapo mbeleni. Sasa wanasema kutoka kule chini hapa Taita tumewaweka akina *mwalugongo*. Ndio wanaendesha ule utawala kijijini. Nasema ikiwezekana hata wale watu kule chini wapewe mishahara. Hiyo tu ndio nimetajiwa. Kwa hivyo nitawapa hii.

**Com. Kabira:** Asante sana. Wale watu wa huko chini ni village elders au ni nani mzee? Village elders. Wale wa chini kabisa ni village elders?

**Edward Mwaliko:** Village elders.

**Com. Kabira:** Okey. Wapewe mshahara?

**Edward Mwaliko:** Yes.

**Com. Kabira:** Okey. Naumetupatia hiyo diagram?

**Edward Mwaliko:** Yes.

**Com. Kabira:** Asante sana. Thank you very much Mzee Mwaliko. Sasa tutamuuliza Naftali Mwadufu. Ako? Okey.

**Naftali Mwadufu:** Kwa mwenyekiti na wananchi kwa jumla, mimi kwa majina yangu naitwa Naftali Mwadufu na Yesu ni

Mwokozi wangu. Jambo la kwanza, nasikia katika moyo wangu lakini kwa ajili ya huyu Yesu, naona kwamba ni nyakati za mwisho. Nitazungumza kitu kama hicho. Namtege masikio sawasawa. Nautege masikio sawasawa.

Jambo la kwanza, nimelima shamba vizuri, nimetafuta madawa ya kuweza kuzuia wadudu, nimenunua mahindi kama ni maharagwe lakini imeoza yote. Je nimetoa watu wa kupandikiza hiyo shamba hata kama ni acre kumi ni acre ishirini. Hebu hiyo mbegu itamea. Sinapata hasara.

Kuhusu ukimwi, kwa Serikali yetu hii ambao naanza kama msingi. Ningeomba akina mama msikilize, unazaa mtoto, kumbe mtoto ana ukimwi. Nalea mtoto huwezi kujua kama ana ukimwi. Mnitegea masikio. Unampeleka nursery mtoto kumbe ana ukimwi. Mara ni hapa, sasa imefunikwa hata hawezi julikana. Mara ni kufua, inafunikwa funikwa vile.

Haya haitoshi, huyu sasa amefika darasa la nane anamaliza, kumbe anaumia ukimwi anamfunza sana anampleka wapi? Vilasi za juu, kumbe ana ukimwi. Hapo twajenga ama twabomoa? Mimi nafanya kazi ya business, nikiwa napimwa kila miezi tatu, kusudi ninapopikia watu chakula nisije nikawaambukiza. Je hapo, ningomba kama Serikali yetu inaweza, na inaweza, kwa mwaka kutokea vilasi vya chini vya msingi kwa mwaka mara tatu. Darasa la mwisho mtoto anapokwenda vilasi vya juu apimwe mara tatu ili ninapopeleka mtoto mbele yuko sawasawa.

Hivyo hivyo, waendelee kupimwa kupimwa ili tujenge Kenya. Si kumpeleka mtoto unafunza mpaka anaenda ng'ambo kumbe unapeleka mtoto mwenye abroad. Hiyo kitu inaudhi. Nilisikia uchungu sana hata nilipoingia hapa, niliona kwamba haya yako mbali, mimi naenda tu nisikilize lakini bahati nzuri, Mungu naye ni pamoja ni wanadamu. Yale ambayo naisikia uchungu nimkurushie kidogo huyo mtu, sisemi ni baba sisemi ni mama. Akaniambia ,'mzee haya mambo ndio sasa uzungumze kama unavyosikia.' Ndio nimetaja. Kitu hicho hakika nimeshangaa. Hata nimeiguzia,hata siku moja nikaiguzia katika baraza, lakini sikuweza kupata ibu.

Mungu wangu ambaye ameniokoa nikaona kwamba hakika tunapotembea sote ni vyema. Kwa maana neno la Mungu lasema "Ikiwa una kijani katika jicho lako, utatoa jani katika jicho la mwingine namna gani? Labda siku ingine watu wote ambao wamekaa kwenye viti ni wagonjwa lakini ni wakutekeleza. Jambo hilo…yangu si mengi, ni hayo tu, mawili. Watoto wawe wakipimwa kwa skuli hata kwenda juu ili wajulikane kwamba wako salama salimini. Mimi niwe na uhakika ninapotoa pesa, nihakikishe mtoto ni mzuri. Yangu ni hayo tu. Munisamehe.

**Com. Kabira:** Mzee, Utaandika? Asanteni sana. Tutamuuliza Daniel Mwachala. Bwana Daniel Mwachala ako? Ametoka kidogo. Ni sawa tu, tutarudi kwa yeye akija. Esther Mwavingwa.

**Esther Mwavingwa:** Mimi ni Esther Mwavingwa kutoka Rong'e sub-location. Kwa viongozi wote, mwenyekiti, na wageni na akina baba na akina mama hamjambo. Tumekuja hapa kwa ajili ya kutetea nchi yetu. Tumetoa matatizo mengi ambayo yako na

tumeonelea. Kwa upande wangu nimekuja kuongezea. Mengi yamesemwa na wenzangu, mengi tuliyaandikisha lakini jambo moja nilikuwa nalo la kwanza ni kwa sababu ya huu msaada ambao tunapata Kenya.

Huu msaada haututoshelei, maanake tunajua kula ni kwa kila siku. Lakini msaada unakuja baada ya miezi na miezi. Nilikuwa nikiomba, kama Serikali ingewezekana, hizo pesa za ghalama zote, wangetuletea kutufanyia ma-boreholes ili tupate kulima kwa njia nzuri. Ili tuwe na msaada wa kutosha siku zote maanake itakuwa ni juhudi la kila mtu kulima ipasavyo na apate chochote ambacho anatarajia. Huo msaada ungekuwa ni bora zaidi kwa wananchi kuliko kutarajia kuletewa msaada muda kwa muda usiowezesha mwanadamu.

La pili, ni kuwa nataka kutoa maoni juu ya viongozi ambao wanaongoza wananchi wao wawe wakikubali mahitaji ya wale ambao wanataka kuongoza kwa njia ifaayo. Kama ni mpangilio ya wananchi, kama ni mpangilio ya wanafunzi, wawe wakitoa malalamishi na wawe wakichukulia maanani.

La tatu, ni wageni ambao wanakuja mbalimbali na miradi. Kuna wengine huja wakihitaji wananchi wana miradi ya kuwasaidia, mojawapo ilikuwa ,Jua-Kali ilikuja wakati mwingine. Unahitaji wananchi, wanajitolea, wanajiandikisha, baadaye mtawaletea msaada, hakuna msaada utafikia mwananchi. Mnaanza kufanyiwa ma-seminar na ma-certificate mtapewa na mwishowe hakuna chochote. Ikiwa watu kama hao wanakuja kwa udanganyifu, inafaa wasije kabisa. Na Serikali ichukulie hatua watu ambao wanaingia kwa wananchi kwa misaada ya uwongo.

Elimu: Elimu imetajwa na watu wengi na elimu tunaomba izingatiwe sana, maanake shida zinaletwa kwa upande mwingine kwa ajili ya mahitaji ya kutokuwa na vyakula vya kutosha. Kama tukipata hizo ma-boreholes, tunaweza tukapata mali nyingi kwa mashamba yetu na tukawasaidia watoto wetu vile inavyotupasa. Pahali ambapo pana Jua-Kali, tunashindwa. Tuna mashamba ya kutosha lakini tunashindwa tukilima hatupati chochote cha kutosha. Kwa ajili ya mvua haiko ya kutosha. Kwa hivyo naongezewa. Ma-boreholes yapatiwe watu ambao wana shida. Hizo pesa ambazo ni za kutoa misaada kila wakati, zitumiwe kwa ma-boreholes ili tupate kufaidi.

Juu ya akina mama kwa miradi yao. Tunaomba wawe na uongozi wa kutosha. Wawe na kazi za kufana. Wawe na uangalifu wa kuangaliwa kwa njia nzuri. Maanake wengine hawajapata elimu ya kutosha. Wanachukua miradi yao kiholelaholela. Hawaelewi maana yake. Wakiwa na ma-officers kamili wa kuwaangalia na kuwaelimisha inaweza kuwa ni bora zaidi. Asanteni.

**Com. Kabira:** Asante sana Bi. Esther Mwavingwa. Na sasa tutamuuliza Elisha Mlivwa.

**Elisha Mlivwa:** Nawasalimu wote viongozi wetu wa kutengeneza Katiba, ndugu na akina dada nawasalimu wote. Nashukuru kwa kikao hiki cha kuweza kutengeneza Katiba yetu ya Kenya ili kusudi tukaweze kujitawala sawasawa. Neno kubwa ambalo nimelikumbuka nikilisikia zamani (naitwa Elisha Mlivwa). Neno nilikuwa ambalo nilisikia zamani na nikaona ni la maana mpaka

leo hii, Julius Nyerere Kabarage wakati anachukua hatua ya kutawala, alikuwa ameeleza watu wote kwamba ‘nataka nikitawala watu wote wawe na umoja na wawe wanaweza kuzungumza hata mtu akiwa mdogo sana’.

Kwa hayo aliendelea kusema na akafanya watu vikundi vikundi. Watu tisa, wa kumi ni kiongozi. Watu tisa, wa kumi ni kiongozi. Na watu shambiro, anakuwa tena kiongozi ambaye anaitwa kinara. Sasa mambo haya ilifanya watu kujuana na kupendana na kuwa kitu kimoja. Leo hii kuna shida moja.

Upande wa Biblia Mungu anasema kwamba watu wakiwa na nia moja, lolote watakalo omba kwa Mungu, hilo Mungu atalifanya. Kweli watu wanasema kuna umaskini, kuna shida lakini mali yote iko kwa Mungu. Na mtu anayezaliwa, huzaliwa na utajiri wake sawasawa. Kwani hii kitu kimoja kikubwa sana ambacho kinaleta shida ni ule uongozi. Uongozi umekuwa sehemu kubwa sana ambapo hawawezi kufikia hata wale walioko chini sana. Hata yule nabii aliyekuwa wa kwanza ambaye anaitwa Moses, alipokuwa anaongoza watu zaidi ya milioni, watu elfu mia sita, yeye aliona kwamba uongozi umekuwa ni mzito kwa sababu watu ni wengi. Hata siku moja alimgeukia Mungu na kumuomba ‘tafadhali ukaniue nisione shida hii, maana mimi siwezi.’ Hawa watu wote sikuwazaa.’ Kwa hivyo jambo hili linaonyesha kwa hakika kabisa lazima huu utawala ugawanywe visehemu visehemu ili uweze kufikia hata mwisho. Kiongozi yule mkubwa ameketi Nairobi mbali, hawezi kujua sehemu za ndogo ndogo kama mimi nimetoka hapa *Zogola.* Na hii *Zogola* nafikiria hata mkisikia hapa *Zogo,* hamjui Zogola ni wapi?

**Applause from the audience.**

Kwa hivyo tukijitawala sisi kidogo, tunaweza kujidumu na kujiongoza sawasawa. Na hiyo mali yetu ambayo tunasikia kuna mali nyingi, kuna mali nyingi hapa kuna madini, kuna wanyama wengi wanaitwa ‘national parks’ ambapo sasa wengine wanapata hizo pesa huko, hazifiki hapa kwa Wataita. Ni kwa sababu tumetawaliwa. Lakini tukijitawala sisi wenyewe, nafikiri tunaweza kufanya mambo yetu sawasawa na hawa watoto wetu wakasoma sawasawa na hiyo hali ikiwa hii ni magonjwa yanatokea huku na huku. Tutayaona sawasawa maana ni sisi wenyewe. Kwa hivyo jambo kubwa hasa ni hiyo *majimbo* tujitawale sisi wenyewe. Ni hilo tu.

**Com. Kabira:** Umemaliza? Okey asante sana Bwana Elisha. Mr. Donald Mwambi.

**Donald Mwambi:** Kwa mwenyekiti, maafisa wote ambao na wazee wote wamekuja kusikiliza Katiba, sisi kwetu tuliketi na tukaonelea haya machache.

**Com. Kabira:** Tafadhali taja majina yako.

**Donald Mwambi:** Majina yangu ni Donald Mwambi. Tulianza kama hivi: Rais awe chini ya sheria. Wilaya isimamie mambo yake yenyewe. Lingine, mtu akiuawa na mnyama alipwe milioni moja. Lingine, bei ya vitu iwe ikisimamiwa na Serikali.

Nikiendelea, ofisi ya DO iondolewe. Mzee wa kijiji achaguliwe na wananchi na awe akilipwa mshahara. Kuwe na chanjo zaidi kwa wananchi kuliko madawa. Madawa ya kienyeji yaruhusiwe katika hospitali. Elimu ya 8-4-4 iondolewe. Lakini kuwe na mitihani ama majaribio ya kila wiki. Wanafunzi wasome bure kutoka nursery mpaka kilasi cha nane. Yetu ni hayo. Asanteni kwa kunisikiliza.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Donald. Na sasa tutamuuliza Bwana Jackson Mudavida.

**Jackson Mudavida:** Kwa maofisa wetu wa Katiba na wazee wetu akina mama, hamjambo. Basi nashukuru kulingana na siku ya leo ya kupanga Katiba katika Kenya yetu. Nafikiri mengi yametajwa, yale ambao nilikuwa nafikiria lakini nitachangia jambo moja kwamba. (Jina langu ni Jackson Mudavida). Ninachangia jambo moja kwamba kuna mambo mengine ambayo tumeyaona kama yako kirahisi kirahisi lakini si rahisi. Na ningependelea mawazo yangu ni kwamba, haina haja ya kufaa shati na kama unafunga tai na viatu hauna. Hawa akina *mwalugongo* na akina ma-chairmen, ni watu ambao wanaanzia chini na tunawaona kama rahisi sana. Lakini kwa kweli watu wale wanashughulika sana.

Chochote kikitokea hata kama ni usiku tunaenda kuita akina *mwalugongo* ili apige filimbi au afanye nini. Kama ni chairmen pia vile vile kama ni wa shule. Ndiye anashughulikia shule ile. Kwa hivyo mapendekezo yangu mimi naona watu hao wanastahili kulipwa mshahara kwa sababu pale ndio chanzo cha elimu kwa chairman. Ofisa yeyote akija anamtafuta chairman, yuko wapi? Inakuwa ni *big name but no money*. Jina kubwa ambalo halina pesa. Yaani shule ile inastahimili kwa sababu ya chairman na chairman yule anachaguliwa na mwananchi, lakini naomba kama Serikali kama ingewaangalia watu hawa kwa mfuko ni afadhali. Kwa hivyo mengi sina. Yangu ni hayo. Asante sana.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Jackson. Natutamuuliza Godffrey Mwaivu.

**Godfrey Mwaivu:** Habari zenu. Wana-commissioner wa Tume ya Katiba yetu ya Kenya, tuna furaha sana……..

**Com. Kabira:** Tafadhali taja jina lako kwa sababu tuna-record.

**Godfrey Mwaivu:** Jina langu ni Godfrey Juma Mwaivu, mzaliwa wa Rong'e Malobeni. Ninatoa asante sana kwenu, kwa kuja, na kweli tumeona hii Katiba ni kweli itatimizwa ama ni malengo mengine? Maanake nikiangalia sana, Katiba ya Mzungu ilikuwa mbeleni. Ni Mzungu alikuwa ameandika hiyo Katiba lakini sijui sisi tukaja tukageuka, hata Mzungu akitoka ng'ambo akija, atasema mimi sikusema mfanye ufisadi. Katiba yangu nilikuwa nasema ni juu ya *majimbo*. M*ajimbo* kweli ni mazuri, lakini tuangalie majimbo iko ya kinamna gani. Maanake kuna *majimbo* ambayo itatuletea madhara kesho.

Yangu ya pili ni rasilimali ya mwananchi. Kwenye kugawanya ile ardhi ikiwa hapa Taita tuna ile County Council yetu, ipatiwe mamlaka ya pesa zile ambazo zinapatikana kwa Serikali. Ni aibu sana sisi Wataita tumekuwa ni wakarimu, na watu wa Mungu

kweli na tunaambiwa na kila mkubwa akija hapa ati 'angalieni nimempatia waziri fulani, waziri fulani, lakini hiyo bendera hatuioni na kitu yoyote hapa. Hatusaidiwi kabisa. Ukweli ni kwamba nataka kama ni Serikali itachukua hizi mbuga za wanyama hizo pesa zikija, sisi tupate robo tatu ya pesa hizo. Robo iende kwa Serikali. Iwe sawa.

Mila yetu ya mwananchi wa Kenya, yaani Katiba iundwe, kila mwananchi wa Kenya awe na haki zake; yaani mila yake ya kikatiba. Na mimi naona Bwana Ghai, hii muda wa Katiba nataka uongezwe kwa sababu Katiba ni kitu kingine chaa maana sana. Inakuja kutusaidia hata kesho. Hii habari ya kusema ati Katiba imalizike haraka, maanake kuna vipengele vingine ambao bado sisi hatujamaliza. Unajua maneno mengine ni ya kufikiria. Na unajua ikipitishwa, tukifanya haraka haraka, hii itakuja kutuumiza kesho. Na lazima tujue Katiba ni nini? Na hata watoto juu ya elimu yetu, tumeona hasa nursery schools ziangaliwe kabisa na Serikali. Kutoka Primary mpaka High School.

Sisi tumekuwa wanyonge, hapa Taita kweli tunalima chakula lakini hatupati chochote. Kwa kweli tungependa Serikali yetu ya kesho, itufanyie mashamba yetu, iangalie mashamba maanake tuna maji kutoka hapa L. Chala. Hii milima yote, hii maji, tulime na maji. Kwa sababu tuna njaa sisi. Maanake kweli tunapata msaada lakini huo msaada hautufai. Watu wengi hawawezi kwenda kwa chifu kwenda kuchukua msaada. Kwa mfano unaitwa uende ukachukue msaada, saa ingine utakuta haujaenda, si utalala njaa? Kwa hivyo kuwa na chakula yako kwa ghala ni mzuri sana.

Jambo lingine ni huyu mtu anaitwa M.H.E Mheshimiwa. Mheshimiwa ndio mwenyewe amemaliza mwananchi wake mwenyewe. Maanake tumemuogopa tunapoona ile bendera ikija hivi, tunakimbia. Mheshimiwa, labda hawa waheshimiwa wetu waongozwe na Mungu, wapatiwe hekima kutoka kwa Mungu yaani waokoke.

Wafanyi kazi wa utawala kama vile polisi. Polisi imefanya maneno yake mazuri sana. Lakini utakuta polisi, mtu amepelekwa kama cell, for example in Voi, wapi, utasikia Mheshimiwa atapiga simu kutoka Nairobi "Mwaachilieni huyu mtu mara moja". Kwa sababu ni mtu ambaye ana bendera, anaheshimiwa na polisi. Huyo ndiye mtu yule mfisadi mkubwa. Sasa ufisadi utakwisha ki vipi bwana? Ufisadi ni hapo hapo. Mtu anaweka milioni mbili, kumi kwa mfuko, na anaachiliwa na Serikali. Kwa nini Serikali inaachilia huyu mtu?

Na namweleza hivi Bwana Ghai, tafadhalini sisi unajua ni watu wa Mungu na tunampenda sana. Hii isiwe ni mara ya mwisho, tunataka mtutembelee tena. Hii seminar naiona ni nzuri sana, imetufunza maneno. Maanake nimeona maneno mengine makubwa sana. Tunataka kwanzia tangu tupate uhuru 1963 mpaka saa hii, Wataita hawajakula hata chochote hapa. Na ndio unaona milima yetu ina mawe, wazungu walikuja wakapima mawe hapa, hatujui, na wakaenda. Hawajatuambia ni nini iko hapa. Tuko tayari kuambiwa hata kama ni shamba yangu iko na mawe niambiwe iko hapo hapo. Niwe tajiri. Kwani nani anakataa pesa? Naona kama nimemaliza. Asanteni sana. Mwende vizuri. Mungu amubariki, tena mrudi hapa. Karibuni lakini mumekuja na wakati mbaya hakuna mahindi ile ya kuchoma.

**Com. Kabira:** Asante sana. Tutarudi wakati ule kuna mahindi. Thank you very much. Daniel Mwanyasi.

**Daniel Mwanyasi:** Kwa mwenyekiti wa kikao hichi, ma-commissioners na wananchi, kwa majina naitwa Daniel Mwanyasi, mkaaji wa hapa Msau. Mimi yale mjadala ambao tunauchangia, tulikuwa na mwakilishi na ashazungumza lakini mimi nitaongeza yangu mimi mwenyewe binafsi. Kwa hivyo mimi, kwa upande wangu ninapendekeza kwamba katika Katiba hii ambayo tunaitengeneza, Rais asipatiwe mamlaka zaidi awe juu ya sheria. Tunataka yeye awe chini ya sheria kama mwananchi wa kawaida. Na kukiwa na jambo lolote hata apelekwe kortini.

Tunataka Serikali za *majimbo*. Na katika mikoa yote iwe na ma-governors badala ya ma-PCs. Tupatiwe Regional Government ambayo tutakuwa na mamlaka kamili. Tutakuwa tukisimamia rasilimali zetu watu wa majimbo. Kama ni Pwani tuwe tunasimamia mali yetu sisi wenyewe. Ijapo kuna Central Government, lakini sisi tuwe na mamlaka zaidi na nguvu za kufanya yale tunayopenda katika mikoa yetu.

Tunataka wafanyi kazi wote wa Serikali ya Kenya wasipatiwe nafasi ya kufanya biashara ama chochote. Wawe wakifanya kazi tu. Maanake kule kupatiwa nafasi ya kufanya kazi, yaani hizo biashara na mambo mengi, wamechangia sana ufisadi katika nchi hii ya Kenya. Huduma zao zimekuwa duni na hawahudumii watu vizuri kwa ajili ya kuangalia masilahi yao wenyewe maanake ni watu wanafanya biashara. Wana tamaa ya kutajirika. Kwa hivyo wasipatiwe nafasi ya kufanya kazi. Iwe kama vile tulivyokuwa wakati wa ukoloni maanake ilikuwa sheria wakati huo, mfanyi kazi wa Serikali haruhusiwi kufanya biashara yeyote, hata kiosk.

Barabara zetu bado zimeharibika hata zingine hazipitiki. Tunapatiwa contract ati wanaokuja baada ya miaka sijui mingapi, wakati tumekuwa hata magari yenyewe yanashindwa kupita. Kwa hivyo county council ikipatiwa mamlaka ya kusimamia mabarabara itakuwa ni vizuri maanake wakati wa ukoloni, council ilikuwa ikifanya kazi nzuri. Walikuwa hawana machini kama tractor. Walikuwa wakifanya kazi na mkono lakini barabara zilikuwa zinatengenezwa vizuri kabisa.

Watoto mayatima ambao baba zao na mama zao walifariki kwa ajili ya ukimwi wamekuwa ni tatizo kubwa katika nchi hii. Kwa sasa hivi tunaona kwamba ikifika miaka elfu kumi ijayo, tutakuwa na matatizo makubwa. Maanake wameachwa. Serikali hakuna hazina yeyote ambayo imetenga kusaidia wale watoto mayatima walioachwa na wazazi wao. Imekuwa ni mzigo wa wale majirani walio karibu. Wakilala njaa ndio tunakimbia kuwalisha, kuwanunulia chakula na Serikali iko. Kwa hivyo Serikali iangalie hilo jambo, itoe kiasi cha pesa fulani, zitengwe ziwekewee katika kwa DC ili ziwe sikisaidia watoto mayatima katika ile area ambayo anafanya kazi.

Tukiingia upande wa elimu, tunataka elimu iwe ya bure kutoka nursery mpaka Secondary education. Na iwe ya lazima. Ya mwisho: hii mambo ya madini, migodi mingi tunaona inamilikiwa na wageni ambao si wananchi wa nchi hiyo. Kwa mfano hapa Taita, tuna mali asili ambayo ni migodi na imetajirisha watu wa nje kabisa na sisi tumebaki maskini; yaani wale ambao ni watu wa kuomba omba. Hiyo migodi inachimbwa ndani ya ardhi ya wale wananchi. Kwa hivyo wapatiwe nafasi mbele kabla ya mtu

wa nje kupatiwa nafasi ya kumiliki migodi hiyo. Kwa hayo machache nasema asante kwa kutupatia fursa hii kuja katika kikao hiki. Hii ndio democracia kamili tumeona kweli mwananchi wa kawaida amehusishwa katika kikao hiki. Ni asante sana Bwana mwenyekiti.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Daniel. Thank you very Daniel Mwanyasi. Bwana Joseph Muliwa.

**Joseph Muliwa:** Kwa mwenyekiti wa mkao huu na maofisa, akina baba na akina mama, hamjambo. Mimi maneno mengi yamesemwa yale nilikuwa nataka kuchangia. Lakini nitasema moja mbili. Yangu kusema ni hii ile ninachangia. Ninafurahi sana kwa Katiba hii ya majimbo na vile imezungumzwa na mimi nachangia hiyo ni sawa kabisa. Na yangu ile nitachangia ni hii. Ile imesemwa kila mwananchi katika vijiji walikuwa na sheria zao. Lakini mambo kweli imeharibika siku hizi, wakati wa huu muda unaendelea.

Kwa upande wa kinyumbani, tuna watoto, tuna akina mama. Sasa kweli mambo imekuja hii ya kujaza watoto holela holela na imetokana na mambo ile ilikuwa ya kiasili kuondolewa. Ilikuwa ikiwa mtoto wako amewekwa mimba na mvulana au na mtu yeyote, lazima amchukue. Kama hamchukui kulikuwa na sheria hivi: Yule mtu atalipa pale ng’ombe moja na ng’ombe moja dume. Itawekwa pale kwa wazee. Na hapo nikaona hayo mambo ndio iliopotea na ndio maana kuna njaa, watoto kuzaliwa nje. Kwa sababu mtu anakwenda anaharibu mtoto wako, anaachwa tu hivi hivi. Au anadanganya anamchukua nyumbani, anakwenda anawekwa mwaka mmoja hivi anateswa hadi anakimbia. Sasa wewe umepata hasara. Kuwe na msimamo kwamba mtu akiharibu mtoto wa mtu kwa hii Katiba yetu ya sasa, iwe na sheria , yule mtu aadhibiwe. Kuadhibiwa kwake alipe kama ni vile ilikuwa kimbele kwa akina babu, atoe ng’ombe moja na moja iende iliwe pale mbele ya wazee ndio aamue kama anataka kuoa sasa aanze kulipa mali. Ndio hii mambo itapungua.

Mtu mmoja alisema hapa, yule mtu akimzaa yule mtoto ndiyo nachangia huu mchango. Asomeshe yule mtoto mpaka amalize. Ikiwa yeye naye ni wa nyumbani hana chochote, atamsomesha na nini? Awe akitimiza yale yalikuwa hapo mbele. Na hapa ya pili nitasema hivi: Katika upande wa mashamba yetu na ardhi, sheria ziliwekwa zingine zakuwa zinaenda lakini hazilingani. Unaweza kuwa mlikuwa na kesi ya shamba na mtu na ukamshinda. Sasa mlisema ‘keti hapo’, mbele ya kijiji, wewe ukashinda, sasa inapelekwa mbele. Sasa pale mbele wale wako pale ni maofisa peke yao ndio watakula wamalize. Unasikia ‘wewe shamba itakwenda kwa huyu’. Na wajua nyumbani wakijijini walipitisha hii ilikuwa namna hii. Hiyo ilikuwa ni mambo isiyoridhisha. Yangu hayakuwa mengi ni hayo tu ninachangia. Maana mengi nilikuwa niseme, kwishasemwa na wenzangu.

**Com. Kabira:** Okey asante sana Mzee Joseph Muliwa. Na tutamuuliza Grafton Mwamba.

**Grafton Mwamba:** Maofisa, wazee na akina mama nawasalimu, habari yenu. Mimi kitu ninachochangia juu ya Katiba ni hii: Nataka Katiba hii iachiwe wananchi. Kwa sababu rasilimali zetu zinaenda nje. Tena ng’ombe ya mtu ikiliwa na simba ilipwe elfu thelathini kwa sababu wanyama hawa wanatoka huko halafu wanakuja kutuchokoza na kutuharibia mali zetu.

Jambo lingine la pili ambalo nitaongezea ni juu ya wasichana na wavulana. Wavulana wanaharibu watoto wa watu kwa makusudi. Akiambiwa mimi niko hali mbaya, hawezi kujali kwa sababu anajua tu hata nikimtia mimba hakuna mtu atakayenifuata kuniuliza "mbona umemfanyia hivi"? Tunataka vijana hao ama wasichana hao, akitia msichana mimba ashitakiwe na atoe mahari. Sina zaidi ni hayo tu.

**Com. Kabira:** Thank you very much Mr. Grafton. Natutamuuliza Flora Mshimba. Flora hayuko. John Mwakugu.

**John Mwakugu:** Kwa Tume ya Katiba na wananchi wenzangu hamjambo. Yangu si mengi kwa sababu naona wengine wametaja. Jina langu kama mmesikia ni John Mwakugu. Langu la kwanza ni jambo la mashamba. Hili jambo la mashamba ninasikitika kuona kwamba chairman wa mashamba ya wananchi kama ni district fulani, fulani, hata hapa ya Taita Taveta, utakuta district chairman anakuwa ni DC. Anakuwa chairman wa mashamba yetu.

Kwa hivyo hili ni jambo ningependa kwa Katiba lihakikishwe kabisa kwamba chairman wa mashamba awe ni mwananchi mwenyewe wa area hiyo. Si DC anatoka Kisumu huko, anakuja kuwa chairman wa mashamba yetu. Halafu anatupatia hasara, unasikia kwamba mtu ako Nairobi, anapata shamba huku kwa sababu amepitia kwa chairman. Lakini ingelikuwa ni mtu wa hapa hawezi kubali mashamba ya kwao kupatianwa ovyo ovyo namna hiyo.

Jambo la pili ni kwa mashamba vile vile. Sisi watu wa hapa Taita ama Rong'e kwa ujumla tumekaa kama watu ambao si wa Kenya. Wakenya wote wako na haki sawa. Tukiangalia kwa upande wa Kikuyu, wako na title deeds, ukienda area zingine title deeds zimepatianwa kila mahali. Lakini hapa Rong'e bado title deeds hazijatolewa. Kile kinasababisha sizitolewe hatujui ni nini na sisi ni wanakenya kama wale wanakenya wengine. Hivyo imechangia sana kwa upande wa umaskini kwa sababu hakuna loan tunaweza kupata kwa bank. Na tumekaa tu hatuwezi kujisaidia kwa njia yeyote.

Jambo la tatu ni la kutokana na Bunge. Tunachagua wabunge wetu wanakwenda pale bungeni halafu anaenda anarudishwa minister. Akirudishwa minister, sisi tuliomchagua ni kama tumekuwa crippled maanake hakuna jambo lolote letu sasa atawasilisha pale bungeni. Mbunge wetu ameenda amefungwa, amenyamazishwa. Kwa hivyo Serikali itafute njia yao kabisa ya kutafuta waziri wao. Sisi mbunge wetu ni mbunge wetu. Tusiwe tukienda pale mbunge wetu anarudishwa waziri.

Jambo lingine ni kodi. Wanakenya tunatoa kodi sote kabisa. Kila mtu anaenda dukani ananunua kitu fulani, analipa kodi ndani yake. Lakini kodi hii tunaona inaliwa na watu wachache tu. Leo hii Mkenya amefariki hapa Mombasa, hapa Nairobi, na ni mtu wa kawaida. Hakika watu wa kwao wasipomchangia, huyu mtu anapelekwa *majimbo.* Anakuwa ni mtu wetu. Na wakati ule wakitaka kodi alikuwa ni mtu wa Serikali. Lakini hebu usikie mkuu wa Serikali amekufa. Unaona helicopter inapitisha maiti mpaka analetwa pale. Analetwa na ndege. Kwani yeye si Mkenya kama mimi ama hawa wengine? Na sote tulikuwa tunatoa kodi. Ile kodi hebu kila mtu apate haki yake. Pesa zitengwe kabisa kama zitakaa kwa DC kama zitakaa kwa nani, Mkenya

akifariki tujue ni elfu kumi, elfu tano zitapewa huyo maiti asafirishwe. Ndio wananchi wachangie vizuri.

Lingine ni Katiba ya Kenya. Sijui kama nimekosea lakini namba 56 mpaka 63 katika Katiba ya Kenya kuna lile jambo la kuita mikutano (public meetings). Hawa watu wa IPPG sijui walifanya makosa kinamna gani, ikawa kwamba mtu ana ruhusa ya kukusanya watu. Lakini kukidhaniwa kwamba huu mkutano ati una tofauti ndani, unakatiziwa. Hilo jambo lirekebishwe, mtu akipewa mkutano apewe mkutano. Maana yule polisi ninayezungumza naye wakati ananipa permit ni mtu anasikiza na tayari kama ata-suspect kitu ni pale kwa pale. Sio anipe permit na baadaye aje kuichukua.

Jambo lingine ni vijana. Vijana wetu wa Kenya wamekuwa wasted. Wamesoma kutoka na pesa za wazazi, kutoka darasa la chini mpaka akamaliza hata mwingine amepelekwa University. Lakini Serikali imemuacha, anakaa pale nje. Mzazi wakati alikuwa anaendelea kulea huyu mtoto na kumsomesha, alikuwa anafikiria kwamba atapata msaada mwingine. Lakini leo hii watoto wote wamerudi wamekaa pale manyumbani na hali kuna wazee wamefanya kazi mpaka vipara sasa hawezi chana nywele maana haiko. Nywele imekwisha na bado ako pale.

Mimi ningeomba Katiba ihakikishe kwamba retirement age irudishwe chini. Wafanye kazi kwa muda mfupi halafu waapishe vijana, badala ya kuwaita vijana viongozi wa kesho, wa kesho, wa kesho na hali mtu anakatalia ile nafasi pale. Ikifika ni wakati kazi zimetangazwa utasikia polisi wanaajiriwa Voi, Wundanyi, Kenya Army wapi, watu wale wako na vipara mpaka hapa ndio watoto wao wanapewa kazi tena. Na hao watoto wetu bado tunakaa nao hapa manyumbani. Hili ni jambo la kusikitisha sana kwa sababu hata Kenya inakaribisha uhalifu kwa njia hiyo maana hao watoto wanaanza kuamua kutafuta njia zingine za kujipatia mapato.

Mwisho kabisa ni budget. Kila mwaka tunasikia budget inasomwa. Hii budget inasomewa Wakenya lakini tunasikia sigara ilipanda, sigara ilishuka, sukari ilipanda sijui mahindi. Hebu huyu mkulima mmemuacha hapa mashambani ako reserve. Mbuzi yake mtu anafika wa butcher anaiinua namna hii anasema 'hii haina kilo mama ni shilingi thelathini'. Budget isomwe hata kwa mbuzi zetu, kuku zetu, na ng'ombe zetu hapa manyumbani pia. Tujue tutaiuza vipi ile ng'ombe. Asanteni kwa hayo machache.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana John Mwakugu. John waweza kurudi kwa muda mfupi, commissioner anataka kukuuliza maswali.

**Com. Keriako Tobiko:** Swali moja tu. Ulisema retirement age irudishwe chini mpaka miaka ngapi?

**John Mwakugu:** Retiring age irudishwe kwa miaka ishirini na tano. Mtu afanye kazi kwa, sorry, kwa thirty five years.

**Com. Keriako Tobiko:** Yaani retirement age iwe thirty-five years?

**John Mwakugu:** Yes. After retire, kijana naye aingie pale.

**Com. Kabira:** Asante. Me I should have retired a long time ago. Okey. Bwana Dominic Ndigo.

**Dominic Ndigo:** Mimi jina langu ni Dominic Elisha Ndigo. Tulikuwa tumeketi chini tukaandika machache. Nimetoka hapa Mchanganyiko village. Tulikuwa tumefikiria, tukaulizana, tukauliza juu ya uhuru wetu wa Kenya sisi. Uhuru ni kwa Wakenya wote, Wakenya wanafaaa wawe na vyama vya kisiasa viwili ama zaidi. Kenya yafaa kuwa na Serikali ya mseto; yaani majimbo. Tukaandika hapa muundo wa Serikali, Serikali iwe ya mseto, mwenye kura nyingi awe Rais. Anayefuata kwa wingi wa kura awe Waziri Mkuu.

Uchaguzi wa haki: Uchaguzi mkuu 'General Election'. Wanajeshi, polisi, prisons, administration police, KWS, airforce na navy wasiwe wakipiga kura kwani hawa si watumishi wa chama chochote. Wanatumikia nchi ya Kenya.

Speaker wa Bunge awe anachaguliwa na wabunge wenyewe. Wafanyi kazi wa umma yaani civil servants. Wakenya wote wawe na nafasi za kazi zilizo na usawa kwa mfano vyeo viziwe kwa kabila fulani.

Elimu: Elimu iwe ya lugha tatu: lugha ya mama (mother tongue), Kiswahili, na Kiingereza, yaani English. Shule za msingi zifunzwe na walimu wanaofahamu lugha ya mwananchi wa pale. Shule za upili: walimu wawe wanahitimu chuo kikuu, wapelekwe popote nchini Kenya. Serikali, yaani ghalama zile za shuleni pale. Serikali ighalamie vitabu na vifaa vinginevyo vinavyohitajika kwa elimu.

Hospitals: Matibabu yawe ya bure kama zamani kote nchini. Chifu lazima awe ni wa kabila analotawala. Awe na umri wa miaka kati ya thelathini na arobaini na tatu; yaani wakati anaajiriwa. Chifu awe akipewa uhamisho, yaani transfer, katika location zilizoko katika wilaya yake. Kambi ya Chifu iwe na ulinzi wa kutosha. Awe na ofisi na karani wake na pia kuwe na nyumba ya kuweka wahalifu, yaani, cell. *Mwalugongo (village elder)* awe analipwa na Serikali.

Kuoana (marriage): Kuwe kulingana na mila na desturi za babu zetu. Kila kabila yafaa kusimamia eneo la kwao imara bila kuingiliwa na bari ama kabila zingine. Yaani hapo kama mimi ni Mtaita, basi tuko na eneo la kwetu la Taita, halifai sana bari zingine kutuingilia kwa undani. Maana kama tuko na rasilimali zetu, sizije zikapurwa na watu wengine wakaenda nazo na sisi tuko hapa tu, tunaambiwa hatujui kitu. Kama ni Serikali inaweza kutuelimisha na sisi tukafahamu ni kitu gani kilicho hapa na tukakitumikia. Kwa hivyo hapo ndio nililenga namna hiyo.

Halafu hapa tukaandika hivi yaani ustarabu na elimu (civilization and education). Ustarabu na elimu zienezwe kwa Wakenya wote hasa mavazi .Pawe na mavazi ya heshima kwa Wakenya wote. Maana sasa kama Kenya tungekuwa na mavazi kama vile Uganda, si nchi ya Uganda iko na mavazi yao ya kiheshima? Hata ndugu zetu kama Wahindi wenyewe wana mavazi yao.

Hata kama wanawake wanafaa suruali mrefu, lakini anafaa nguo ingine at least imefika chini kwa magoti. Lakini si kama vile tu Mkenya akifaa suruali, msichana, basi suruali yake inakaa hata amefaa na T-shirt. Vile anatembea hata unarudi kushindwa. Tunapata aibu kwa nchi yetu nzima. Hii sheria ya kujilinganisha tu maana si Mtaita ama nani. Iwe tu mavazi ya Kenya yawe ni ya heshima. Nafikiri yangu yalikuwa hayo machache na nashukuru kwa kunisikiliza. Asanteni sana.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Dominic kwa hayo maoni. Na sasa tutamuuliza Stephen Magadi.

**Stephen Magadi:** Kwa majina naitwa Stephen Magadi na nimetoka area ya Mtiayo. Ningependa kutoa shukrani kubwa kwa siku ya leo kwa sababu tulikuwa tunasikia Yash Pal Ghai kwa redio lakini leo tumemwona hapa ameingia kwetu. Je wananchi mumekubali? Mmemwona Yash Pal Ghai, sio kusikiza katika redio. Ati ooh huyu mtu yuko namna gani? Anatengeneza Katiba namna gani? Huyu ndiye yeye mwenyewe leo mumemwona. Si kweli wananchi? Hata mimi mwenyewe nimeshukuru sana kwa sababu nimemuona. Sijui mumpigie makofi ya kumwalika…..

**Applause from the audience.**

**Com. Zein:** Nadhani mumwelewe vizuri, ndugu yetu anaposema mumemwona Yash Pal Ghai ni kwamba Tume yake imekuja sawa.

**Stephen Magadi:** Hiyo ni sawa. Na ni wao wenyewe amewatuma hawa ndugu zetu waje tukae hapa kikao hiki ili tueleze matatizo yetu na muyafahamu. Wakati mwingine utakao kuja Mungu akitujalia tuone mabadiliko kulingana na vile ambavyo tunatoa haya maoni yetu. La kwanza mimi naweza kurudia rudia tu maanake mengi yameelezwa na wenzangu, na nimeyaunga mkono.

Lakini hapa kwangu mimi nasema watoto wasome bure kutoka class cha kwanza mpaka form four wasome bure, bila malipo. La pili, vijana watafutiwe kazi. Sioni kwa nini Serikali inasema eti kazi hakuna, mimi nashangaa sana, kazi hakuna na Serikali yatangaza kila wakati.

Watoto wetu wanamaliza shule, wameenda mpaka hata vyuo vikuu lakini hawana kazi. Kwani kazi zetu zimeenda wapi sisi Wakenya? Si kazi zetu sisi wanakenya tunazo? Ziko nyingi ila shida moja ambayo tumekuwa nayo sisi Wakenya ni mataifa mbalimbali wamekuja wakachukua nafasi hizi zetu za Wakenya. Tukawa sasa sisi Wakenya tunakosa. Mtu anayetoka nchi zingine ambaye ana ma-grade zake na Mkenya hanayo hiyo grade, hawezi kuandikwa. Hawezi kuandikwa kwa sababu yeye hana zile grades. Lakini anaendea mlango wa nyuma. Anajiweka pande huu, "Bwana wewe umetoka wapi?" "Nimetoka hivi na hivi na hivi." Kwa hivyo hiyo kitu tumesema leo mimi mwenyewe kwa binafsi yangu maoni yangu. Tafadhali watoto watafutiwe kazi wasizidi kukaa hapa nyumbani na kuvuta vuta mabangi, na kulewa pombe za ovyo. Hiyo mimi sioni vizuri.

La tatu ningependelea hospitali ziwe za bure maanake watu wengi sasa wamezidi kupotea kwa sababu ya ugonjwa huu umekuja mbaya wa ukimwi. Na singependelea. Wajua sasa siku hizi watu wengi wakishajua kwamba mtu wake ana ugonjwa, anamficha nyumbani, hatoki. Tukienda kwa madaktari mwananchi anaambiwa 'huyu ana malaria huyu, mwacheni aende. Mwandikie panadol tu.' Anaandikiwa panadol. Wewe huambiwi kwamba unaugua ugonjwa gani, na mimi nikirudi kule naweza kwenda ku-survive maanake sijaambiwa lolote, si mimi niko sawasawa.

Hiyo ndiyo kitu kinafanya sisi Wakenya tuzidi kuingia ndani kwa kupotea kwa sababu ya huu ugonjwa. Ningeomba kamati hii ambayo iko sasa, ambayo inaongozwa na Bwana Yash Pal Ghai achunguze hii maneno ambayo tunapata taabu sana ya wananchi kufa ovyo ovyo. Ukimwi unatumaliza, pombe za kienyeji zinatumaliza kwa hivyo la nne ningependa pombe za kienyeji zirudishwe zile za zamani. Vya zamani.

Hivi hapa tuko na kimoja hapa ng'ambo karibu kabisa, tuko na kingine hapa, kimefungwa. Kingine kiko Kigomo, kimefungwa. Kingine kiko pale Kishamba upande wa Roi kimefungwa. Kwa sababu ya nini? Hatujui. Ati vilabu vinaharibu watu akili. Kwani kweli wewe unaweza kuwa kwa klabu halafu unakwenda unakunywa pombe mpaka unashindwa na akili yako ya kukuongoza nyumba yako? Unaweza kunywa pombe mpaka unashindwa kujiongoza nyumbani kwako?

Saa ile unakwenda kukunywa vile ninavyojua unaweza kwenda kunywa pale kwa bar unakutana na wazee wenzako, mnatoa mawazo, majadiliano iko hivi na hivi bwana. Iko shida nyumbani kwangu. Iko namna bwana, bibi yangu na watoto hatusikizani, kwani nimekuwa namna gani? Nipatie mawazo ni vipi? Napatiwa mawazo pale. Na mimi ninapokwenda nyumbani naweza kujirekebisha. Kama nakunywa pombe sana ni lazima nijirekebishe eti 'kumbe jana nilikunywa vibaya na wenzangu wameniambia hivi na hivi. Nimekunywa mpaka nikalala naambiwa na wenzangu. Hilo pia lafaa lizingatiwe na hii kamati yetu ya marekebisho ya Katiba.

La nne: Mfanyikazi yeyote alipwe pesa zake za uzeeni kwa haraka. Mwezi mmoja akienda, wa pili apate pesa zake za mzee. Sio eti njoo kesho, njoo kesho. Hiyo tabia nimeona sana hapa katika hii Kenya yetu na sijui ni kwa nini inakaa namna hii nimeshindwa.

La tano wazee wa vijiji wako pamoja na Serikali, pamoja na - chifu na naibu wake. Hawa watu ambao wanaitwa wazee wa vijiji ni wazee ambao wana kazi kubwa sana. Jambo lote likipatikana mpaka nimwone mzee wa kijiji. Nikimwona mzee wa kijiji ndiye atanipatia nguvu niende pale kwa mkubwa, maanake siwezi kuenda kwa mkubwa kabla sijaona huyu mdogo. Kwa hivyo walipwe mishahara yao kawaida na wafanyi kazi wote kwa sababu tushawaajili sisi wananchi wa nyumbani. Walipwe mishahara yao kutoka wao mpaka na wale wadogo wa *mwalugongo*. Sioni kama hapo kuna makosa wakilipwa jamani! Sasa Yash Pal Ghai pia atafanya hiyo kazi, ashughulike, aangalie matatizo ya wananchi kama hayo.

La sita: Wizi umezidi hapa Taita. Na sioni ni kwa nini mwizi anaweza kupatikana hapa, anapelekwa kwa chifu au anapelekwa kwa mzee wa mtaa, mzee wa mtaa anakwaambia "Bwana haya maneno wacha nikwandikie barua uende mbele. Pale mimi nina nguvu zaidi nitapeleka kwa mkubwa wangu." Ikifika pale, mtu ameshtakiwa kabisa na yeye mwenyewe kabisa ni huyu huyu amenifanyia hivi. Ukienda pale, ataandikiwa barua, aitwe pale kwa office ya chief, akishatoka pale kwa office ya chief, tutaenda zote kwenda sijui mashtaka lakini kidogo pale sasa wewe mzee mambo yako imekwisha, wacha nizungumze na yeye.

Mambo hayo itakuwa tena mimi niko mbele na yeye yuko nyuma. Sasa tumefanya nini? Ni ufisadi. Kula maneno kama hiyo chakula ya pesa namna hii ya kikombo kombo huku narudi tukutane njiani uniambie "huyu jamaa alikuwa amenipeleka kwa chifu akanishitaki ati nimemwibia, sasa mimi nimetoka, kwani amenifanya nini?" Hiyo hatutaki katika Serikali hii itakayokuja ingine mpya.

Jambo la saba: Janga la ukimwi ndio limekuwa tatizo kwetu zaidi. Lishughulikiwe zaidi na zaidi. Vijana wa siku hizi nimewaona mara nyingi sana. Wako hapa manyumbani, kila kijana, ni msichana ni mvulana anaogopa msichana. Mvulana anaogopa msichana. Haya, msichana naye anaogopa mvulana hata siku hizi inakuwa sasa kila msichana akiona mvulana hivi anapitia kando, anamwekea mgongo. Sio kama vile tulikuwa zamani umwambie kwamba '"Bwana we ..sijui vipi bwana, mimi hivi nilivyo, mimi nataka nikuoe bwana'.

Kwani ukimwambia hivyo kuna nini? Kule kutukanwa hakuna neno. Basi waambiwa "Wewe ni mjinga kabisa." Hutukanwa sisi, "Wewe ni mjinga sana hauna akili wewe, unakuja kuniuliza, angalia sura yako, sura yako ni kama ya nyani ama kama ya mbwa." Sasa wewe ukisharudi pale moyoni mwako unaona hivi "Huyu msichana amenitukana namna hii, wacha akae." Anaringa. Wapi? Humbembelezwa pole pole tu, pole pole. Kama janga hili la ukimwi limekuja na hili janga ni libaya sana jameni. Yatakikana kila mtu awe ana mwenzake wasaidiane maisha. Kwa hivyo nilikuwa naomba hilo janga limalizwe.

**Com. Kabira:** Hebu tafadhali tumsikize.

**Stephen Magadi:** Asante sana. Kwa hivyo yangu ni hayo tu sina mengi zaidi. Asante sana.

**Com. Kabira:** Kwa hivyo unasema tufanye nini mambo ya wasichana na vijana. What is your recommendation?

**Stephen Magadi:** Mambo ya vijana. Mambo ya?

**Com. Kabira:** Mambo ya wavulana na wasichana.

**Stephen Magadi:** Mambo ya wavulana na wasichana wasikae hivi hivi bila kuoana. Nimeongea mambo ya wasichana kwa sababu siku hizi janga la ukimwi limekuja. Watafute polepole, polepole.

**Com. Kabira:** Tafadhali tusikie vile anasema. Sorry tafadhalini mupatie wakati.

**Stephen Magadi:** Hili janga la ukimwi limekuja, kijana asiogope msichana na msichana asiogope mvulana.

**Com. Prof.Wanjiku Kabira:** Wafanye nini?

**Stephen Magadi:** Kwa sababu wameogopa hili janga la ukimwi. Wameogopa.

**Com. Kabira:** Wameogopa?

**Stephen Magadi:** Wanaogopana.

**Com. Kabira:** Si wanaogopa kwa sababu ya ukimwi?

**Stephen Magadi:** Kwa sababu ya ukimwi.

**Com. Kabira:** Kwa hivyo unataka wafanye nini?

**Stephen Magadi:** Nilikuwa naomba Serikali pia izingatie madawa ya kienyeji ipewe uhuru. Kila mtu apate dawa apelekwe kwa hospitali.

**Com. Prof. Wanjiku Kabira:** Asante sana.

**Applause from the audience.**

**Stephen Magadi:** Nashukuru, yangu ni hayo tu.

**Com. Kabira:** Asante, andika jina lako kwa huyo msichana. Asante sana. Bethuel Mwasalu. Ngonjea kidogo Mwasalu, tupatie dakika moja tu kuna mtu anataka ku-clarify. Si ndiyo?

**Dominic Ndigo:** Mtaniwia radhi ile retirement age nilikuwa nimezungumzia nilikuwa nimetaja miaka ishirini na tano. I meant working period. Ndio nilikuwa nimetaja lakini haki ni mtu a-retire na forty years. Poleni. Thank you.

**Com. Kabira:** Sasa tutamusikiliza Bethuel Mwasalu.

**Bethuel Mwasalu:** Asante sana ma-commissioners wetu kutoka Tume ya Ghai. Wananchi wote nawasalimia, hamjambo. Mengi yamezungumzwa zungumzwa lakini nitaongezea mahali fulani. Kwanza ningeanza na pointi hii ya mwenyekiti wa baraza. Katika Katiba ijayo naomba mwenyekiti wa baraza achaguliwe na wananchi wote wa sehemu ile. Na pia awe na nguvu za kusimamia ama apewe mamlaka ya kusimamia mikutano ya DDC badala ya mfumo ule ulioko kwa sasa, DC ndiye anayekuwa mwenyekiti wa DDC na hali members wanakuwa ni wale Head Of Departments ambao mara nyingi huwa ni watu wa sehemu ya nje ya baraza lile. Ama ya wilaya hiyo. Sasa mambo huwa yanafanywa na watu kutoka nje na hata kama ni kupendekeza miradi huwa inapendekezwa na watu kutoka nje. Ambayo hiyo inaonyesha wazi kwamba si haki maana hao watu labda hawajui hiyo area vile ilivyo. Lakini wao hupendekeza tu halafu sehemu zingine zinabaki nyuma.

Ya pili ni sheria ambayo inayosimamia kwamba mwananchi wa Kenya aishi pahali popote nchini Kenya. Sheria hii ningeomba ifanyiwe marekebisho. Mwananchi aruhusiwe kuishi lakini asiwe na mamlaka ya kuchaguliwa nyadhifa kama vile ubunge, ama udiwani. Kwa sababu mara nyingi hii imechangia wale watu ambao ni wachache kama Wataita hivi. Watu wakija kutoka sehemu za nje, waje labda watu mia tatu, na sisi Wataita huwa tunawakaribisha. Wakija mia tatu na labda wale watu wa area ile ni watu mia moja, basi kama ni sehemu ya diwani huyu diwani ametupwa nje. Tutakuwa na mtu ambaye ametoka nje labda Mkamba, Mjaluo, ndiye atakuwa diwani na utamsikia labda ni wa Ron'ge. Kwa hivyo tungeomba hao watu wasipewe mamlaka ya kuchaguliwa katika nyadhifa hizo.

Sheria inayo simamia mbuga za wanyama igeuzwe badala ya kuitwa National Parks iitwe Game Reserves. Maanake hili jina National Parks mara nyingi imechangia mwananchi yule ambaye yuko karibu na hawa wanyama asifaidi chochote. Mali ikichukuliwa inapelekwa Central Government, mali ikichukuliwa yapelekwe Central Government. Kwa hivyo hili jina National Park katika Katiba ijayo liondolewe kabisa. Iwe ni Game Reserve.

Karibu na mwisho. Mambo ya elimu: Elimu iwe ya bure, kwanzia nursery school mpaka kidato cha nne. Na iwe ni ya lazima. Mtoto yeyote wa Kenya lazima asome na asome bure. Halafu mwisho mwisho huu mpango wa ulazaji wa mashamba unaoitwa consolidation. Katika Katiba ijayo ama ambayo tunaiunda sasa, tungesema kwamba mpango huu uondolewe kabisa. Kusiwe huu mpango wa consolidation. Uwe ni ile mipango mingine ya ulazaji. Kwa sababu mpango huu umeumiza.

Kama area yangu, Kenya tangu 1969 ndio huo mpango ulianza hapa. Mpaka sasa haya mashamba hayajalazwa, wananchi bado ni squatter. Sasa na wakati uhuru ulikuwa unapiganiwa, ulikuwa unapiganiwa kwamba kila mwananchi asiwe squatter katika nchi yake. Sasa hawa watu watakuwa squatter kwa miaka mingapi? Tungeomba mpango huu uondolewe na wananchi wapewe mashamba yao vile yalivyo kama hizi sehemu zingine ambazo zimebakia maana labda katika Kenya ni hapa tu kumebakia. Hiyo sehemu yangu labda ya Rong'e juu na hapo sehemu kidogo. Kwa hivyo huu mpango uondolewe.

Mwisho kabisa, ningeomba Katiba hii ijayo iwe ya majimbo. Mungu alikuwa na mpango mzuri, akaumba Mtaita na utaitani

kwao, Kikuyu na Kikuyuni kwao, Mjaluo na ujaluoni kwao. Kwa hivyo hata sasa tuheshimu mambo ambayo Mungu aliweza kuyapanga sisi tusije tukayakosoa. Asanteni.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Bethuel. Na sasa tutamuuliza Oliver Mwadembo.

**Oliver Mwandembo:** Bwana Chairman na ma-commissioners na wananchi hamjambo. Kwa majina yangu naitwa Oliver Mwadembo kutoka hapa Mwabota na mimi yangu sina mengi ya kusema kwa maana mengi yametajwa. Nikigusia kwa mfano: Mambo ya majimbo nayaunga mkono. Majimbo nayaunga mkono. Sheria ipitishwe kwamba katika kila mkoa ama kila wilaya basi watu wajisimamie wenyewe. Hivo kwamba watu wakijisimamia wenyewe, ni na uhakika kwamba watakuwa na uwezo wa kusimamia rasilimali zao kibinafsi.

Jambo lingine ambalo nimesema limetajwa na limezungumzwa ni mambo haya kama kwa mfano: National Parks ibadirishwe na badala yake iwekwe Game Reserve. Hapa Taita, Tsavo National Park ndio kubwa kuliko zingine na kwa hakika National Parks zikigeuzwa na ziwe game reserves nina uhakika kwamba Wataita tutafaidika. Mambo yamesemwa hapa kama mfano michango ambayo tunahitaji katika maendeleo ya sehemu yetu. Kwa kweli tukiwa na kitu kama hicho ni manufaa kwetu na tunaweza tukafaidika ikiwa kama National Park itageuzwa kuwa Game Reserve.

Halafu mhusika mwingine ameongea juu ya boreholes kwa kuondoa umaskini. Naunga mkono katika sehemu hizi kama mahali ambapo mpo kwa kweli Serikali ingefaa ifikirie jambo hilo la kuondoa umaskini hasa sehemu hizi kame. Sehemu za nyanda za chini hizi. Kwa hivyo boreholes zikiweko tutapunguza umaskini.

Jambo lingine ambalo pengine kwa binafsi ningelitaja ni juu ya ulemavu ambapo kwa kweli ingepaswa wapewe haki zao. Haki zao ni zipi? Za kielimu na mambo kama hayo. Yaani ningetoa mfano huu: Sheria iweko, mtoto yoyote aliyelemaa asifichwe manyumbani na yeyote ambaye atapatikana na kutomtoa mtoto yule katika kwa mfano kuchanganyikana na wenzake, ama kumhusisha katika elimu ili apate elimu, basi sheria hii iwe kali ili kwamba ambaye anayehushika ashitakiwe. Maanake wananchi mnaweza kubaliana na mimi nikisema kwamba kuna walemavu wengine, kwa mfano, unaweza kuona mtu amelemaa miguu ama hasikii lakini umemnyima elimu. Lakini ile elimu ukimpatia mtoto yule ana taranta yake ambaye amezaliwa na Mwenyezi Mungu. Mtoto yule si ajabu siku za baadaye atakuwa ni kiongozi. Na akiwa kiongozi atasaidia wananchi kwa jumla na zaidi ya hapo kijamii. Kwa hivyo tafadhalini sheria hiyo iwekwe.

Jambo lingine ambalo ningelitaka pengine sheria itakapoudwa, wakati huu ambao tunao utaona kwamba ati kwa upande wangu ningeonelea kuwe mtu mmoja kazi moja. One man one job. Tunasema, tunalilia ya kwamba, tunalia kila wakati eti hakuna kazi. Na hali kwamba utaona mtu mmoja amesimamia majukumu hata karibu sita. Mmoja utasikia ni chairman wa board fulani, mtu huyo huyo utasikia ni director wa board fulani, mtu huyo huyo utasikia ni mbunge maalum na mambo kama hayo. Kwa hivyo tafadhalini, sheria iwekwe, one man one job.

Tuingilie wafanyi kazi wa Serikali na waalimu. Mishahara ya mtumishi wa umma na mwalimu iwe ikichunguzwa mara kwa mara. Hawa wafanyi kazi ni watu wa kiwango cha chini na tumeona kwamba mara kwa mara utasikia Serikali hasa zaidi inawakumbuka wale wenye vyeo vya juu kabisa. Unasikia mtu ni Permanent Secretary, mtu huyo mshahara wake ukilimnganisha na yule mfanyi kazi wa kawaida kwa kweli ni jambo la kusikitisha, na msiba mkubwa.

Maana Permanent Secretary ama chairman ama director wa body fulani unasikia mshahara nusu milioni. Haya nusu milioni. Mfanyi kazi wa kawaida naye, mshahara wa chini kabisa ni shilingi elfu tano. Sasa shilingi elfu tano kwa kweli ulinganishe na shilingi nusu milioni. Ni haki hiyo? Basi jambo hilo lichunguzwe, mishahara ya watu wa kima cha chini tafadhali ipandishwe. Sijui kama mmenipata? Nasema hivi, mishahara ya wafanyi kazi wa kiwango cha chini kwa utumishi wa Serikali na walimu ipandishwe. Isiwe vile ilivyo sasa. Hilo ni pendekezo.

Jambo lingine pengine nakaribia kumalizia, kuna speaker ambaye amezungumzia jambo la utungaji mimba. Pengine msichana ametungwa mimba. Jambo hili tafadhali nikilisizitizia zaidi lifuatwe zaidi. Yeyote ambaye atapatikana na kosa kama hilo atafutwe, afanyiwe kikao, ahakikishwe kuwa ni kweli alihusika? Na kama alihusika basi asimamie ghalama za malezi hadi yule mtoto atakapo maliza shule. Hapo hapo ningeongea juu ya ubakaji. Hawa rapists wenye kuwashika wasichana kwa nguvu, sheria tafadhali, sheria za Kenya zimelegea kwa upande huo na sijui zimeregezwa kwa njia gani. Pengine ni ufisadi tu kama vile ulivyotajwa hapo mbeleni. Ningependelea yoyote ambaye atakayepatikana na kumkaba mtoto wa kike, hasa mtoto mchanga mwenye chini wa miaka kumi na minane, huyo ni mtoto huyo, tafadhali sheria iwe kali zaidi kuliko ya sasa. Nafikiri wakina mama wataniunga mkono. Na wazee vile vile.

La mwisho kabisa ni jambo la ardhi, yaani, hasa zaidi title deeds. Wataita na Mkoa wa Pwani kwa jumla kwa kweli tumekuwa tuko kwetu, tumezaliwa humu humu. Lakini tuko ni kama ma-squatter. Kwa hivyo ningependekeza sheria iwekwe mtu yeyote ambaye yuko mahali anapoishi, basi kutengwe siku fulani, yaani, siku kadha ama miezi kadha isipite zaidi ya miezi mitatu, mtu yule pasipo kupatiwa title deed. Title deed iwe ni lazima kwa yeyote ambaye anamoishi pale asiishi pahali pake kwa zaidi ya miezi mitatu. Yaani ni sharti kila Mkenya mahali popote anapoishi awe na title deed. Maana mnajua title deed kama alivyosema hapa ni muhimu zaidi kwa maendeleo ya mtu binafsi. Kwa hivyo yangu ni hayo. Karibuni hapa kwetu tena.

**Com. Kabira:** Asante sana lakini nina swali kidogo nataka kukuuliza. Kuhusu haya mambo ya wale wanapatia wasichana mimba umesema wachukuliwe hatua, ninauliza kama wanaenda, si wanarudi shuleni? Wakipata watoto.

**Oliver Mwandembo:** Wengine hukataliwa.

**Com. Kabira:** Wanakataliwa na nani?

**Oliver Mwandembo:** Yaani kwa mfano amepata mimba sivyo? Nilisema hivi afanyiwe kesi halafu apatikane na hatia kama ni kweli alihusika, basi ingekuwa vizuri kama yule mtoto alikuwa anaenda shule, akubaliwe nafasi ya kuendelea na masomo. Lakini ulezi ule wa mwana basi ukabidhiwe yule ambaye alitenda jambo hilo.

**Com. Kabira:** Asante sana. Tutamuuliza Samuel Mutito.

**Samuel Mutito:** Asante sana kwa Tume hii, mwenyekiti wake na wale wote wanahusika ma-commissioners. Kupata nafasi kama hii kwangu ni furaha kwa sababu ni kama bahati tu. Ajabu ni kwamba Katiba hii ambayo tunataka iundwe upya imechelewa sana kwa sababu tangu tunyakue uhuru mpaka hivi sasa ndio ingefanyiwa kama vile inavyofanya hivi leo. Mambo nafikiri yangekuwa barabara. Hayangeharibika jinsi yalivyo haribika hivi sasa. Kwa sababu kutokana na hali hii ya wananchi kutojua Katiba yao.

Tunasikia Katiba iko, iliundwa huko Lancaster na wananchi hawaifahamu sawasawa. Mpaka kufikia wakati huu, Katiba nyingi zimeundwa lakini wananchi hawazijui. Lakini hii ya leo, mwananchi anahusika kabisa kwa sababu anaweza kutoa maoni yake na yakawekwa katika hiyo Katiba. Hii ndiyo nafasi ya muhimu sana kwa mwananchi kuipata maanake ni nadra sana. Tumeipata kwa bahati tu. Na ingekuwa hizi Katiba zote mwananchi angepatiwa nafasi kama hii ya leo, nafikiri Kenya yetu haingepata hasara ambayo imetufanya sasa kuwa ni watu maskini kabisa.

Maendeleo imerudi nyuma na mambo yameharibika kabisa. Hata sheria hazijulikani kama ni sheria. Ziko pale kama karatasi tu ndio inajulikana kwenye karatasi kuna sheria fulani. Lakini haifanyi kazi sawasawa. Sasa mengi yameongewa na hata kuyarudiarudia ni kama kupoteza muda. Mimi nitaanza na sehemu ya walemavu.

**Com. Kabira:** Lakini ni vizuri utaje tu kwa sababu ya record.

**Samuel Mutito:** Kama nikutaja nitasema kwamba wilaya zipewe uwezo wa kujisimamia zenyewe. Kwa sababu wilaya zikipatiwa nafasi ya kujisimamia wenyewe kwa mambo yao basi kila wilaya, itajua ni shida gani zilizo katika wilaya hiyo. Kwa sababu kama wilaya hii yetu ya Taita, yote yamezungumzwa kuhusu mbuga za wanyama na mambo mengi. Kwa hakika sehemu kubwa ya Taita imechukuliwa na mbuga za wanyama. Na Mtaita yuko kwenye milima milima tu, ati ndio anaita mashamba. Na sehemu ile nzuri imekaliwa na wanyama. Na wote wanahesabiwa ni Wakenya. Faida yote inayopatikana kutokana na wanyama wale inaenda katika Serikali kuu. Mwananchi hapa anabaki ni hivi hivi tu. Kwa hivyo ningeonelea kwamba mambo yasimamiwe na wilaya kusudi mambo yaende sawasawa.

Kwa upande mwingine mambo ya walemavu yameongewa lakini shida moja ni kwamba mwananchi wa Kenya hajafunzwa mambo ya mlemavu sawasawa. Mambo ya kuhusu mlemavu haijafundishwa Wakenya sawasawa. Utaona mlemavu anahesabiwa kama kitu. Kama mimi nisiona hivi, utaona nahesabiwa kama chombo. Hata naweza kuwa napita kwenye njia

labda hata watu wanaangalia tu 'huyu anaenda atapita pale sawasawa'. Inakuwa kama sasa kitu cha kuangaliwa kinakwenda namna gani. Maanake ni mlemavu hachukuliwi kama ni mtu aliye na faida pale. Badala ya kuonyeshwa sawasawa, atawachiliwa tu na watu wanaangalia kama vile wanavyoangalia sinema huyu anaenda vipi. Atapanda pale lile korongo atalipita sawasawa ama ataanguka. Kwa hivyo mwananchi hajaelimishwa sawasawa elimu hii ya mlemavu.

Tumezungumza mlemavu, mlemavu lakini bado haijaandikishwa. Na tungetaka elimu hii itolewe kwa Wakenya wote wajue mlemavu naye ni mtu sawasawa na mwananchi mwingine. Shida tu ni ile shida ya viungo kama ni macho ama sikio au kutoongea vizuri au kutotembea sawasawa. Ndio hapo iko shida lakini akili ziko sawasawa na za watu wengine. Kwa sababu akipatiwa nafasi anaendelea vizuri kawaida na wale watu wengine. Nafasi ndio walemavu hawapatiwi sawasawa. Nimeona mimi nilikuwa katika vyuo vya walemavu na kwa hakika siku hizi tangu uchumi umekwenda chini, vyuo vya walemavu vimeharibika kabisa, kwa mfano tuna kimoja hapa 'Bura rehabilatation' ambacho ni chuo cha walemavu wa mkoa mzima. Lakini ukikiangalia sasa jinsi kilivyo, kinashangaza. Kweli ni cha Pwani nzima hii, Pwani nzima inasimamia chuo hiki na kiwe katika hali ile. Si mlemavu ananyanyaswa tu, kwamba anasaidiwa na kumbe bado anataandikiwa kitanda cha ulemavu aendelee kulemaa zaidi.

Kwa hivyo mambo ya walemavu katika Katiba inayokuja, yasimamiwe na walemavu wenyewe kwa sababu kunguni anaomuuma mlemavu, anayemjua huyo kunguni ni mlemavu mwenyewe. Kwa hivyo mambo ya walemavu yasimamiwe na walemavu wenyewe na zaidi ya hivyo hata katika uchaguzi unaokuja, tungetaka walemavu wapewe waziri wao ili kwamba waziri yule asimamie mambo ya walemavu kabisa. Kama ni misaada inayohusu walemavu itolewe kwa vizuri. Sijui hapa tumechanga michango ya walemavu , ma milioni kadhaa, lakini sasa sijui kama yanafanya kazi gani. Kama kweli yalikuwa ni ya walemavu, mbona vyuo vya walemavu vinakufa? Haziendelei. Hizo pesa zingefanya kazi za kuziinua vile vyuo vilivyokufa ili ziendeshwe na walemavu wazidi kupata misaada kwa elimu si cha rehabilitation peke yake.

Kuna vyuo vingi vinavyohudumia walemavu. Kwa hivyo pesa hizo zinatumiwa vibaya. Hazisimamiwi, na zingesimamiwa na walemavu wenyewe labda wangezigawanya vizuri wakisaidiana na wale wengine. Si semi ati walemavu wakifanya hivyo wafanyi kazi hawatusilikisha. Lakini tupewe nafasi ya kujisimamia mambo yetu. Kwa sababu hata sisi tulio hapa vijijini, hata hiyo misaada hatuioni. Hatuioni hiyo misaada inayosaidia walemavu. Vijijini hatuioni. Sijui kama kuna walemavu yeyote hapa anaweza kusema nasema uwongo. Kama kuna mlemavu aseme kama ninasema uwongo hapa. Kuna misaada kweli inawafikia walemavu ya kuwasaidia kweli ya kuwaendesha? Sioni, mimi sioni hata sijaipata lakini mamilioni yako, yaliyochangwa, yamechangwa kwa sababu gani? Ya kusaidia walemavu kujiendeleza. Kwa hivyo Katiba isaidie kusimamia mambo hayo ili walemavu wanaokuja na walioko waweze kujimudu katika hali zao. Kwa hivyo sitasema mengi kwa sababu kuna wengi wanaotaka kuzungumza na ningeshukuru sana kwa nafasi hii ambayo mumenipatia.

Kuna lingine limekuja katika moyo. Unajua shule zetu hizi, vile tunasema sijui namna gani. Nidhamu zimeharibika, tunasikia mambo yameharibika huku na kule, unajua sababu gani? Zamani shule nyingi zilikuwa zinasimamiwa ni mission na neno la Mungu lilikuwa linapenyezwa kwa wingi sana. Na kanisa linalosimamia kama shule hii ya Mwakinyungu ilikuwa inasimamiwa na

kanisa la Anglican basi nidhamu inaelekezwa, inashindiliwa kwa neno la Mungu ili watoto wazidi kuwa na tabia nzuri. Lakini siku hizi ni mtoto na masomo tu.

Hata kama mwalimu atafanya kurekebisha rekebisha lakini tabia hasa kuinyosha kabisa. Unajua roho ya mwanadamu hunyoshwa na neno la Mungu. Awe ni muislamu atanyoshwa na neno la Mungu. Kwa hivyo nafikiri kama shule zingesimamiwa na dhehebu zilizohusika nafikiri nidhamu ingekuwa sawa. Pia vijijini, nidhamu zimeharibika kwa sababu zile Katiba zilikuwa zikisimamia hali ya mwananchi, hazisimamiwi sasa. Wazee walikuwa na jukumu kabisa mtoto wangu ni sawasawa na mtoto mwingine. Mtoto yote ni mtoto wangu kama mimi ni baba. Huu ndio ulikuwa utamaduni wa mwafrika.

Siku hizi tunazungumza utamaduni utamaduni lakini utamaduni kama umekwisha, umekwisha kazi wa mwafrika haufanyi kazi. Kwa sababu siwezi kumkuta mtoto wa mwingine pale nikamwambia umekosea, unamwambia kama nani? Lakini zamani sivyo. Nikimwona mtoto wa ndugu yangu amekosea, nina haki ya kumwaadhibu ama kumsahihisha kwa sababu akiharibika ni taifa linaharibika. Lakini siku hizi si hivyo. Ndio sababu taifa la Kenya siku hizi limeharibika kwa sababu nidhamu ile ya zamani haifuatwi ama sheria za zamani hazifwatwi utamaduni.

Kwa hivyo utamaduni, tunapozungumza utamaduni, Katiba hii izingatie utamaduni ni utamaduni wa namna gani tunaozungumzia kwa sababu tunataka kufanya kazi ili mwananchi wa Kenya aendelee kuwa na nidhamu ya hali ya juu. Mitindo ya kigeni imeharibu nchi yetu zaidi.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Mutito kwa hiyo maoni yako. Na sasa tutamuuliza Joseph Mwachoni. Joseph Mwachoni ako? Hayuko. Kwa hivyo tutamuuliza…..okey utazungumza. Umesema laini moja?

**Joseph Mwachoni:** Okey asanteni sana jina langu ni Joseph Mwachoni, mimi ningependekeza swala la hasa…..nachangia juu ya umaskini na katika moyo wangu ningeonelea ni vyema kwamba kuwe na sheria ambayo inaweza kuipa jukumu kama ni Council ama ni DDC. Iwe na uwezo wa kujua kwamba zile pesa zote ziko generated katika district ile zinabaki pale kwa kuweza kuendeleza sehemu ile. Kwa sababu kama tulivyosikia, pesa zinazotoka kama ni Barclays zinaenda mahali fulani na mambo kama hayo. Sasa sheria hiyo inaweza kuwasaidia wale watu ambao wanaishi katika eneo hilo kuona kwamba wanaweza kufanya mradi gani.

Hapa nilipokuwa nikifikiria nilikuwa nikifikiria juu ya mito. Sisi tunaishi area ya ASL (Arid, Semi-Arid land) na kuna mto na sasa huu mto tunaweza kufunga dams ambazo zinaweza kutusaidia kwa irrigation na zinazotusaidia kama kufuga samaki. Mahali kama ni maji mengi inaweza kusaidia ku-generate electricity. Hata kama kuna sheria ambayo yaweza pitishwa iwe kwamba kila sehemu kuna mto kama huo. Ni seasonal river lakini iwe yale maji yametengwa kusaidia wale watu wa sehemu hiyo.

**Com. Kabira:** Asante. Joseph musaidie…….

**Samuel Mutito:** Kuna kitu ambacho nimesahau. Tunaona maandishi haya ni ya watu walio poor sighted, siwezi kusoma kilichoandikwa hapa. Kwa hivyo Katiba hii tunayotaka iandikwe tunataka ichapishwe katika vitabu kama the braille ambavyo vinaweza kueleweka na mlemavu kama Mutito hivi ambaye haoni. Hata vile ikiandikwa katika lugha za wale watu wanaohusika na mambo ya bubu, iandikwe hata bubu ajue kwamba Katiba ya Kenya inasema nini? Iandikwe katika lugha zao kwa maandishi yao. Kila mtu ajisomee bila kudanganywa. Hivyo ndivyo nilikuwa ningetaka kusisitiza.

**Com. Kabira:** Okey Asante sana Bwana Mutito. Margaret Munga, Margaret ako? Ako hapo? Ninauliza kwa nini akina mama hamzungumzi. Hayuko? Nitamwita mwingine Dorcas Fikina. Dorcas ako? Wako nje. Na Luciana Mwairuwa. Luciana ako? Hayuko? Angelina Mwakodi.

**Angelina Mwakodi:** Wageni wetu wa Katiba pamoja na wananchi, mimi langu ningelitaka nizungumze juu ya *manamba*. Tangu tulipokuwa watoto sisi tulikuwa tunajua conductor na driver na turn boy. Hii kitu inaitwa *manamba* hatujui imetoka wapi. Inatuumiza sisi watu wa biashara. Tunaomba ikiwezekana turudishiwe conductor, driver na turn boy. Kwa sababu hiyo kitu naona wao *manamba* wanatunyanyasa hizo pesa wanazipata ni za dhuluma kwa sababu hawatufanyii kazi, wanazipata za bure bure. Mimi mwenye biashara ninaumia na hata mwenye gari anaumia kwa sababu *manamba* wanaomba pesa nyingi kuiingiza lile gari kulijaza. Na mwenye gari naye anaumia analipa driver, analipa conductor, analipa county council kile kiwanja na tena *manamba* anawalipa.

Kwa hivyo mimi naona watu wa biashara kama hawa watu wa magari pamoja na sisi abiria ambao tunaenda kununua vitu vyetu vya biashara tunaumia. Irudishwe kama zamani kwa sababu zamani elimu ilikuwa kidogo na watu walikuwa wakisafiri na walikuwa wakijua hili gari litanipeleka mpaka linifikishe mahali ninaenda. Siku hizi watu wamesoma na ninajua kibao kikiandikwa nitajua hiki kibao ni cha Msau, ni cha Mombasa na kadhalika. Lakini tumeletewa watu wengine wanaitwa *manamba* ambao hunyanyasa watu na kuchukua pesa za bure. Kitu hiyo mimi inaniuma sana hata nimefurahi sana kupata siku ya leo na kuongea kitu hicho.

La pili ni kazi. Tunaambiwa kazi hakuna hapa Kenya. Kwa sababu ya ufisadi. Kama kwa mfano kama kuandika watu kama kufanya ile census na hizi kura zinakuja. Unaona mwalimu ameandikwa ama daktari ndiye yule yule anapatiwa kazi ile na kuna watoto wamesoma, wako na ma-certificates kama wale walimu ambao wamesoma. Unaona mwalimu ndiye anarundikiwa pesa hizo na kuna mwingine anashindwa hata na kulea watoto wake na bibi yake.

Kuna wengine wanashindwa hata na kusomesha watoto wao. Hata kuna vijana wetu wanakosa kazi lakini tunaona mmoja anarundikiwa kazi mbili, anazifanya na anataka pesa kila mwezi na tena anapatiwa hiyo ya contract afanye. Kwa nini hiyo isipatiwe yule ambaye hana. Kwa Kenya yetu tunahimiza mtu akiwa na kazi haruhusiwi kupatiwa ile kazi inakuja ya contract.

Na lingine ninasema ni kuhusu traffic wetu. Hawa traffic wetu wamekuwa wanapatiwa kile kitu kidogo na wao ndio wanasababisha kule barabarani kuwe na ajali nyingi. Unaona gari imejaa hata imezidi ile balance na unaona mtu anapatiwa kitu kidogo, hiyo gari anairuhusu inaenda. Na baadaye muda kidogo unasikia imepinduka. Tunaomba kama sheria yetu ya Kenya wananchi kwa sababu ndio wanabebwa, na ndio wao wanatoa pesa zao kusafiri, wakiona kama traffic huyo anapatiwa pesa, wana haki ya kumshtaki pamoja na yule driver.

Na lingine ni la kuhusu wanawake wale ambao wanazalisha (wakunga). Wakunga wamepatiwa elimu na Serikali lakini hawajapatiwa zile certificates za kujulikana kwamba wao wana ujuzi. Wanapopeleka wagonjwa pale Voi, hata hawawezi kuhudumiwa kisawa na yule daktari mwingine. Tukipatiwa zile certificates, nikienda hata kama ni Voi nitajulikana. Tunawaomba Serikali iwe ikiwaangalia kwa kuwapatia vifaa. Na kuwapatia hizo certificates ili nikipeleka mgonjwa aende ashughulikiwe kama mimi mkunga nimempeleka. Asiwachwe hivi hivi kwa sababu pale sina certificates wala sina kitu chochote cha kujijulisha mimi ni mkunga basi mgonjwa wangu hawezi kuhudumiwa vilivyo. Nafikiri ni hayo.

**Clapping from the audience.**

**Com. Kabira:** Asante sana Bi. Rose na ulikuwa umeandika ambayo hutaki kuzungumza? Kuna ingine?

**Angelina Mwakodi:** Lingine ni la kuhusu hii pombe ya kienyeji. Sisi akina mama ni sisi tuliitwa kwa mkutano na tukasema pombe ziondolewe lakini umefikia wakati tuseme zirudishwe. Kwa sababu wavulana wetu wameelewa hata wengine wamesoma wana elimu kubwa lakini kwa wakati huu hawajijui hata mzazi ameanza kuona afadhali singefundisha mtoto huyu. Anaona hiyo mali yake imepotea kwa sababu wengine wamekuwa akili zimeruka, wanakula madawa ya kulevya wakichanganya na hiyo pombe. Kwa maoni yangu nasema hivi: Sisi Wakenya tuko kama ma-squatter kwa sababu tuliondoa pombe ya kienyeji tukakaribisha zile pombe za kigeni.

Huyo mgeni anapata pesa na zile zetu za kienyeji tumeziondoa. Ningeliomba kama ni vilabu virudishwe, watu wawe wakinywa kwa masaa kama ni saa kumi. Viruhusiwe kufunguliwa saa kumi ili vijana wetu watakuwa na uoga wa kwenda pale kwa club. Kwa sababu zimekuwa ni za mtaani. Hata unamwona mtu mwingine ana nyumba yake, anamka saa kumi na mbili hata hanywi chai, anaenda kwa huo mgangala, anashinda hapoooo.

**(clapping from the audience).**

Hata wengine wanasema ati 'bibi ya fulani amepata mtoto amefika hivi ati kwa sababu anatumia family planning' hakuna family planning. Family planning inafanywa na bwana kwa sababu akija, anakuja kama ni asubuhi hakuna kazi inaendelea.

**(Clapping from the audience).**

Kwa hivyo mpangala umefanya wanaume wengi wameisha kabisa hata wana kazi manyumbani. Na huo mpangala unachangia hata vijana wetu kupata huu ukimwi. Ukimwi unatokana pengine na mpangala. Ule mpangala kwa sababu kijana anatoka kule kutoka asubuhi anashinda hapooo sasa hata akikutana na yule msichana njiani hajijui, hajui yule msichana ana ukimwi, wanaendelea na kazi kumbe vile amepatwa na viini. Kwa hivyo tunaomba huo mpangala uondolewe na ufanywe vilabu kama kawaida.

Hata kama Yesu ametuokoa, lakini imefikia wakati tuseme mpangala urudishwe wa vilabu lakini wa masaa. Sio ule wa free kuanzia saa kumi na mbili mtu anakunywa chai hata saa ingine anafanya sisi wanawake tunalaumiwa hatulishi wanaume chakula, hatuwafulii nguo. Sasa utamfulia lini akiwa anashinda hapo kutoka saa kumi na mbili, anashinda hapo, chakula hali, sasa anakaa kama mtu ambaye ukimwi na ni kwa sababu hali. Hali chakula kabisa na bibi anampikia chakula kinashinda hapo hapo kikingojea mtu, hakuna mtu anakuja kula chakula. Chakula yake ni hiyo pombe tu.

Kwa hivyo tunaomba Serikali yetu ingawaje sisi akina mama tulitoa ruhusa hiyo pombe iondolewe, tumesema irudishwe na iwe na viwango vya umri wa kunywa hiyo pombe. Kama ni mtoto aanze kama ni miaka kumi na nane kuendelea lakini sio mtoto wa kuanzia miaka saba, miaka mitano anakunywa hiyo pombe.

Na lingine Kenya yetu mimi nakumbuka wakati nilikuwa nikisoma shuleni, hata ilikuwa ni hapa hapa Mwakinyungu. Tulikuwa na wimbo wa Kenya nzima ulikuwa unaimba kwamba nguo fupi ziondolewe katika Kenya hii. Na wimbo huo tuliuimba wakati wa Hayati Mzee Jomo Kenyatta. Mbona siku ya leo tumeona zile nguo zimerudishwa. Tabia ya kuiga Wazungu wale wanakuja ma-beach. Tunasema hizo nguo zinatutoa aibu sisi Wakenya. Mambo ya kuiga Wazungu sisi akina mama tunasema huo mtindo uondolewe. Unaona msichana amevaa nguo lakini ukirusha kalamu pale chini, hawezi kuiokota, sasa mimi mama ndiye ninaona aibu. Tunasema hizo nguo za mini-skirts ziondolewe katika Kenya hii. Yangu ni hayo.

**Clapping from the audience.**

**Com. Kabira:** Asante sana Mama Angelina. Rose Wali ako? Hayuko? Pauline Nzeru? Hayuko? Purity Mbui? Nitauliza tukiendelea na haya mambo, akina mama wale wanataka kuzungumza wajiandikishe majina kwa sababu hakuna wengi wamezungumza na munaona wana mambo mengi wangetuambia. Si ndiyo? So we will talk to Jason Sako. Ako? Hayuko? Esther Mwang'ombe?

**Esther Mwang'ombe:** Ma-commissioners wetu, mabibi na mabwana mimi ni Bi. Esther Mwang'ombe. Jambo la kwanza ningesema ni juu ya sheria. Hukumu itolewe kulingana na sheria na sio kulingana na uwezo wa kifedha, cheo kazini na kadhalika. Kwa mfano utaona kuwa sheria inabana mwananchi wa kawaida kuliko hao wafanyi kazi wa Serikali. Ni maoni yangu kuwa iwe ni askari, ni mkulima ni nani, akiwa amefanya makosa basi sheria ifanye kazi sawasawa bila ubaguzi au

upendeleo.

Pia kuwe na uhuru wa vyombo vya habari, redio, magazeti, TV na zinginezo kutoa habari kwa umma bila vizuizi. Kwani vyombo hivyo vimekuwa na vizuizi na ndivyo vya kutuwezesha kujua vile tunavyoongozwa. Kuna visa vinavyotokea vya kusikitisha lakini vyombo hivyo havitoi habari kwa kuwa havijalindwa kikatiba. Unakuta kuwa vinafunikwa. Kama ni mtu mkubwa amefanya jambo basi linafunikwa halielezewi. Kwa hivyo tungeomba ya kuwa kuwe na uhuru katika vyombo hivi.

Kwa upande wa elimu ningependekeza kuwa hawa walimu wa shule ya vidudu, nursery school teachers pia nao ikiwezekana walipwe na Serikali badala ya kulipwa na wazazi. Wazazi wanapata shinda kuchanga, kutoa michango ili kulipa wale walimu wa nursery school. Ningependelea kuwa hao walimu wa nursery school nao walipwe na Serikali. Ni hayo tu.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana Bi. Mwang'ombe. Javan Rongoma.

**Javan Rongoma:** Asanteni sana. Mimi ni Javan Rongoma kutoka Kishamba location. Tulitayarisha memo yetu ambayo imeshawakilishwa hapa lakini ningependa pia kutoa langu ambalo lilikwenda kunijia nikiwa nyumbani baada ya kuachana na wenzangu. Katika Katiba za nchi majirani hapa na Kenya wanayo wanaita 'schedule one, two, three, four' ambayo Katiba yetu nafikiri haina. Baada ya hiyo dibaji ambayo pia haiko. Sasa katika hizo schedules, moja ambayo wameingiza katika Katiba yao ni mpaka wa nchi yetu ya Kenya ningependa uorodheshwa hapo katika Katiba, iwe ijulikane kamili kamili kwamba nchi yetu ya Kenya imechukua nafasi mpaka wapi kutoka wapi.

Ya pili hizi districts pia ningetaka ziwe na mipaka ambayo imeorodheshwa katika Katiba kwa sababu ikiwachwa huru namna hiyo, mambo mengi hutokea baada ya Katiba kuchapishwa. Kama hivi sasa ninaweza kutoa mfano wa Taita Taveta district. Ile ramani ambayo ilikuwa imewekwa na mkoloni 1963 and below, ilikuwa imeweka mipaka yote katika Kenya, districts zote katika Kenya mipaka yao ilikuwa inajulikana kabisa. Katika Taita Taveta, mpaka wetu wa South (Kusini) umeharibiwa na watu ambao wana influence. Tukienda pande za juu (North) pia imerudishwa nyuma, imewekwa ndani na huo ndio mfano mzuri ambao unaweza kupewa Wataita taveta district kwa sababu naelewa. Pahali ilipokuwa wakati wa ukoloni na pale mpaka wetu wa Taita Taveta uko kwa sasa. Kwa sababu uliharibiwa na wale wanasiasa ambao wakati huo baada ya kupata uhuru walikuwa karibu kabisa na mamlaka. Sasa hapo katika Katiba ningependa mipaka yetu ya cities za Kenya ipangwe vizuri na ma-districts zijulikane.

La pili ningependa kuunga mkono wenzangu ambao wamezungumza juu ya utamaduni na ukabila ambavyo tungependa utamaduni wetu utiliwe mkazo katika Katiba kwa sababu mambo mengi yameharibika kwa sababu Katiba yenyewe haina mkazo wowote katika utamaduni. Na katika utamaduni huo, mambo mengi ambayo yametajwa tajwa hapa kama vile mambo ya heshima ya vijana kutoka zamani, mambo ya kurekebisha tabia mbaya za vijana kama ilivyo sasa. Utamaduni ulikuwa ni kwamba, mzazi yeyote ambaye ni mkubwa wa umri wa babako, lazima umheshimu kama babako.

Kwa hivyo kila district ilikuwa na utamaduni wake ambao walikuwa wanaofuata. Hata si mambo ya ajabu wakati huo, mtoto kukutana na mzee njiani, anakuta anapanda juu ya mti, anaambiwa ateremke na achapwe. Na si babake, lakini anajua huyu ni mzee wa rika ya baba yangu. Na tena akienda akitaja hilo jambo kwa babake nyumbani, huko ndio tena atachapwa zaidi. Kwa hivyo walikuwa wanaogopa kabisa kabisa kuchezacheza njiani. Tena si ajabu wakati huu ukute kijana na msichana wamekaa njiani wanazungumza mambo yao ya karibu kabisa wanakuona wewe mtu mzima unakuja, hawezi kuwacha topic yao. Wanaendelea tu, hata uje upite. Lakini zamani wakati huo, haiwezekani kabisa kabisa. Kitamaduni cha Wataita kwa mfano, ilikuwa haiwezekani hiyo kabisa. Kwanza wakikuona kwa mbali hata huwezi kujua wamepiga kona wapi. Ilikuwa ni utamaduni huo. Kwa hivyo Katiba ya sasa tungependa iunge mkono na ikaaze utamaduni wa mwafrika na huo ukabila ambao makabila ambayo yana utamaduni wake ifuatwe kamili.

Lingine kama wenzangu walivyosema ni juu ya pombe ya mnazi na hizi zingine. Naunga mkono kwa sababu mnazi si kahawa, kahawa ni tunda peke yake. Lakini mnazi hutumiwa wote mzima. Mti wote mzima wa mnazi hutumiwa na mwanadamu ambayo kwao mnazi uko. Wacha ile pombe peke yake. Lakini ule mti ni mti wa zamani na sijui ulikuja kudharauliwa wapi? Lakini tungeomba tusipiganie tu peke yake mnazi, kuna pombe pia za kienyeji ambazo zilikuwa hapo zamani kama hapa Taita, kama umeshapoza mtoto wa mtu, kama haujapeleka pombe ya *muratina* kule, wewe hauwezi kujulikana unataka kuoa huko. You are not serious kama hujapeleka debe ya pombe pale. Maana huo ni utamaduni. Sasa siku hizi, imebadirishwa iwe chai. Hata sijui ndio maana wasichana wanakwenda wanaolewa wanarudishwa. Maana ule utamaduni ulipoachwa hata divorces zimejaa kabisa kabisa. Na tulikuwa na utamaduni mwingine hapa, msichana akishafika umri alikuwa anawekwa ndani ya nyumba au *mwari*.

Walikuwa wanafanyiwa karamu fulani na mafundisho hapo katika nyumba mwezi mmoja. Akitoka pale, ameshakuwa msichana ambaye ameshafundishwa, anajua tabia na desturi za nchi yake au kabila lake pale. Kwa hivyo hapo ndipo amekuwa ataogopa hata kusimama simama na wavulana ovyo ovyo maana ashapitia katika ile course. Kwa hivyo nasisitiza kwamba utamaduni usiachwe katika Katiba, mkaze.

Elimu imetajwa kwamba watoto kutoka nursery hadi form four iwe ya lazima na ya bure. Naunga mkono jambo hilo kwa sababu kwa sasa hivi tulivyo, vijana wengi wamekaa nje hata kanzu hakuna na hata akisema anataka kazi ikipatikana, hawezi kupata, hawezi kufanya kwa sababu elimu hana. Na sio eti ni akili hana, ni kwa sababu mzazi wake alikuwanga tu uniform. Only uniform. Wajua shule zingine ziko very strict. Kama huna uniform, huyo mtoto hasomi hapo. Haya uniform, fees, fees imeondelewa tumeambiwa hivyo, lakini kwa mpango mpango. Afadhali wakati ule tulikuwa tunatoa fees. Mimi nilisomea hapa. Nilikuwa nalipa shilingi tatu kwa mwaka mmoja hapa wakati huo. Three shillings. Kwa hivyo ningetaka Serikali ichukue mzigo huo kutoka kwa wazazi ili kupunguza ile tunaita ‘illiteracy’.

Tukiingia katika hali ya matibabu, hapo mimi naunga mkono waliozungumza hapo mbele kwamba kama elimu itakuwa bure pia

utabibu uwe bure. Kutoka dispensaries, health centers mpaka district hospitals. Kama umekuwa referred kama ni Kenyatta labda huko pengine, lakini sasa hapa chini huo ugonjwa utakupeleka Kenyatta, huo ni wa kupeleka saa ingine. Kwa hivyo pia hapa chini watu wengi wanakufa kwa sababu hawana pesa za kulipia ghalama za matibabu. Kwa hayo machache, ningeomba tafadhalini sasa mchukulie hayo kwa mzigo na nimekomea hapo, asante.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe hapo. Dickson Mwakwari.

**Dickson Mwakwari:** Waheshimiwa wa Commission ya Katiba na wananchi wenzangu, hamjambo. Basi majina yangu ni Dickson Edward Mwakwari. Nimetoka sehemu hii ya Mwakinyungu, kijiji kidogo ambacho kinaitwa Rahai. Na yangu niliyo nayo la kwanza: Ninapendekeza Serikali ijayo, iwe ni Serikali ya majimbo. Kwa sababu tukiwa na Serikali ya majimbo, tutakuwa tunaangalia mambo yetu sisi wenyewe. Kama ni wakuu wa Serikali yetu, tutakuwa sisi wenyewe tutakuwa tunashughulukia mambo yetu wenyewe.

Mashamba yetu tutakuwa tukiyaendeleza na hatutakuwa na unyanyasaji katika sehemu yetu. Kwa sababu kwa hivi sasa tunaweza tukasema, viongozi walioko Serikalini sana sana wale wakuu si sisi wenyewe ni wa kutoka sehemu zingine ambao hata kama ni pesa zimeletwa huku za biashara, sisi Wataita, hatuambiwi ya kwamba kuna pesa ili twende tuzichukue tuzifanyie kazi. Lakini tukiwa ni sisi wenyewe tutakuwa tukijishughulisha na mambo yetu kikamilifu.

Ya pili, ninasema ya kwamba, watoto wasio na wazazi kwa mfano waliofiliwa na wazazi wao kwa ajili ya janga hili la ukimwi, wawe wakipata msaada wa elimu kutoka kwa Serikali. Serikali ijishughulishe na elimu pamoja na chakula chao. Pia wajane ambao hawajaajiriwa, kuwe na kiwango fulani kutoka kwa Serikali ambacho wajane hao watakuwa wakipatiwa kila mwisho wa mwezi ili kuhudumia maisha yao kadhalika na watoto walio nao.

Lingine ninasema ya kwamba, watoto wakitimiza umri wa miaka kumi na nane, wawe wakipatiwa vitambulisho vya nchi yetu bila kulipishwa malipo yoyote. Kwa sababu hivi sasa wanalipishwa. Na ninakumbuka mimi wakati nilichukua kitambulisho sikuwa nimelipishwa chochote. Wakipata vitambulisho, pia wawe wanapatiwa kadi za kupigia kura ili wawe nazo tayari, kukitokea ni kupiga kura kusiwe na shida yeyote.

La mwisho ninasema ya kwamba madaktari walioko ndio wameendeleza ugonjwa huu wa ukimwi. Kwa sababu gani? Kwa sababu ikiwa ameona mgonjwa ana ukimwi, haambiwi kwamba ni ukimwi, bali anafichwa anaambiwa ni homa. Na ikiwa ni homa, yeye akirudi nyumbani homa hiyo inaendelezwa kila mahali. Na raia hawezi kujua kama mtu huyu ana ukimwi. Wanajua tu ana homa ama ana typhoid ama wakati mwingine tunaambiwa ni TB. Na hata akifa, saa zingine kama mikono yetu ina vidonda, tuna-osha tu tukijua mtu huyu amekufa kwa ugonjwa wa TB. Lakini kumbe ni ukimwi na sisi tuliobakia tunabaki na ugonjwa huo katika mili yetu. Kwa hivyo madaktari wawe wakisema ukweli. Asante.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe hapo ndugu yangu. Patrick Karindo. Jemizah Mwandaviro.

**Jemizah Mwandaviro:** Kama mlivyosikia kwa majina yangu mimi ndiye Jemizah Mwandaviro sio Jeniffer Mwandaviro. Wageni wetu wa siku ya leo pamoja na viongozi wetu nawasalimu nyote hamjambo. Kwangu mimi yote ambayo nilikuwa nizungumze naona kama nimeongea kwa kuchelewa. Yote hayo yashasemwa lakini langu sasa ni kuunga mkono yote yaliyosemwa na wenzangu.

Kwanza yangu ningeanza na wale watu wa *mwalugongo*. Kwa kweli mtu wa *mwalugongo* ambaye ni mzee wa kijiji ana kazi kubwa sana kwa sababu yote ambayo huwa inahusika yeye ndiye huwa anatujulisha. Kama ni mkutano ni lazima yeye atoke atujulishe ndio sasa tujue kesho kuna mkutano ama kama ni kazi ya kijiji lazima tujue kupitia kwa mzee wa kijiji. Kwa hivyo mimi ningesema wangekuwa wanapatiwa kamshahara kidogo kwa kazi yao ambayo huwa anafanya.

Pili ni kuhusu chakula hiki cha msaada. Kwa kweli chakula cha msaada huwa tunaletewa lakini hakiji mara kwa mara. Kinakuja kwa muda. Pamoja na hayo ningependa kuongezea kama ingewezekana ikifikia ni wakati wa msimu wa kupanda tuwe tukipata angalao kama ni mbegu ya maharagwe ama ya mahindi ili tuwe na mahali pengine tukipanda shambani tujue hapa, ni mahali tumepewa msaada wa mahindi au maharagwe.

Halafu tatu ni kuhusu walimu wa nursery zile shule za vidudu, mimi ningeomba kama ingewezekana, wawe wakipatiwa mshahara kupitia kwa Serikali. Halafu nne ni ule ugonjwa wa ukimwi. Kwa kweli huu ugonjwa umekuwa ukizungumziwa sana. Hasa kama ingewezekana, hatuwezi kujua huyu ana ukimwi ama huyu hana.

Kama ingewezekana ingekuwa kila mtu angekuwa anapimwa kwa mwaka pengine safari moja au mbili ndio sasa kama ni baba akija pia apewe kama ni kazi kama vile tulipewa kadi za chanjo hii ya akina mama. Tulichanjwa ya tetanus. Awe na kadi akija nyumbani amuonyeshe kama ni mama, mimi nimepimwa nimeonekana hivi. Kama ni mama naye anyoeshe bwana yake nimeonyeshwe hivi niko hivi. Ndio tujue bwana amepatikana au mama amepatikana ama yeyote ambaye amepatikana ajulikane huyu ana tatizo fulani.

Kwa hivyo isiwe ati nikuja kuulizana wewe umetumwa umeambiwa aje? Kama ni baba anasema “haii.. nitakwambia baadaye sijui.” Iwe ni kweli kadi imeonyesha kweli mama huyu ameonekana ako hivi. Ili pengine mama hajapatikana uepukana na huo ugonjwa kuliko kuwa tunawacha watoto bila wazazi. Hiyo ni shida kubwa kweli kwa sababu tunahurumiwa watoto kama hana baba hana mama wengine hata mwishowe pia watoto pia wanaenda. Kwa hayo mimi nimefika hapo. Karibuni tena wageni wetu.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Sasa kuna wale ambao wako na maandishi (memorandum) na hawataki kuzungumza. Kama uko na memorandum na hutaki kuzungumza unaweza kuleta na kuji-register hapa. Kuna Jotham Ruma, ameacha

memorandum yake hapa na hajajiandikisha. Humphrey Wughoma.

**Humphrey Wughoma:** Kwa majina mimi ni Humphrey Wughoma, natoka kijiji cha Msau, Koroi. Chairman wa kikao hiki na wananchi wote hamjambo. Mimi naunga mkono yule msemaji wa kwanza na wa pili kwa yale yote walizungumzia. Lakini kwa upande wangu nilikuwa na kitu kimoja nilikuwa nataka kukiguzia ambacho nafikiri katika hawa wawili walioongea hawakulitaja. Nazungumzia habari ya hizi tume zinazochaguliwa na nikizungmzia hivyo sisemi eti ni Tume hii ya Katiba. Kuna tume nyingi huwa zinachaguliwa hapa Kenya. Hasa Rais mwenyewe ndiye huzichagua hizi tume. Tume za kuchunguza mambo fulani fulani siziwepo kwani tume hizo zinatumia pesa nyingi za mwananchi na baada ya kumaliza kazi yao, Serikali haitangazi matokeo ya tume hizi kirasmi. Ama kwa wakati mwingine inavunjwa kabla ya kumaliza kazi yake. Tume kama hiyo twaweza kusema ambayo ilivunja kila mwananchi moyo kabisa ni ile ilikuwa ya kifo cha Dr. Ouko. Hiyo haikutoa chochote kabisa. Watu walikuja kutoka ng'ambo, wanakuja kuchunguza hizo tume, pesa wakatumia kwa wingi na hiyo tume haikutoa uamuzi wao.

Number two. Nazungumzia habari ya elections. Ningeona ni vizuri diwani ama mbunge asipatiwe nafasi ya kutafuta kura zaidi ya vipindi viwili. Tukiangalia kwa sasa kuna wabunge wengine tangu 1993 yeye yuko pale mpaka saa hii. Lakini kama wangepewa vipindi angalao hata mimi mwenyewe naweza kujitokeza nikajaribu, lakini sasa ni yeye tu ni yeye tu.

Tatu, limetajwa ni rafiki yangu mmoja hapa, mtu mmoja, kazi moja. Hiyo kuna vijana wengi ambao wanakosa kazi na unaona mtu mwingine anakushikilia kazi ishirini. Hajali wengine.

Nne kabisa ambalo ni la mwisho, nilikuwa nazungumzia habari ya plots hizi za biashara. Tuangalie kama Voi hapa. Tukiangalia mimi nikienda hapa na natoka wilaya hii hii ya Taita, nikijaribu kutafuta kiwanja pale, siwezi pata. Mtu anatoka sijui wapi, Nairobi, Kisumu wao ndio wako na ma-plot mengi hapo Voi. Sasa kwa upande wangu nilikuwa naonelea Katiba iwekwe ya plot za biashara zipewanwe kwa mwananchi wa hapo hapo au mwananchi wa wilaya inayohusika. Nafikiri yangu ni hayo.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe hapo Mzee wangu, jiandikishe pale. Silvano Mzee.

**Silvanus Mzee:** Asante sana Commissioners na waliohudhuria nyote hamjambo. Mimi kwa majina ni Silvano Mzee na langu la kwanza linaenda kwa local authority, county council plots. Nilikuwa naonelea kama county council ingekuwa na authority ya kuweza ku-prosecute mtu ambaye ana-encroach yaani kwa mfano unakuwa na plot na unakuta mwenzako labda hasa kwa upande wa wanawake ambao nimeona hiyo example. Mtu anaingia na akienda kwa county council anaambiwa sisi hatuna uwezo wa kumtoa huyo mtu na wao wenyewe ndio walitoa hiyo plot. Kwa hivyo naonelea kwamba county council yenyewe iwe na hiyo authority ukienda pale kwa msaada wote wachukue hilo jukumu badala ya kukurudisha ama kukupeleka kwa adminstration ama kwa upande wo wote ule.

Hilo ni la kwanza. La pili linahusika na land hivo hivo. Kwangu naonelea kwamba mashamba mengi yameshaandikishwa lakini

utakuta kwamba yule mtu ambaye amepata title deed ndiye anaweza kushitaki mtu ambaye ana-encroach ama mtu ambaye anamtatiza kwa shamba. Anaweza kumshitaki kwa sababu ana title deed lakini hivi kwa sasa hivi utakuta mtu ambaye ana number itachukua muda mrefu sana hata kukuja ku-settle hiyo case. Unakuta wanasumbuana, wanasumbuana na huyo mtu atakuwa na uwezo mdogo sana. Kwa hivyo nilikuwa naona Serikali yenyewe ingechukua hilo jukumu hata kwa vile wote wawili walikuwa pale na number wameshapata. Kwa hivyo mtu awe na uwezo wakati wa kumshitaki mtu ambaye wanasumbuana moja kwa moja.

Halafu lingine ni kuhusu waalimu. Kwa maoni yangu naona ya kwamba ni vizuri walimu wawe wakipelekwa in-service za guidance na counseling mara kwa mara. Yaani kwa mfano sasa hivi unakuta walimu wanafundisha watoto wengine ambao labda wameachwa na wazazi wao kwa sababu ya ugonjwa wa ukimwi na wengine ni mayatima. Sasa unakuta mwalimu anahimizwa asiadhibu labda kwa kiboko, atoe adhibu yeyote ama afanye guidance and counseling.

Lakini unakuta mwalimu huyo huyo ana ujuzi mdogo sana kwa hiyo guidance and counseling. Na hii guidance and counseling utakuta kwamba ni jambo ambalo linasomewa hata kwa degree lakini utakuta kwamba mwalimu ana uwezo mdogo sana wa kufanya hii guidance and counseling. Kwa hivyo nilikuwa naona kwamba wawe wakipelekwa kwa in-service za guidance and counseling mara kwa mara ili waweze kuwasaidia hawa watoto.

La mwisho, nilikuwa naona kwamba kwa upande wa elimu hapo hapo, kanisa liwe na jukumu zaidi la kuweza kukuwa na maongozi ya kiroho hasa kwa mashule. Yaani wawe na programme. Haswa haswa programme. Bali na pastoral programme, wao wenyewe wawe na programme yao. Maanake unakuta walimu sio wote ambao wako na ule ujuzi wa kiroho lakini utakuta kanisa lenyewe linaweza kuwa na nafasi nzuri kwa upande huo. Kwa hivyo langu nasisitiza hapo ni wawe na programme hasa katika mashule. Kwa hivyo kwa hayo, nashukuru sana.

**Com. Keriako Tobiko:** Okey asante sana. Jiandikishe hapo ndugu yangu. Harun Hassan.

**Harun Hassan:** Tume ya kurekebisha Katiba na wananchi wa Msau na Mchanganyiko, hamjambo. Kwanza mimi niko hapa kuakilisha masilahi ya waislamu lakini baada ya kuwasomea yale waislamu wanayotaka, nitarudi nifafanue kidogo mambo ambayo nafikiri yanahusu Wakenya kwa ujumla. Kwanza kwa waislamu: Kadhi Mkuu yaani Chief Kadhi lazima achaguliwe na waislamu wenyewe sio achaguliwe na Serikali. Kama kwa saa hizi, twaweza kuwa Rais ni Mkristu kwa hivyo hana ruhusa wa kuchagua Kadhi Mkuu, Kadhi Mkuu achaguliwe na waislamu.

Point number two. Baada ya hayo tuwe na Kadhi wakuu katika division, district na provincial na wote wachaguliwe na waislamu. Halafu kati ya hao kadhi wakuu, lazima wawe na qualifications zifuatazo:

1. Awe mwanaume.
2. Lazima awe muislamu.

3. Awe mwenye elimu ya kidini.
4. Awe ni mchamungu.
5. Awe mwadilifu.
6. Awe na umri wa miaka thelathini na mitano na kuendelea.
7. Awe na kumbukumbu nzuri.

Halafu katika upande wa hukumu, yaani Judiciary, kama yeye Chief Kadhi mkuu ameshindwa na masilahi fulani, hayo masilahi tulikuwa tunayaomba yapelekwa kwa mujjahid. Mujjahid ambao ni watu wanasimamia waislamu wote kote duniani na nafikiria headquarter yao iko Iran. Mujjahid, you can note somewhere.

Mavazi ya kitaifa: Mwanaume avae nguo ya kiume na mke inafaa afae nguo za kike zenye kuzitili uchi. Kwa mfano, nguo izitili mwili wote, isipokuwa uso, viganja vya mikono na viganja vya miguu. Hata mashuleni wavae wakiheshimu dini. Kwa mfano kama sisi waislamu twaweza sema tuko na nguo zetu rasmi. Wanawake wanafaa wavae buibui na wanaume kanzu. Sasa kwa hivyo tulikuwa tunaomba pia Serikali ya Kenya, twashangaa sana kuwaona mandugu zetu wa kike wanavaa mini-skirt, nini. Kwa hivyo Serikali yetu kama pia ni Wakristu, muwe na vazi la heshima.

Point number three: Twaona katika nchi yetu kuna sherehe, sherehe kama vile Christmas mko na Easter. Pia sisi waislamu tumeona tu mumetupa tu sikukuu moja ya I-dul-fitr. Tulikuwa tunaulizia pia mtambue sikukuu kama ya Idilhaji, hashula, ambazo ziwe ni public holidays. Juu hata kama nyinyi ni wakristu mungefurahia pia kupumzika siku ya Idilhaji ama siku ya Hashula ama siku ya I-dul-fitr pia.

Ibada: Katika ibada hapa kuna kitu inasema katika sheria ya Kenya kuwe na uhuru wa kuabudu. Sasa huu uhuru wa kuabudu twashangaa sana twasikia kuwa kuna kanisa zingine zimeingia nchini Kenya za kuomba mashetani kuomba nini. Sasa tulikuwa tunaona, badala ya kuwe na uhuru wa kuabudu, inafaa iwe kuwe na uhuru wa dini. Sio uhuru wa kuabudu. Maana tukisema uhuru wa dini tutakuwa na wakristu, waislamu na pengine dhehebu lingine moja hivi. Lakini tukisema uhuru wa kuabudu, mtu anaweza kuabudu hata jiwe. Kwa hivyo tuwe na uhuru wa dini wala sio uhuru wa kuabudu.

Uraia: Katika uraia yaani citizenship, tulikuwa tunaulizia kama ingewezekana Serikali ipatie mtu uraia mara mbili. Yaani ya kwanza iwe ni pahali pa kuzaliwa ‘automatic citizenship’ halafu ya pili pahali popote sasa waweza kwenda kama umeenda nchi ile umehamia, iwe sasa ni citizenship ya pili.

Point number six: Haki za watoto na wanawake. Zote ziwe za Kiislamu. Watoto wafundishwe dini yao hata mashuleni. Halafu kuna point number saba, kazi na nafasi ya masomo ya nje. Siku hizi jameni twashangaa zaidi baada ya Osama kulipua hilo jimbo katika Marekani, umekuwa ukienda kutafuta kama ni ma-passport nini. Wauliziwa jina lako wakishasikia tu Muhammad ama Hassan nini, wanaweza kuleta mambo mengi ya uchunguzi. Kwa hivyo tulikuwa tunaomba kama ni haki kama hizo zitolewe

bila kupendelea upande wowote.

La mwisho ni kitambulisho: Hati ya kusafiria na hati ya kuzaliwa. Kama hizi zote tuseme kitambulisho, ID card, hati ya kusafiria (passport) na birth certificate, tulikuwa tunaonelea sisi waislamu juu sisi wote ni Wakenya na tunapenda Kenya, kila mtu mwananchi anaitwa Mkenya awe na hizo vitu. Kama tu vile uko na kitambulisho upatiwe pia passport na birth certificate bila vikwazo vingi. Hayo ndio tulikuwa nayo upande wa Kiislamu.

Sasa nitazungumzia mawili matatu kuhusu nchi ya Kenya. Kwanza kabisa nilikuwa nataka …sijui kama Wakenya wangefikiria kitu kimoja! Watu wengi wanasema kuwe na *majimbo*, sikatai kuwe na *majimbo*, lakini wakati kama huu mimi kama ningeulizwa ningesema kwanza tujipatie miaka ishirini ijayo ndio tuanzishe mfumo wa *majimbo*. Maanake saa hivi kama tujuavyo Kenya ina makabila arobaini na mawili.

Kwa hivyo ukisema *majimbo*, watu wale hawaelewi wanaanza kuangalia Mkikuyu yuko hapa, Mjaluo yuko hapa, nani yuko hapa. Na kusema ukweli kama tunataka sisi Wakenya tuzuie umwagikaji wa damu katika hii nchi, tulikuwa tunaona ni haki kusiwe na utawala huo wa majimbo maanake kwa saa hizi, mwananchi ungimwambia majimbo, sio wote wanaelewa. Mwingine anafikiria Mkikuyu, nani nani. Kwa hivyo kuzuia hayo, nilikuwa nasema Serikali iwe na vyama viwili peke yake.

Halafu kumekuwa na shida katika uamuzi wa kura katika nchi yetu. Sasa nilikuwa naonelea kwa upande wangu ili kuzuia michafuko baada ya kura ama nini, tulikuwa tunaonelea yule atakayepata kura mingi katika uchaguzi ujao, atangazwe kuwa Rais. Halafu yule atakuwa na votes, yaani number two, atangazwe Waziri Mkuu. Natumai tukiwa na vyama viwili, hapo tutakuwa tumedumisha amani.

Jambo la mwisho nilikuwa nataka nizungumzie kuhusu bangi. Bangi kama a herbal, we can talk of it is a drug. Na ikiwa kama ulaya, twasikia Britain, U.S. A wameagiza vyuo vyao vikuu wafanye uchunguzi kuhusu huu mumea, kwa nini Katiba yetu isifanye uchunguzi kuhusu bangi halafu waangalie vile wanaweza i-control kuliko kukashifu kitu ambacho hutumii. Kwa hivyo nilikuwa naulizia Serikali pia iangalie mambo ya bangi. Intensive research kuhusu hiyo kitu.

Halafu kuna jambo la mwisho, kuna hii sheria ilibuniwa juzi ati hakuna kuadhibiwa shuleni. Sasa hata kama sisi vile tulikuwa tunasoma, tulikuwa tunaadhibiwa na waalimu, ndiyo at least tukapata kitu kidogo. Kwa hivyo nilikuwa naomba kama ingewezekana, kama ni caning nini ziruhusiwe katika shule ili ile adabu ya watoto at least iwe high grade kidogo. Kwa hivyo ni hayo machache tu shukrani.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana Bwana Hassan, jiandikishe pale. Delvan Munyasa.

**Delvan Munyasa:** Kwa maofisa wetu wa leo wa Katiba na wananchi kwa ujumla nawasalimu nyote. Kwa majina mimi

naitwa Delvan Munyasa kutoka Ronye Mombota. Jambo langu la kwanza…. nafikiri mengine naunga mkono ambayo yamesemwa na wenzangu na mengine nitazungumza. La kwanza, ni kuhusu elimu. Kwa hakika sisi wazazi tunaumia sana tena sana. Elimu tunataka lakini uwezo hatuna. Kwa hivyo ningeliomba Katiba hii yetu ya Kenya iangalie sana mambo ya elimu juu ya watoto kwanzia darasa la kwanza mpaka standard eight wasome bure.

La pili ni juu ya haki ya mwananchi. Mwananchi ana haki zake lakini hatimiziwi na shida hii inaendelea sana na mwananchi anajaribu vile awezavyo lakini hakuna mwelekeo na inakuwa ni kilio kwa mwananchi analilia Serikali 'kwa nini tumepata uhuru lakini matunda hatuyaoni'. Sababu ni hii mwananchi ana ufugaji ana ng'ombe, mbuzi nasema kwa ujumla ufugaji. Lakini mnyama wake akiliwa na mnyama wa porini, ukijaribu kupiga ripoti kwa game warden, hakuna kitu ambayo inachukuliwa kwa haraka.

Mimi kwa hakika ningelipendekeza haki ya mwananchi iangaliwe sana kama ni ngombe wake ameuliwa, alipwe. Hata kama ni elfu ishirini. Lakini ahakikishiwe ng'ombe wake amelipwa. Nasikitika mtu akiuliwa, ukipeleka ripoti, hakuna hatua inachukuliwa haraka. Ni lazima uchunguzwe kwa muda mrefu na labda kiwango utakuja lipwa na tunavyojua mwanadamu hana kiwango cha kulipwa. Lakini kitu ambacho atakuja kulipwa, ni kitu kidogo sana na kitakuwa kimechukua muda. Atasumbuliwa hili na hili ndipo alipwe. Kwa hivyo hiyo tunaomba, Katiba yetu ya nchi ya Kenya, iangalie jambo kama hilo. Malipo ya mwanadamu kwa sababu hakuna kiwango hata akilipwa milioni mbili, sio eti amelipwa ghalama la mtu.

La tatu: Ni kuhusu akina *mwalugongo*. Kwa hakika hawa watu nawahurumia sana. Hata jambo likija kufika kwa Rais limeendea kwa *mwalugongo*. Ni mtu mwenye kazi ngumu kweli kweli hakika. Kwa sababu wakati wowote akilala hakulala ana uhuru wa kuamshwa. Ni saa nane anapigiwa mlango na anashughulikia jambo la mwananchi. Na akishalishughulikia kwa hakika hawa huchukua jukumu kushughulikia mwananchi vilivyo. Na jambo hilo mpaka lipitie kwa chifu na chifu achukue hatua vile iwezekanavyo. Lakini limetokana na *mwalugongo*, kazi ngumu zaidi. Kwa hivyo mimi ningelipendekeza hawa watu wawe wakilipwa. Ni haki.

Pointi ya nne, tulipopata uhuru, tulifurahi sana na tukapiga vigelegele sana tukijua kweli tumepata uhuru, tutafanikiwa, tutaona maendeleo na maendeleo hiyo tuliisikia kwa masikio na vitendo vilitendwa. Tuliambiwa mashule yatajengwa na kweli yalijengwa tuliona. Mahospitali yatajengwa na kweli yalijengwa tuliona. Lakini, jambo la kushangaza, mahospitali haya yamekuwa ni ya matajiri, maskini anaumia. Kwa sababu ya nini? Ukienda pale mahitaji ambayo utaambiwa utashindwa. Basi utabaki ukiuliza sasa nitafanya nini?" Ningelipendekeza madawa yawe ya bure.

Naenda la tano. Kwa hakika wagonjwa wanapougua, shida moja huwa usafirishaji. Kama mimi hapa nimesimama nimetoka sehemu za Mombota. Na kama niko na mgonjwa, wakati wa mvua hakika siwezi kumpeleka hospitali kwa sababu ya barabara. Na mahali pengine panategemea kivuko, madaraja hamna. Wakati wa mvua unaweza kuja na mgonjwa mkasumbaa hapo hapo kwa daraja hata mgonjwa akafa. Hapo mtapitia wapi? Kwa hivyo jambo hilo Serikali iangalie. Watutengenezee madaraja ili mwananchi ahudumiwe vilivyo. Kwa hivyo kwa hayo machache, nafikiri nimefika mwisho.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana Mzee wangu. Jiandikishe hapo. Philip Mwalomo.Patrick Mwemba. Evans Kasenge.

**Delvan Munyasa:** Jambo lingine ambalo ningelisisitiza ni juu ya watu ambao wali-retire. Kwa hakika tunapata shida sana mimi mojawapo nikiwa nime-retire. Shida yenyewe ni malipo kulingana na miaka ambayo imefikia ya kupumzika, lakini ukienda pale habari ya malipo unaambiwa ngoja. Na form ishajazwa lakini naambiwa 'Tuko katika shughuli, tunaishughulikia, kwa hivyo tumeshukuru kwa sababu umetuletea kilio chako na tuko katika hali ya kushughulikia mambo yako." Kwa hivyo nataka mambo hiyo mtu akisha-retire amaliziwe haraka aachane nayo.

**Evans Kasenge:** Kwa mabwana wote walioko katika mkao huu wa leo, mimi kwa jina ni Evans Kasenge mtaa wa Ronye Malubini karibu na Councillor na nadhani mnanielewa. Basi nitasema machache tu. Kwa jambo la retirement. Mimi nilikuwa katika idara ya 'Ministry of Culture and Social Services'. Na nilianza kazi hiyo mwaka wa 1974 kule Bura Rehabilitation Centre na wenzangu wengine hapo hapo kuendelea kwa miaka mitano halafu transfer Mombasa. Mwaka wa 1979 mpaka 1980. Miaka miwili. Tena ku-retire ni 1st July 1993. Bado malipo. Ni kama fungu la pili ambalo zijamaliziwa. La kwanza lile linaitwa N.S.S.F. nilipigana sana miaka minne. Barua nimeandika, maofisa waliniandikisha wakapeleka kwa chief commissioner kuandika ripoti zangu. Sasa barua ikaenda, majibu sikupata. Nikaandika ingine ya pili sikupata, mpaka miaka minne, nilikuja kupata mwaka wa tano. 1998 ndio nilipata hiyo. Nimekwenda Wundanyi mara mingi sana nikiambiwa "ngoja mambo yako utajibiwa." Nikienda kila mara naambiwa ' majibu yako utayachukua'. Mpaka miaka mitatu, mpaka miaka minne. Sasa ninapoelewa kwamba kuna promotion ambapo inafikia karibu na ku-retire, mtu anafanya miaka mitatu, minne kwa ule mshahara mkubwa ile up-grading lakini niliona kwa roho imekuja iwezekane kwamba nipate hiyo.

Na ilikuwa 1988, ndio promotion ilitengenezwa hapo. Salary ilikuwa chini sana, nilianzia na mia tatu hapo Rehabilitation Center Bura. Kwendelea, kwendelea, kuja Wundayi 1991, miaka mitatu. Tukapanda kidogo ikakuwa elfu moja na shilingi hamsini. Hapo tumepanda eti.

**Com. Keriako Tobiko:** Mzee wangu nikuulize, unapendekeza nini?

**Evans Kasenge:** Sasa la mwisho ni ile promotion sijapewa mpaka sasa. Lakini nimetuma barua nangojea. Sasa nimeandika barua ya kwanza 1998, majibu sikupata. Tena April tena, nikaandika sikupata majibu tena. Mpaka tena ya tatu hivi nikatuma ingine na nangoja majibu. Na copy ziko. Zote nimeweka pending. Na sijui kwa nini siwezi kupatiwa. Naambiwa 'ngoja kidogo' . Sasa kuna wale ambao walilipwa ile inaitwa handshake. Sasa wao walilipwa haraka sana na mimi mtu original wa miaka 55 sipati hiyo. Na mimi nikaona….

**Com. Keriako Tobiko:** Pendekezo lako ni nini? Mzee wangu nauliza pendekezo lako ni gani katika hii Katiba mpya. Tufanye namna gani ndio kusikuwe na kesi nyingine kama hiyo yako.

**Evans Kasenge:** Ni ile tu nilisema ya promotion. Hiyo tu.

**Com. Keriako Tobiko:** Ilipwe mara moja?

**Evans Kasenge:** Ilipwe mara moja. Ni hiyo tu. Asante

**Com. Keriako Tobiko:** Asante. Jiandikishe pale. Jotham Ruma. Margaret Wakesho. Peris Kijala.

**Peris Kijala:** Kwa majina mimi ni Peris Kijala kutoka Rowenyika. Mimi nimetoa asante kwa Tume ya Katiba vile imefika hapa Taita. Kwa sababu tulikuwa tunasikia tu ikipita kwa mbali lakini kwa vile imekuja hapa karibu, tumetoa shukrani sana kuwaona. Kwa sababu sisi tulikuwa tunalia, ni wapi Katiba tutaandika na inaandikiwa wapi? Tulikuwa tunasikia Katiba ikiandikwa tu kwa magazeti ama kwa vitabu lakini hatujawahi kuiandika sisi wenyewe. Tulikuwa tunatumia ya wakoloni, na leo hii nina furaha kusikia hiyo Katiba nimekuja kuiona leo. Nilikuwa nafikiria labda ningekufa kabla sijawahi kuandikishwa kwa Katiba. Kwa hivyo leo ni furaha kwangu na kwa hiyo Katiba mimi ninatoa maoni yangu, mengine nimeunga mkono ambayo yamesemwa. Lakini sasa nitaunga mkono na mengine nitasema.

Sisi kwa kweli tunataka majimbo. Lakini hiyo majimbo mimi ningependekeza majimbo, tunataka majimbo yale ambayo si ya vita. Kwa sababu kuna majimbo mengine hapa tunasema majimbo kumbe si majimbo ya kisawasawa. Inakuwa ni majimbo ya kivita. Kwa hivyo ningependekeza majimbo hayo isiwe majimbo ya vita kama vile kulitokea mwaka mwingine hapo Likoni. Hayo sio majimbo mazuri. Tunataka tuwe na majimbo ya kufuata sheria kikamilifu na sheria hiyo iwe inasimamiwa kikamilifu. Na hayo majimbo yawe ni ya kabila vile Mungu alitenga. Kwa sababu Mungu alijua ndio akatenga na yakatengwa na mipaka yao.

Ndio tukapewa lugha tofauti tofauti. Kwa sababu ya hizo lugha, tufuate hizo lugha zile tumepewa. Na tukapewa hizo kabila kufuatia na mipango ya Mungu mwenyewe. Na Mungu akapanga Wakamba wakae kwao wakiwa wanasikilizana lugha kwa nchi yao. Na Wataita wakawa ni Wataita watupu wanasikilizana. Wakikuyu hivyo hivyo pia mpaka Wazungu. Mpaka wengine tukapewa rangi tofauti tofauti. Na tunataka hiyo ifuatiliwe hivyo.

Kama ni Mkamba anakuja kukaa Taita, aje kwa mpango na kwa kufuatilia sheria. Asiwe amekuja kuingia ni Mtaita, awe ni Mtaita na aje na sheria zake kutoka kwa Wakamba kuleta kwa Wataita. Akija kwa Mtaita, akaribishwe kikamilifu kama vile sheria zilikuwa zamani. Akaribishwe na wazee wa nchi. Kama ni Mtaita, akaribishwe na Wataita na asipewe mamlaka yoyote ya kumiliki ama ya kugawanya miji ya Taita. Awe tu amekaribishwa kama vile tunaolewa kwa Wakikuyu, tunaolewa kwa Wakamba. Awe tu ni kama mtu ameolewa, asiwe na mamlaka na tuishi kwa usalama tusiwe kuwa na vita. Hiyo ndiyo majimbo mimi ninapendekeza.

Pili ni haki za watoto. Kuna haki za watoto za elimu. Hizo haki za watoto za elimu zinatakikana zichukuliwe kisheria. Kwa sababu kuna hizi haki za elimu, watoto kweli wana elimu, hii elimu nayo kila mara tunaambiwa elimu ni bure. Hata kwa magazeti, kwa maredio, inatangazwa elimu ni bure kwa watoto na watu wazima. Lakini tafadhali sio bure kwa wakati huu. Hakuna cha bure.Tunaona hakuna cha bure ingawaje inatangazwa. Imekuwa ni pesa na sio elimu ile ya zamani.

Elimu ya leo imekuwa ni ya pesa. Tunalipa karo, vile tuliambiwa hatulipi, tunalipa. Na zamani tulikuwa kweli tunalipa na tunalipia ukweli. Kwa sababu nikilipa tu karo ya shule, ninapewa kitabu hapo, ninapewa kalamu, sitasumbuka, sitafukuzwa. Ninafukuziwa tu kama mzazi wangu hakuenda kufanya kazi. Lakini siku hizi, mtoto anakosa elimu kwa kitu kidogo tu. Kule kufukuzwa kwa kitabu, kwa kalamu, kwa uniform na kwa fees. Ingawaje tumeambiwa hakuna malipo.

Kwa hivyo ningependekeza Katiba hii igeuze ule mfumo wa zamani, mtoto kupewa kila kitu hapo kwa hapo bila mzazi kwenda kununua kitabu, bila kuenda kununua kalamu, awe akiingia shule ameingia. Mzazi awachwe na uniform. Hata kama ni malipo, iwe si malipo ya juu, iwe ni malipo ya kadre ambayo mzazi ataweza kukusanya kulipiza huyo mtoto. Na akiwa hivyo, nafikiri sote tutasoma. Kwa sababu siku hizi elimu yetu imekuwa chini kwa sababu ya mtoto kufukuzwa.

Pia uchunguzi uwe kwa mwalimu. Siku hizi discipline imekosekana, kwa mwalimu mpaka kwa mtoto. Mtoto hana discipline, mwalimu hana discipline. Mwalimu na mtoto ni sawa. Kwa mavazi pia kwa kila kitu. Mwalimu unamwona ni mwalimu, anavuta sigara mbele ya mtoto, analewa mbele ya mtoto, na mtoto naye anafuata hivyo hivyo. Vile amleavyo ndivyo akuavyo. Kwa hivyo tunapata hasara. Na kumefukuzwa kwa mtoto kumekuwa ni ovyo.

Mambo ingine ni ya mzazi inapelekwa kwa mtoto. Badala ya mtoto kukaa asome, anatolewa hapo anafukuzwa kwa sababu ya makosa ya mzazi. Badala ya huyo mzazi kuitwa na kutatua hiyo kesi, sasa inakuwa kesi ni kwa mtoto. Mtoto anafukuzwa siku mbili, siku tatu yuko nyumbani amefukuziwa ati ni kazi ya umoja, pesa za shule, na pesa za shule mtoto hatafuti mzazi ndiye anatafuta. Na hapa tuna kamati zile za mashule.

Kamati za mashule tafadhali zirekebishwe na zifanye kazi zao kikamilifu. Tunapochagua kamati za mashule sio tunachagua tu zifukuze mtoto, tunachagua hiyo kamati i-deal na mzazi wa mtoto. Ndio maana tunachagua hiyo kamati. Na kama hawezi, ikae hiyo kamati. Kwa sababu tunaona mara nyingi mtoto anapata hasara kwa sababu ya kufukuzwa fukuzwa ovyo ovyo na hiyo kamati, na anafukuziwa mambo ya mzazi.

Pili ni haki za wale wasichana wanaozaa nje ya ndoa. Wasichana hao wanapata taabu kwa sababu akizaa mtoto huyo, hana mahali pa kukaa. Huyo mtoto atakuwa anaranda randa ovyo ovyo kwa sababu amekosewa haki. Hapati haki kwa sababu ni mtoto wa mwanamke. Mwanamke kwa mzazi hapatiwi haki. Kama ni shamba hapatiwi, hata mbuzi hapatiwi. Hakuna chochote atakachopatiwa hapo kwa sababu yeye ni mwanamke. Lakini mwanaume hapo kwa mzazi ana haki. Na hapo ndio naomba

Katiba irekebishwe kama mzazi ndiye amezaa mwanamke na amezaa mwanaume, mzazi huyo apatie mwanamke haki na mwanaume. Kwa sababu wote ni watoto wake, alibeba miezi tisa. Hakuna mwingine alibebwa mwezi mmoja.

Kwa hivyo hao watoto Katiba irekebishwe watoto hao waangaliwe na wapewe haki. Wale wanaokaa nje wapewe mashamba nao wao wawe na haki zao kama vile mwanaume anayepatiwa. Labda awe ameolewa. Na kama ameolewa na kwa bahati mbaya ameregeshwa kwa sababu siju hizi ni kuolewa na kuregeshwa. Akiregeshwa pia, aangaliwe kikamilifu. Atafanywa nini. Mambo yake yaangaliwe na sio tu kuchukuliwa ovyo ovyo. Kwa sababu kuna mtindo umekuja eti kwa vile tumewachana na huyo bwana sasa watoto ninanyang'anywa na makosa haiangaliwi. Saa zingine mtu anaambiwa hata huyo mtoto asiende kumwona. Ama akiwa amepata kazi asipatiwe chochote na huyo mtoto. Kwa hivyo sheria irekebishe hiyo.

Kwa elimu nimeomba ikiwezekane sheria igeuze walimu wa nursery walipwe na Serikali kama wale walimu wengine ambao wanalipishwa. Walimu wa nursery walipwe na Serikali, sio watumiwe kwa wazazi. Kwa sababu kazi anayofanya ni kubwa na unaona halipwi mshahara wa maana. Saa ingine analipwa mia mbili ama mia nane. Hata haifiki elfu moja na kazi anayofanya yeye ndiye chanzo cha elimu.

Sasa ninazungumzia juu ya mifugo yetu. Tunazungumzia juu ya wanyama wa pori lakini hatujazungumzia juu ya mifugo yetu tunayo kaa nayo. Hiyo sheria tunaomba ikiwezekana iangaliwe vizuri kwa sababu ndovu ama nyati ikiingia kwa shamba ninadai ilipishwe. Ilipwe pesa. Na yule mnyama wangu kama ng'ombe kama nani, akienda kuharibu chakula cha mwenzangu, hayaangaliwi kama vile nyati tunamzingitia.

Tuangalie vile vile kama ni mahindi yako imeharibiwa, iangaliwe ilipwe kisawasawa. Isiwe ni kufutana futana ama isiwe kama hujashika mwenyewe ama mbuzi umpeleke kwa chief ama kwa sub-chief ndio utahakikisha. Isiwe hivyo. Iwe tu nikipata huyo mnyama kwa shamba langu na nijue ni wa nani, nipeleke hilo jina ashikwe ama alipishwe. Hiyo ndiyo yangu na nimekomea hapo.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana Mama. Jiandikishe hapo tafadhali. Collen Nanyika. Anderson Mwaita.

**Anderson Mwaita:** Ma-commissioners wote wa Tume ya kurekebisha Katiba, mimi niko na maoni machache ambayo ningependa hasa kusaidia hata wale wenzangu waliotoa maoni yao. Kwanza ningeanza na hii maoni ya watu kutaka Serikali ya majimbo.

Ningependa kuwapatia mwangaza kidogo kuwaelezea kuwa Serikali ya majimbo haitakuwa labda suluhisho la matatizo. Isipokuwa ningeonelea kuwa kupewe mamlaka kwa hizi local Government, ma-councillor na ma-mayor, naona kitu kama hiyo labda ingeweza kuwasaidia wao wenyewe wataweza kuwafuata ma-councillors na ma-mayors ili kuwatatulia shida zao. Baadala ya kusema kuwa Serikali ya majimbo itaweza kutatua matatizo yao. Local Government wenyewe nina uhakika

watakuwa na uwezo hata wa ku-manage resources za wananchi ambazo ziko hapo within.

Pili ningependekeza namna hii: Ningependekeza katika kuchaguliwa kwa ma-ministers wa cabinet, wasiwe wakitoka katika wale wabunge tunaowachagua. Watu hawa watoke katika tu, watu ambao ni wasomi. Walio na elimu na ujuzi wa kutekeleza kazi tofauti tofauti katika wizara tofauti tofauti. Baada ya kutumia wale wale wabunge kwa sababu mara mingi tunaekewa ma-ministers, wengine wanawekwa kutoka kwa bunge ni ma-ministers lakini ujuzi hawana. Wamepewa tu sababu ya ku-influence mwananchi ambaye alimpigia yule mbunge kura yake, ili kumfurahisha tu mwananchi. Lakini majukumu si yale tunatarajia.

Halafu lingine la tatu, ningesema hawa wabunge pia wawe na muda mfupi. Lile lingine nimesikia wakisema pia, yaani akisha kula mara ya kwanza afanye kwa term ya kwanza na ikiisha hiyo, arudi tu nyumbani apatie nafasi mtu mwingine tena aendelee.

Lingine ni kuhusu kutoa hati za kumiliki mashamba, ID cards na hata hizi cards za upigaji kura. Mimi ningefikiria mtoto kwanza, akifikisha miaka kumi na nane, apewe ID yake kabisa wakati huo huo. Na wakati huo apewe pamoja na kadi yake ya kupiga kura. Halafu akifika miaka kama ishirini na mbili, ishirini na tatu akimaliza masomo, at least awe na uwezo wa kupewa title deed yake free ya shamba. Sio ati kwenda kutoa pesa ama kununua ya kuinua. Wakati shamba ile ni haki yake mwenyewe.

Halafu ningependekeza pia elimu ya bure ya msingi kwa Wakenya wote. Iwe ya bure kabisa sio kama vile tunavyodanganywa tunaambiwa ni ya bure na hatuoni ikiwa ya bure mpaka leo. Halafu na huduma za matibabu, ningependelea pia hizo huduma ziwe ni za bure kwa wananchi wote. Kwa sababu tumeona watu wakiteseka na magonjwa na hata hatimaye wanafariki kwa sababu ya kutokujimudu kwao kifedha.

Halafu ya saba ningepongeza Tume hii na natoa maoni kuwa ingewezekana kwa sababu Katiba hii sio ati tuikibadirisha leo, tutakuwa tumemaliza kabisa kabisa. Vile tunavyo ikosoa hii ambayo iko saa hii. Sio ajabu hata baada ya miaka miwili mitatu, tutaenda kuikosoa hii tena kwa makosa kadha. Kwa hivyo ningependa Tume hii iendelee iwe ikifanya kazi yake kwa muda wote. Nafikiri nitakomea hapo.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu, jiandikishe hapo. Silvia Wakesho.

**Silvia Wakesho:** Kwa majina ni Silvia Wakesho. Langu la kuongeza hapa ni kwamba: Kitu cha kuwaambieni kina mama, akina mama nilikuwa nataka niwaambieni kwamba mwanamke msafi sana yaani mwanamke yule anakuwa msafi sana si mwanamke mzuri ndani ya nyumba. Maanake mwanamke akiwa msafi sana ndani ya nyumba hataki zile kazi chafu chafu. Sasa anataka zile kazi chafu chafu afanyiwe. Sasa kama atakuwa afanyiwe atakuwa akiajili wafanyi kazi kila mara. Sasa wale wafanyi kazi atakuwa akiajili, kila akikaa kidogo ameondoka. Kama ni mfanyi kazi kidogo ameondoka. Ameondoka kwa nini? Kwa maana yule mama ategemea kazi zote afanyiwe na yule mfanyi kazi. Yeye hataki kushika kazi zote za nyumbani.

Sasa yeye kazi akija labda ametoka kazini akaketi hapo, anakaa pale na yule msichana kama ni mfanyi kazi afanya kazi zote amaliza. Yeye yuko hivyo hivyo. Sasa ndio namwambieni kwamba taifa hili, hamtalijenga na usafi bali ni usafi na uchafu mzitoe kwa vyote. Kwa hivyo huo ni mfano nimeuweka kwa wabunge wetu tunawaowachagua hivi tunaenda katika uchaguzi, wabunge tunawachagua ili watufanyie kazi. Na kwa vile tunataka watufanyie kazi, kazi ni matatizo yetu yaliyoko katika vijiji vyetu na mikoa yetu.

Watufanyie kazi kulingana na maoni yetu vile tutakavyo wapa shida zetu. Na tunataka tujue kama wabunge tunapotoa shida zetu, shida zetu zinapitia wapi mpaka zifikie kwa Bunge. Hata zikifika kwa wabunge ndio ziingie Bunge. Yaani matatizo yetu yajulikane sana. Sasa tunataka tuunde siasa nyingine mpya. Tuwe hatutoi – maoni kwa *mwalogongo*, yapitie kwa chief, sub-chief mpaka kwa DO hivo hivo. Yatakuwa yakienda *mwalogongo* na sisi twangoja. Kwa nini mbunge wetu asikuje akatuuliza mna matatizo gani? Na tulimchagua atutetee pale. Atakaa pale Bunge ajue matatizo ya watu wa pahali fulani ni matatizo gani. Anataka afanywe hivi na hivi.

Sio mambo yaende mlongolongo twangoja, twangoja tu. Sisi tunataka tukitoa shida zetu kwa mbunge wetu, tunasema shida zetu ni hizi, zinaenda straightforward. ziende pale zitatuliwe pale pale. Kama haziwezekani ni shida ya fedha, tunaambiwa ‘ mutasubiri fedha haziko za kukamilisha shida yenu.’ Halafu tutajua matatizo yetu yamefika pale, tunangoja tunangoja fedha zikipatikana, tatizo letu litatuliwe. Haya nimemaliza na hapo.

Tunaingia kwa upande wa kazi. Kwa upande wa kazi kwa hakika munaona vijana wengi hata walio na elimu za juu sasa hivi, hawana kazi. Na wengi sasa wamezingatia sasa wengine wamerudi mashambani wanalima. Sasa tunasema kama wakilima, ikiwa watazingatia kulima ata kuna wakati mwingine hapa tuliletewa mbegu tukalime. Na kweli tulishika mbegu tukalima na wakupanda wale walipanda walistahili wakapanda. Lakini sasa je, kuna swali moja hawakuuliza wale waliowaletea msaada kama huo. Vile vyakula tukavyolima wataziuzia nani. Ikiwa ni tomata, ikiwa ni sukuma, ikiwa ni spinach. Wataziuzia nani zile mboga. Zitakuwa zikae hapo masokoni zioze. Zitakuwa zinaoza hapo. Ama mnaweza kufikiria tunaweza kuletewa msaada wowote ule wa kusaidia wakulima hao wa mashamba madogo madogo.

Uwasaidie kama wakati huu wetu wa kulima tuna msimu tunalima. Kuna msimu wa maharagwe, tuna msimu wa kupanda tomato, sukuma na mboga. Lakini wakati zinakua kwa wingi, zinakosa market. Tunataka tujue hivi; kama ni mimea yetu ama mavuno yetu tunayaweza kuyauza wapi. Maanake kwa hakika mkulima anajitolea kwa moyo lakini kufika kule kuuza zile bidhaa, zinakosa mahali pa kuuza na itambidi tena aziuze kwa bei ya urahisi hata kulingana na yale mahitaji ya madawa yale aliyoyatumia na ghalama. Anakuja kuziuza kwa hivyo hivyo kwa bei ya rahisi maanake anajua nikizuiza hapa ni rahisi, nikizipeleka huko mbele zinakutana na zile za wengine. Itakuwa sasa ndio bei imeshuka kabisa.

Kufika pale ni traffic zimeshagongwa mpaka Voi. Ubebe mzigo tikiti ni hivo hivo. Sasa itakuwaje. Nitafikiria jambo lingine la

kutuletea kama ni mashini za kutengeneza kama ni tomato sauce, tunajua wakulima wa Wundanyi, area hiyo ya Ronye, kama sisi tutakuwa na kituo chetu hapa cha kutengeneza kama ni tomato sauce. Na awape wakulima moyo wa kulima, yaani wa kulima vyakula kwa wingi maanake wanajua hakiharibiki. Najua nikilima tomato zangu nikifika pale, zinapokelewa, tunatengeneza kama ni tomato sauce. Inatengenezwa ni preserved, haiharibiki. Sasa nina tomato ninakuja sokoni, ninajaribu kuziuza, kuzipiga bei, zinakuta na za mwenzangu na za yule na za yule, saa hiyo nisharudi nazo nyumbani. Nikienda nazo nyumbani, sina la kufanya. Labda nizitumie, nizitumie, zikibaki zingine zinaoza hapo. Hapo hasara yote. Sasa wanafikiriaje kuhusu jambo hilo la wakulima wale wadogo wadogo. Wengine wana mahindi. Ukifika wakati wa mahindi, wote wakaharibu labda wameivuna. Hawainunui kwa mara moja.

Jambo lingine ni kuhusu jamii na hasa kuhusu huu ugonjwa wa ukimwi. Ukimwi umemaliza watu wengi na hata hivi unazidi kuwaangamiza wengi. Lakini chanzo hasa, tumechunguza chanzo cha ukimwi ni nini? Chanzo cha ukimwi ni kutotii. Chanzo cha ukimwi kwanza kabisa ni kutotii. Na huko kutotii kunatokana na watoto ambao hawasikii wazazi wao. Watoto ambao hawasikii wazazi wao. Tangu hapo zamani, akina babu zetu walikuwa wanaoa kama bibi watatu, wanne, lakini hatukuwa tukisikia mambo haya kama ya ukimwi nini. Magonjwa labda yalikuweko kwa sababu hawakuwa na vifaa vya kuwapima, labda yalikuweko siwezi kutambua lakini ugonjwa siku hizi wa ukimwi unaletwa na kutotii kwa vijana. Na hiyo mara nyingi inatokana na wakati wa marriage.

Kuna wakati unataka kuoa msichana kama vile ni kijana, unataka kuoa msichana na unaenda kwa mzazi wako unamwambia ‘ baba unajua mimi nimempenda msichana fulani nataka nimuoe’. Sasa babako labda atakaa kwa muda na hujui ni kwa nini babako amekaa kwa muda. Amekaa, akakaa halafu akaja kukwambia “Mimi sitaki nikuone na msichana yule.” Na hukujua kwa nini alikwambia hivo asikuone na msichana yule. Ulimchukua mjinga sana ukaona labda anataka kukuingilia mapenzi yako ama nini. Kumbe yule mzazi wako ashaerevuka tabia za yule msichana si nzuri. Zinalingana na za kwako.

Sasa zile tabia za yule msichana zinalingana na za kwako ni hatari kwa maisha yetu. Basi anakwambia ‘sitaki nikuone na msichana yule’. Lakini wewe kwa kutotii, unaendelea na mapenzi yako hata mnafika kuoana. Unaambiwa na babako “Now you are free you can do whatever you wanted.” Sasa anakwambia hivyo amekuweka uhuru, sasa amekuweka uhuru ni kwamba hili neno nataka nilisema ndani ya kanisa maanake, harusi zinaozwa wapi? Makanisani. Lakini yule pastor anaoza, hana uhusiano wowote. Yeye anaozwa na harusi ile ni kawaida ya mapenzi. Lakini yeye hajui. Basi yule mtoto anaambiwa na babake “You are free to do whatever you want.” Basi yeye anaona raha sana maanake maisha yake is free. Pale nyumbani atakuwa hasikii mzazi. Basi hapo ndio sasa chanzo kinaendelea cha freedom. Sasa mtoto atakuwa hana ushauri wowote pale. Mzazi akienda hivi, hata akienda makosa kwa maana yuko free, yuko free.

Sasa yule atakuwa ni bibi yake labda ako-free na yeye ako-free vile wanavyotaka. Sasa wakati ninaketi mimi nikikuwa ninakaa, ninasikia kikapo cha wanawake wanazungumza wakasema: “There is danger of marrying a con-man and a con-woman. There is danger in life.” Na mimi nikachukulia hilo jambo manani. Nikafikiria nikasema “Ni kwa nini hawa

wanawake wamezungumza haya mambo.' Ni kweli ama ni ulongo? Lakini mimi nikija kuchunguza naona haya mambo ni ya ukweli. There is danger of a conwoman and a conman, yaani watu ambao wanaenda katika njia moja hawatakikani kuoana. Hiyo ni jambo la kwanza katika maisha. Na ukienda ukichunguza sana, all are cold blood na sasa hakuna mtu anapikia mwenzake healthwise. Healthwise hakuna mtu anapikia mwenzake. Sasa inakuwa, virusi kukuambukiza ni haraka sana. Yaani magonjwa yoyote kukupata katika mwili kuingia kwa damu ni haraka maanake hakuna kinga yeyote.

Hakuna yule mwingine anapikia mwenzake. Sasa there is danger. Hata tunataka utafanya utatuzi na hao watu wa health, wachunguze tabia za wazazi, na wakija kuchunguza tabia za wazazi, utakuta tunataka tujue kwanza na watoto. Hawa watoto wanaozaa, wanatatizika kinamna gani. Maanake kama tutawaacha hivyo hivyo watakuwa wanabomoa. Tutakuwa tunasema "Ukimwi umezidi ukimwi umezidi, unaendelea kuua, magonjwa yanazidi'. Kumbe magonjwa tunayaleta sisi wenyewe hapa.

**Com. Keriako Tobiko:** Sasa Bi. Wakesho malizia.

**Silvia Wakesho:** Kwa hivyo nasema utiifu wa wazazi na uwe. Na kwanza heshima. Nataka kwanza kuzungumzia mambo ya tuition. Tuition tuna karakana, tumejenga, karakana kila mahali. Na nilikuwa ninapendelea ikiwa kweli ni vizuri, nyumbe za tuition zijengwe za elimu kote kila mtaa za kufundisha watoto. Maanake kuna mchezo unaendelea hata hivi unaendelea na wanafunzi na walimu wanaweza kujidai kwamba wanafanya tuition lakini huku huku mchezo wa mapenzi unaendelea.

Kuja mzazi kugundua, anasema mtoto wake amekwisha kuharibika. Kumbe anaambiwa na mtoto " Mama naenda tuition." Akifika tuition ni chumbani hapo kwa mwalimu, ndio nyumba, ndio kitanda, mchezo unaendelea. Mama mzazi kuja kugundua baadaye, mtoto ashaharibiwa, mwalimu akishajua ameshafanya mess, transfer ashaenda. Kwa hivyo mambo hayo yachunguzwe sana. Na heshima tunataka baina ya wanafunzi na walimu. Wanafunzi wawe na heshima na walimu wao.

Mwalimu wako akikutukana, mpeleke mbele kwa mbele mpaka kwa headmaster. Usikae, mpaka ukaja kusema eti mwalimu amenifanya hivi na hivi na kumbe wewe mwenyewe ndio ulikuwa unayaficha ficha. Kama ulikuwa unataka kuyaweka waziwazi ungeenda mbele kwa headmaster ukamwambia "huyu mwalimu anakutukana." Anakutukana kwa sababu gani? Kama ni tuition umeenda tuition na umeenda kwa nyumba yake, anakufunza na akianza kukutukana na kukushika shika, wewe nenda kwa headmaster "Ninaenda tuition kwa mwalimu anayefundisha, lakini nikifika huko, mwalimu hana heshima na mimi." Kwa hivyo walimu tutajua vile tutafanya kama tutamwambia hiyo tuition aache lakini asiendelee na mchezo huo wa kuharibu watoto. Ninasema walimu wanakoseana heshima lakini watoto wenyewe ndio hawasemi mambo yale wanayoona ndani.

**Com. Keriako Tobiko:** Bi. Wakesho. Malizia sasa.

**Silvia Wakesho:** Kwa hivyo yangu ni hayo. Nimemaliza.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana. Jiandikishe hapo. Alvis Nyambu.

**Alvis Nyambu:** Kwa majina naitwa Alvis Nyambu Ibrahim kutoka Mwatate. Ningependa kutoa pendekezo langu kwa jinsi vile anavonikera pia. Nazungumzia kuhusu idara ya wafungwa (prisons). Prisons imekuwa na tabia wakifunga mtu mfungwa halafu kwa bahati mbaya aadhiriwe pale akiwa jela huwa mpaka arejeshwe nyumbani kuja kuzikwa.

Jambo la pili ningependelea Serikali iwe ya majimbo na sio majimbo tu bali majimbo ya kiuchumi. Rasilimali zetu ama rasilimali za huyu mwananchi pahali alipo zihakikishiwe mwananchi mwenyewe. Huduma za afya ziwe za bure. Siku hizi zasumbua sana. Mtu akiwa mgonjwa ni kushughulika huko na huko. Imekuwa hata mpaka madaktari wamegundua madawa ya Serikali watayaweka halafu wapeleke kwa clinic zao. Pia madaktari ambao wanafanya hospitali za Serikali, wasiruhusiwe kuwa na clinic zao binafsi.

Elimu iwe ya bure kwanzia kiwango cha Primary hadi chuo kikuu ili wananchi wote wa Kenya wapate kuerevuka. Rasilimali zetu kama misitu, madini, na mashamba ama ardhi yahakikishiwe zile za mtu wa asili ama yeye mwenyewe ndiye anaweza kuzihifadhi, awe anazitunza. Nazungumza kuhusu mambo za kura. Wakati kura kama zapigwa, ningependekeza, kura ziwe zikihesabiwa katika vituo vya kupigia kura pale pale. Hesabu ndio ipelekwe kule kwa kuhesabiwa, wahesabu peke yake.

Kuna kifungu cha Katiba ya sasa kinachosema, Mkenya anaweza kukaa mahali popote pale akiwa hata kama ametoka wapi. Ningependekeza kiondolewe na kiwe kinyume chake. Kama mimi Mtaita niwe naweza kukaa Taita na nikajivunia mimi ni Mtaita niko Taita. Sio ya kwamba iwe mtu atatoka kwingine na aje huku kuja kunisumbua na kumiliki ardhi tusumbuane. Kila mtu ana mipaka yake.

Nazungumzia kuhusu walemavu ama watu walio na ulemavu. Wapewe haki zao zote za kimsingi. Kama elimu, kazi na waheshimiwe na kujengewa maghorofa. Kuwe kikatiba, kuwe kunajengwa nyumba za maghorofa ambazo zinaweza kufikiwa na walio na ulemavu kwa urahisi. Isiwe inajengwa kwa stairs mpaka mtu ambaye hawezi kupanda na ile wheelchair itakuwa vigumu afike kule juu. Iwe kiasi ambako anaweza kufikia kama ni ofisi fulani ataka kufikia kule juu kwa ghorofa.

Pia na hapo hapo vibanda hivi vya kupigia simu, telephone booths, walemavu wengi hawawezi kupiga simu kwa kutumia hizi booths ambazo ziko kwa saa hii. Kuwe na uhuru zijengwe kiasi ambako zinaweza kufikiwa na mtu mlemavu. Zinajengwa juu, ziwe at least za chini kidogo. Kuwe na heshima kimavazi, kikatiba. Wasichana ama wanawake wasiruhusiwe kikatiba kuvaa nguo ama suruali ndefu ambazo zinawabana na kuonyesha uchi wao. Kwani wengine wanazivaa na kuonywesha, ku-display the body. Kwa hivyo hiyo ni makosa. Hata kwa kimila si sawa. Hilo hilo lafuatia mwanamke, iwe kikatiba, akivalia nguo isio msitiri uchi wake kikamilifu, akinajisiwa, mnajisi asihukumiwe maanake ni kama kujitakia mwenyewe.

Kuhusu bangi: Mimi kama dini yangu inavyoniruhusu ama madawa yote yale ya kulevya ama madawa yeyote mabaya,

yasiruhusiwe, si halali. Ama hata zichunguzwe, yana uwezo gani yana uwezo gani. Kuwe ni kisababu. Ikatazwe kabisa, bangi isitumike ama ulevi wowote ule kwani zinaharibu wananchi wengi hata watoto. Vijana kwa wazee, wanaharibika kwa hiyo bangi. Wakuta ngumi zaendelea barabarani sababu ya bangi. Kikatiba biashara ama tabia ya umalaya na ushenge ipigwe marufuku kabisa. Kwani hiyo hiyo ndiyo yaeneza na kuchochea kupatikana kwa ugonjwa na kueneza ugonjwa wa ukimwi. Yangu ni hayo mafupi. Asanteni.

**Com. Keriako Tobiko:** Sawa. Utatupatia hiyo karatasi. Asante sana ndugu yangu. Claudea Ngwayi.

**Claudea Ngwayi:** Mwenyekiti na ma-commissioners wetu. Mwenyekiti wetu wa baraza la wilaya na maofisa wote mliofika hapa kwa Katiba. Hamjambo. Yangu kwanza naomba hivi; iandikwe katika Katiba hii yetu mpya kwamba kuwe na elimu ya bure kwa wanafunzi kwanzia Nursery hadi kidato cha nne. Lakini kwa walemavu iendelee kwanzia nursery hadi university level. Halafu wanapomaliza university level, wajengewe Jua-kali sheds zao na wawe wanaweza wakaunda kama kazi za mikono na vitu ambavyo watakavyotengeneza. Pia kuwe kuna shirika maalum ambalo litabuniwa na Katiba liwe la kikatiba la kuwauzia vifaa hivyo. Kama kwa mfano majiko.

Halafu rasilimali aina yeyote ile, madini, gemstones, wildlife, marine life ambayo imepatikana kutoka eneo fulani, tuhakikishiwe na Katiba mpya kwamba rasilimali hiyo kabla haijakwenda kwa Central Government imetumika hapo hapo kwa mwananchi yule yule wa mahali ambapo imepatikana. Kiwango fulani kiende kwa Serikali Central Government lakini kiasi fulani kiachwe. Hata kama ikiwezekana 50% of whatever is got there, iachwe hapo hapo. Sehemu ya National Park, tunaomba Katiba mpya tunayoibuni leo iwe inaweza yaani wasukume kidogo kama 10% of whatever land they have, hii National Park.

Halafu iwe allocated kwa mwananchi halafu igawanywe upya na jamii. Na kwa mimi mwananchi na mwingine na mwingine, nisiruhusiwe na Katiba kuwa na ardhi ambayo inazidi acre hamsini ambayo ni ardhi yenye rotuba wakati ambao wananchi wa hapo mahali hawana hata acre moja.

National Park: Tunaomba tuirudishe iwe Game Reserve. Pia napendekeza ofisi ya DC ama Dc mwenyewe asiwe yeye ndiye mwenyekiti tena wa District Development Committee bali ofisi hiyo iachiwe chairman of the county council wa mahali hapo. Ambapo yeye ndiye atakuwa kama chairman wa DDC. Na huyo chairman wa county council atakuwa amechaguliwa na mwananchi. Cheo cha waziri mkuu kibuniwe. Ili waziri mkuu awe ni kiongozi wa Serikali na Rais teule atakuwa ni kama vile tunasema ‘ceremonial President’ ambaye ataongoza taifa.

Wazee wenye miaka sitini na tano na kuendelea waweza kuangaliwa kidogo na Serikali. Wawe na earning scheme ya kuwasukuma wakati wakingojea siku zao za mwisho. Walimu wa shule za msingi (primary school teachers) tunaomba pia Katiba iwekwe kwamba wawe wakivaa sare au uniforms. Wawe wakijulikana.

Wafanyi kazi wa Serikali au civil servants, wakishafikia ule umri wao wa kustaafu, isiwe tena ati inakubalika rahisi au kwa njia yeyote ile mfanyi kazi yule wa Serikali anaweza akarudishwa kusimamia ofisi yote ya umma kama hizi government corporations ama hizi Parastatal bodies. Awe akisha-retire, ame-retire na anaenda nyumbani kuzungumza.

Walimu wa nursery. Umekuwa ni mzigo sana kwa wananchi. Tunaomba kubuniwe kakati fulani ili kwamba walimu wa nursery wawe wakilipwa na baraza la wilaya la mahali ambapo mwalimu anafundishia county council ama municipal council. Wale wenzetu wanaokuja ambao si Wataita wanatutembelea, ni Wakenya wenzetu tunawakaribisha. Waje kama wafanyi biashara lakini wasiwe kama mabwana wakubwa wanakuwa na hadiri kubwa kuliko mimi mwenyeji ambaye nimezaliwa mahali hapo.

Katika kifungo cha Katiba kinachosema 'mimi nikiwa na sehemu ya ardhi, ni ardhi yangu ni mali yangu tu kwa kimo cha futi tatu ' halafu kile kinachopatikana zaidi ya hizo futi tatu ni ya Serikali kiondolewe. Iwe chochote kinachopatikana zaidi ya hizo futi tatu, kama si changu kiwekwe ni cha jamii halafu jamii itaamua itakuwa vipi.

Mpango wa Primary school feeding programme tunaomba uendelee na unapoendelea, tusitegemee sana ile tunaletewa na wafadhili. Tuwe tuna njia ambayo tutabuni ama itabuniwa na Serikali kupitia kwa Katiba ambayo tunaunda leo. Huo mpango uwe ni wa lazima.

Halafu mwisho sehemu moja au sababu pia ya kuenea kwa huu ugonjwa wa ukimwi ni huku kuhalalisha matumizi ya *condoms* kiholela holela. Vile naambiwa ni mapenzi ya kiholela holela inachangia ukimwi, pia na yale matumizi yake ya *condom* kiholela holela. Tunaomba hivi, zizipeanwe kama mtu hajachunguzwa amekomaa ila tu watu ambao labda kwa sababu fulani fulani hivi, kama wameshindwa kupanga uzazi wakubaliwe. Maana haya matumizi yamekuwa hata ukitembea njiani, unakuta *condoms* njiani. Ni hatari hasa kwa watoto wadogo ambao hawajui hiyo ni nini mpaka wengine wanafikiria ni vibofu wanapuliza. Sasa tayari ameweka mdomoni, ameshika.

Halafu pia yale matumizi kama zimewekwa mahali tuseme shuleni ama hospitalini, kwa mtu yeyote aende avute atoe. Hivyo wengine wanavuta wako under-age. Nikisema under-age ni vijana ambao ni below eighteen years. Sasa tukiwakubali ikiwa wataendelea na mambo hayo au na matumizi hayo, ni sawasawa na kumpatia mtoto wa miaka kumi bastola halafu umwambie lenga. Ataitumia vile anavyopenda. Asanteni.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu. Jiandikishe pale. Sasa kuna mtu yeyote ambaye angetaka kuongea na hajatajwa? Any person who would wish to speak? Okey. Hakuna. Basi wacha nimwite chairman wa Constitutional Committee wa hapa, atufungie mkutano huu na maombi. Ako wapi? The chairman of the committee. Or any member of the committee if the chairman is not there.

**Clara Sally Juma:** Basi kwa niaba ya hawa commissioners wetu waliofika hapa na kwa niaba ya committee hii ya Mwatate

Constitution na nyinyi wananchi kwa ujumla, ningependa kuchukua nafasi hii, kuwashukuru wale wote mmefika hapa na kutoa maoni yenu kwa moyo mkunjufu hata bila kuogopa. Na kwa sababu hiyo, mumetoa maoni yenu, ningependa kuwashukuru katika hali ya kuvumilia pia. Mumevumilia tangu asubuhi hadi sasa, mko nasi hapa. Kwa hivyo wananchi kutoka Ronye kutoka hapa Msau, kutoka Rong'e kati na sehemu zingine mbalimbali, wale ambao wamefika hapa nawashukuru sana.

Na hivyo hivyo ningependa kuwafahamisha kwamba kesho commissioners hawa watakuwa Mwatate, Kenyatta High School, kwa wananchi wote wa Mwatate. Kwa hivyo hata kama umetoa maoni yako hapa leo na una haja ya kufika Kenyatta High School kesho unakaribishwa. Kwa hivyo usione uoga ama kama umezungumza mengine na mengine umesahau ukifika nyumbani unaanza kufikiria mengine labda hujazungumza. Basi karibu tena Mwatate kesho, kuzidi kutoa maoni ya kuendeleza kujenga taifa letu la Kenya.

Kwa hivyo tunawakaribisha Mwatate kesho kwanzia saa mbili kamili hadi saa kumi na mbili. Na huenda ikawa labda kesho umati wa watu utakuwa na si ajabu kazi itakuwa kubwa. Kwa hivyo mwenzangu ningetaka kukufahamisha ukiwa una moyo wa kufika hapo, fika mapema kwa sababu wengi wanatarajia kufika kesho na kutoa maoni yao.

Pia jambo lingine ni kwamba ningependa kuwashukuru, Chiefs wetu na Assistant Chiefs kwa kuwaleta wananchi kwa pamoja na matangazo ambayo yamepita huku na pale na hawa Commissioners wetu wamefika na wakaona watu kwa ujumla. Kwa hivyo, kwa haya yote, nawashukuru sana na kwa sababu muda umeenda ijapokuwa wakati uko lakini kwa sababu wananchi wenyewe mmeshaisha katika hali ya kutoa maoni yenu, ni kwamba tungetaka kufunga sasa. Mwenzangu, unanyosha mkono unataka kuongea lolote?

Tulikuwa tumeambiwa kwamba Commissioners watakuwa hapa mpaka saa kumi na mbili na kuendelea………(inaudible).

**Clara Saru Juma:** Ni kwamba labda kidogo tu, ni kwamba tafadhali hata kama wako hapa mpaka saa kumi na mbili lakini ile si saa kumi na mbili nikumaanisha kwamba kama list ingekuwa hivi sasa ingali inaendelea na kuandikishwa, unaona? Na watu wanazidi kuja kuendelea kuandikisha. Basi wako hapa hadi saa kumi na mbili. Lakini kwa kuwa umekuja na muda ulikuwa umeshaisha unakaribishwa kuja kutoa maoni yako, usianze kuchapa mbio kesho huko Mwatate. Na kama kuna mtu yeyote huko nje tafadhali ana haja ya kutoa maoni, Commissioners wanataka kuondoka na tusianze kuwapiga break halafu tena huku tuendelee tafadhali. Karibu.

**Ronald Mshimba:** Jina langu ni Ronald Mshimba, Councillor hapa Msau. Changio langu ambazo labda ningetaka kutoa katika hii hali ya uandikishaji wa Katiba ni kwamba ningesema katika vyama vya kisiasa vyote vighalamiwe sawa. Vijaribu kughalamiwa sawa kutoka kwa fedha za umma. Katika muundo na aina za Serikali, ningetaka kusema kuwa wakuu wa wilaya na wakuu wa departments mbalimbali wilayani wawe ni wakaazi wa wilaya ambao waelewa maswala ya wananchi hao.

Wakuu wa Serikali za mitaani wawe na uwezo mkubwa. Hii ni kusema kuwa Provincial Administrators kama DC wajaribu wapokonywe nguvu zao zile za kuweza kuingilia kama ni masilahi kama ya wakulima. Nafikiri kuna wakati DC amekuwa na nguvu kubwa unasikia anasema labda kuhusu hizo kitu fulani. Wakulima wasiuze kama anasema ni mahindi choma ama kitu kama hiyo. Tunataka nguvu kama hizo zipunguzwe na msinichukulie labda naongea hali ya majimbo ama nini. Nikisema wakuu wa wilaya wawe ni wakazi wa pale, sisemi labda Mkikuyu asiwe hapa. No, professionals wawe kote lakini wakuu kama wa wilaya na departmental heads wawe ni wenyeji wa pale ambao wanaelewa masilahi ya pale, wanaweza kushughulikia zaidi watu wa pale.

Bunge: Wabunge wapewe nguvu zaidi. Kuna wakati tunakuta kuwa Bunge labda wamepitisha kitu, mswada fulani kama huu wa juzi sana wa mnazi, lakini Rais analalia upishaji huo wa Bunge. Wabunge wanasema kitu lakini inatokea kuwa Rais kwa vile ndiye anakuwa na nguvu zaidi, anakataa mapendekezo ya mswada huo na inabidi iwe hivyo hivyo. Suggestion yangu ni kwamba Bunge ipatiwe nguvu kubwa kushida Rais. Rais apokonywe ule uwezo wa kuwa yeye ndiye anaamua kila kitu.

The public wawe na power ya kupigia MP vote of no confidence ikiwa atapatikana na makosa kama vile ya ufisadi ama immorality na kadhalika. Mishahara ya wabunge: Wabunge wasiwe na uwezo wa kujiongeza wenyewe mshahara. Hivyo ni kusema kuwa Bunge labda wanaketi dakika tano halafu wanasema wanapitisha nusu milioni. Kuwe na tume maalum ambayo inaweza ikaangalia juu ya mishahara ya wabunge. Na hao wabunge wa nominated MPs, ningependekeza kuwa kusiwe na nominated MPs maanake sanasana hii imeendelea kupuzwa, watu wanachagua marafiki zao. There should be no nominated MPs.

Rais pia asiwe na uwezo wa kuvunja Bunge. Labda uwezo huu upatiwe speaker ama tume maalum lakini asiwe na nguvu hizo kibinafsi. Mamlaka ya Rais: Rais awe ni mtu ambaye labda tunamchagua yaani kumewekwa kiwango fulani cha elimu, miaka na moral standards zake ziangaliwe na past history. Awe vetted na kama Parliament namna hii. Ama kuwe na committee fulani ambayo inaweza ikam-vet, wa-vet mtu ambaye anastahili kuwa Rais.

Rais aweze kuondolewa mamlakani atakapopatikana na kosa kama la ufisadi, immorality, kutumia mamlaka vibaya. Provincial Administration: Provincial Administration ningeomba labda machief, ni suggestion yangu, Ma-DC, DO, Chiefs, Assistant Chiefs, warudi nyumbani kwa maana hakuna kazi ambayo wanafanya ya maana. Hizo duties zao ambazo wamefanya zimeendelea kulingana na kushikana sana na viongozi wa mitaani. Ni kama hapa mtaani unaweza ukashindwa ukiwa una swala, labda utapata Councillor ama utapata Chief. Lakini Chief kwa vile kutokea zamani, crown imekuwa ni kubwa, maswala ya Councillor anachukua. Na hata ukimuuliza Chief jana alikuwa akifanya nini ama Sub-chief, sanasana huwa hawajui walikuwa wakifanya nini ama anything of what they do. Kwa hivyo hizo kazi zao, wale Councillors wa viongozi wa Serikali za mtaani, wawe powered zaidi na nguvu zao zirejeshwe chini.

Mahakama. Maofisa wa mahakama wachaguliwe. Wachunjwe na Bunge ama tume maalum. Wawe ni watu ambao

wamechunjwa wakaangaliwa hali ya elimu yao, moral standards, nafasi zao ziwe nzuri. Waruhusiwe kuwa ukiwa labda umepelekwa kortini uwe una ruhusiwa kuweka rufaa kwa kila kitu. Hata kama utakuwa umefanya capital sin, uwe unaruhusiwa kukaa nje, upatiwe ile right yako ya kukaa nje ndio uendelee kujitetea. Sio kwambia umewekwa kizuizini kabla hujakuwa proven guilty na bado unaanza kuteswa.

Serikali za mitaa: Mayor na wenyekiti wa Serikali za wilaya wawe ni watu wamechaguliwa moja kwa moja. Sio kwenda kuchaguliwa na madiwani waliochaguliwa. Inakuwa wamechaguliwa na watu kidogo. Watu ambao sana sana unakuta hiyo campaign hutembea sana, wale wenye pesa ndio wanaunganaungana wale ma-councillors wengine halafu wanachukua hizo viti. Nafikiri hiyo ni moja kwa moja. Kiwango cha elimu pia cha ma-mayors, moral standards zao na past history ziwe ni vitu zinachunguzwa sana.

Serikali pia ifikirie ijaribu kujitoa katika maswala ya local government ya Serikali za wilayani. Maanake unakuta katika let's say City Council, Municipal Councils, County Councils, the chief Accounting Officer ama the Chief Labour Officer yule wakuangalia sana maswala ya pesa na hilo eneo, anakuwa ni ofisa wa kutoka kwa Serikali. The Town Clerk, the County Clerk nini na nini?

Kwa hivyo unakuta wale watu ambao wamechaguliwa na wananchi wa kuangalia labda maswala ya fedha za pale, wanakuwa hawana uwezo mkubwa kushida yule mteuliwa ama bwana kiongozi wa Serikali ambaye amewekwa pale kuangalia swala hilo la fedha na labda la kisheria. Kwa hivyo wale ma-councillors wenyewe hawana nguvu ya kufanya mambo yao bila ya huyu bwana ambaye ametoka kwa Central Government.

**Com. Keriako Tobiko:** What is your recommendation on that? For the Chief Officers.

**Ronald Mshimba:** The Chief Officers?

**Com. Keriako Tobiko:** Yes.

**Ronald Mshimba:** They should be de-linked. The Government should be de-linked from the Administration of the Local Government. That is to say, even the Chief Officer, the Chief Legal Officer and the Chief Accounting Officer who is usually the clerk should not be there. That post should be…..a sorting should be done to see to it that, that post is created and heard by somebody within the council. Not a nominee by the Government.

**Com. Keriako Tobiko:** They be appointed by the Councillors?

**Ronald Mshimba:** Whatever, whichever way to define but not …

**Com. Keriako Tobiko:** Not from the Central Government.

**Ronald Mshimba:** Yes, not from the Central Government. Rais awe waziri wa Serikali ya mtaa na awe na uwezo ndio wa kuvunja mabaraza. Avunje mabaraza, iwapo kunashukiwa kuwa kuna ufisadi katika mabaraza hayo ama kuna gross mis-performance. Kuwapo uhakikisho kwamba baraza halishughulikii maswala ya wale watu waliowachagua. Hapo basi iwe waziri ama anayeshughulika na Serikali za Ulaya, anaweza akavunja.

Haki za kimsingi: Tungeomba usalama. Kuwe na police patrols, kuwe na police posts zijaribu ziongezwe ili tuwe na usalama. Katika hali ya afya iwe iko bure. Ile cost-sharing ambayo tunafanya na sisi tunaendelea tu kufa sana. Umaskini umeendelea kuzidi na hata hiyo pound tunaitishwa, wengi nafikiri hatuna. Kwa hivyo afya iwe ni ya bure na tujaribu iwe karibu. Zile kama ni dispensaries, zijaribu ziongezwe. Maji pia iwe karibu, iwe bure ama iwekwe kwa kiwango ambacho kinafaa Wakenya ambao uchumi umewachapa ikawa hawana mengi.

Haki za watoto: Watoto wasipigwe, wasitumishwe, wapewe uridhi wafikapo miaka kumi na nane. Haki ya ardhi na mali: Nafikiri vitu kama madini ziwe ni vitu ambazo zinasimamiwa sana na Serikali za mitaani. Watu wa Serikali za mtaani wawe wana nguvu zaidi ya kusimamia mali ya asili, kama vile madini. Kuwekwe sheria ya kulinda misitu. Kuwe na sheria labda ambayo itaangaliwa iwe inafuatwa na bado iwe ni watu wa locals wenyewe wafanye mpango ndio misitu isikatwe. Misitu isikatwe. Miti iendelee kupandwa. Chenicheni za maji zilindwe yaani water catchment areas zijaribu zilindwe siziwe encroached. Tunaona huu ukulima kuzidi kwa population, saa zingine corruption tuna-encroach mpaka water catchment areas. Zinafaa zilindwe.

Katika hali ya ukulima, yaani, Agriculture. Agriculture hapa Pwani, tunataka mnazi uhalalishwe, yaani uwe legalized. Maanake unasaidia kiuchumi eneo hili la Pwani. Land tungeomba title deeds, Coast Province nafikiri imebaki imekuwa kama most of it ni trust land, government land, imekuwa ni for grabbing. The locals should be given title deeds. If these title deeds lasts for forty years for now since independence, there isn't much we can do without them.

Industries: Industries tujaribu tuone labda zinazambazwa mtaani. Katika 75%-80% ya population ya Kenya tunaona inaendelea kuishi vijijini. Kwa hivyo kusiwe ile hali ya congestion in towns. Tungependa viwanda viizidi kusambazwa huku mtaani ambapo kuna sitima na kila kitu. Kuwe na one man one job. Hii shida ya kazi, unakuta chairman yuko huku, chairman, chairman, chairman one person. Kwa hivyo one man one job.

**Com. Kabira:** One woman?

**Ronald Mshimba:** When I am talking of one man, I mean human beings. Mtu mmoja afanye kazi moja. Asante sana.

**Com. Keriako Tobiko:** Asante sana ndugu yangu.

**Clara Saru Juma:** Kwa sababu sasa tunaendelea kumaliza ni kwamba ningemuomba mzee wetu hapa ambaye ni mwenyeji wa hapa, aje atufungie kwa maombi. Na wale ambao mmevumilia mkawa pamoja nasi, nawashukuru. Na baba wakati unaomba, ni kwamba hawa wageni wetu ambao wamefika hapa, wako pamoja nasi, ujaribu kuwakumbuka katika safari ya kesho na kazi ya kesho. Na katika hali hii ya kurekebisha Katiba, ni kwamba Mungu atupatie Katiba mpya na Katiba nzuri ile ya kutulinda sisi wananchi pamoja na haki zetu. Mzee wangu karibu. Kwa majina naitwa Bi. Clara Saru Juma, ni Councillor wa Chavia ward na pia ni mwanakamati wa Mwatate Constituency.

**Dilvan Munyaji.** Nafikiri ningeliomba kwa kumheshimu Mwenyezi Mungu, tusimame sote. Hata walio nje, wasimame na watulie mahali walipo ili tuweze kumtolea Mungu shukrani kwa vile ametuweka mpaka wakati huu.

**Maombi.**

Mungu wetu tunakushukuru kwa vile tumeanza na wewe na sasa tunafikia nafasi ya kumaliza na wewe. Tunasema ni asante.Asante kwa maofisa wetu ambao umewaleta kutoka mbali na zaidi ni kwa Serikali yetu hii tukufu ya Kenya, kwa kutatua matatizo ambayo tuko nayo sisi wananchi. Yote Bwana tumekuachia, yale yote tumezungumza Bwana. Tunataka ututumie wewe na uweze kuyatekeleza wewe kwa sababu wewe ndio mweza wa yote. Sisi ni binadamu tu. Tunazungumza na tunapanga lakini wewe unajua. Sasa tumefika wakati wa kuachana lakini Baba tumewachana kimwili lakini kwa kiroho tuwe pahali pamoja. Na waweka mkononi maofisa wetu ambao wako mbele yetu na zaidi ya yote Bwana nimewakabidhi mkononi wakati wanapoondoka kwa sababu wanaenda na chombo ambacho kimeundwa na mwanadamu. Tunataka wewe uwe dereva na uwaongoze mahali waendako wafike salama salamini. Na hali kesho tena wako hapo kwa mambo kama hayo, twataka Baba uwaongoze na uwalinde. Hata kwa safari yao, wapeleke Baba na hata sisi hapa tulioko ambao wengine tumetoka mbali na karibu tunataka uwe mlinzi mwema, umpeleke kila mmoja mahali ametoka afike salama salamini. Baba tunashukuru kwa sababu siku ya leo ilikuwa siku ya furaha na mambo yote tumeyakabidhi mkononi mwako, mapenzi yako yafanyike.Tunaomba haya machache, na yale ambayo tumeacha Baba utuombee. Naomba hayo machache kwa jina la mwanaye Yesu Kristu Bwana wetu. Asante.

Meeting ended at 6.00 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**